

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Nne – Tarehe 10 Novemba, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, leo tunaanza kama kawaida Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 39

Hospitali ya Wilaya

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Wilaya za Kakonko, Buhigwe na Uvinza ni Wilaya mpya ambazo hazina Hospitali za Wilaya.

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali za Wilaya katika Wilaya hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imeidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 500 kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 1.5 hadi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imetenga eneo la ekari 80 na imekamilisha michoro ya Jengo la Hospitali ya Wilaya. Halmashauri imeshauriwa kuweka kipaumbele na kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa kuanza na jengo la wagonjwa wa nje, utawala na maabara unaogharibu shilingi millioni 450. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imetengewa shilingi milioni 500 kuendelea na ujenzi. Kazi hii inatekelezwa na SUMA JKT na kazi inaendelea. Ujenzi wa hospitali unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 6.4 hadi kukamilika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Genzabuke.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Kakonko kwa sasa wanapata huduma katika Kituo cha Afya cha Kakonko na kituo hicho kimezidiwa kwa sababu msongamano wa watu

ni mkubwa. Kituo hicho kinahudumia wananchi kutoka hadi Mkoa jirani wa Kagera kwa maana ya wananchi wa Nyakanazi, Kalenge pia na wakimbizi kwa sababu katika Wilaya ile kuna kambi za wakimbizi, Waziri amesema kwamba mwaka 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 500.

Je, Waziri yupo tayari sasa kutokana na jinsi wananchi wanavyopata shida pamoja na waganga na wauguzi kwa sababu watu wakiwa wengi waganga nao wanachanganyikiwa, yupo tayari kufuatilia hizo shilingi milioni 500 ziweze kwenda mara moja Kakonko kwenda kuwasaidia wananchi? (*Makofi*)

Swali la pili; kwa wakati huu ambapo Wilaya ya Uvinza haina Hospitali ya Wilaya, wananchi wanapata huduma katika vituo vya afya na zahanati, lakin vituo hivyo vya afya pamoja na zahanati havina watumishi wa kutosha.

Je, katika mgao huu wa wafanyakazi ambao wataajiriwa kwa sasa, Serikali iko tayari kabisa kupeleka watumishi wengi wa kutosha kwenda kusaidia katika Wilaya ya Uvinza ambayo haina Hospitali ya Wilaya? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Genzabuke kwa jinsi ambavyo anafuatilia huduma hasa kwa wanawake katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, napenda kumthibitishia kwamba fedha hizo ambazo zimetengwa kwenye bajeti ya 2017/2018 nitazifatilia na kuzisimimamia mimi mwenyewe binafsi kuhakikisha kwamba zimekwenda haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, wiki hii iliyopita tumekamilisha upatikanaji wa watumishi 2,008 ambao sasa hivi wanaendelea kugawanywa katika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Halmashauri mbalimbali. Leo hii nitahakikisha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imepata watumishi wa kutosha angalau kwa mahitaji ya asilimia 50. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni moja ya Halmashauri ambayo haina Hospitali ya Wilaya na tuna vituo vya afya vinne, kituo cha afya kimoja cha Lupembe ni cha zamani, hivi karibuni tumefungua chumba cha upasuaji tayari *operation* zinaendelea pale. Tuna Kituo cha Kichiwa ambacho tunatarajia pia tuwe na *theater* ili kuwahudumia akina mama wasitembee umbali mrefu kwenda Kibena.

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kujenga au kuanzisha chumba cha upasuaji ili akina Mama katika Kituo cha Afya cha Kichiwa ili akina Mama wasisafiri umbali mrefu kwenda hospitali ya Kibena ambayo ipo mbali sana na wanapoishi ambapo Jimbo la Lupembe lipo. Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri wa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Ungando.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kituo cha afya cha Kichiwa kumbukumbu zangu katika programu yetu ya vile vituo vya afya vya kwanza 172, katika vituo vile kuna fedha ambazo tulipata kutoka Canada, fedha zile zimeshaendelea katika maeneo mbalimbali na baadhi ya vituo sasa hivi wameshafika *level* ya renta, lakini kuna zile fedha kutoka *World Bank* ni kwamba upelekaji wake wa fedha utakamilika ndani ya wiki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba wananchi wako watarajie kwamba jinsi gani waweze kushiriki kazi lakini fedha zile tutatumia *force account*. Niwasih i hasa viongozi wetu huko katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, zile fedha zinapokuja lazima wazisimamie vizuri tupate *value or money* na wananchi waweze kupata huduma. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ungando.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Halmashauri ya Kibiti ni Halmashauri moja ambayo imetoka Wilaya ya Kibiti na kituo chake kikubwa cha afya Kibiti lakini hivi sasa Kimezidiwa kutoa huduma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Hospitali ya Wilaya ya Kibiti? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hoja anayoizungumza Mheshimiwa Ungando ni hoja ya kweli na kwa sababu nilikuwa naye katika vile visiwa 40 vya Delta kwa kutwa nzima na changamoto ya afya kule ni kubwa sana, ndio maana katika kipindi cha sasa tumepeleka fedha katika kituo cha afya kimoja ambacho mimi na Mheshimiwa Mbunge tulizunguka mpaka usiku pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la progamu ya uanzishaji wa Hospitali ya Wilaya ya Kibiti, naomba nikusihii Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana kwa pamoja kwa sababu lengo letu kubwa zile Wilaya zote zilizokosa hospitali sasa tuweze kuwa na progamu maalum kwa ajili ya kujenga hospitali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ungando naomba nikupe faraja kwamba tutashirikiana kwa pamoja tuangalie *way forward* tunafanyaje tupate Hospitali ya Wilaya ya Kibiti kwa sababu *population* ya watu pale ni kubwa hasa ukiangalia barabara ya Kilwa lazima tuhakikishe kwamba tunafanya jambo hilo kwa haraka. (*Makofii*)

MWENYEKITI:Ahsante, Mheshimiwa Almas.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Kwa vile matatizo haya ya afya katika Wilaya ya Kakonko yanafanana sana na ukosefu wa Hospitali ya Wilaya ya Uyui na Wilaya ya Uyui tumejitalidi kupitia Halmashauri kujenga hospitali lakini tumeishia kwenye *OPD* na tungeomba Serikali ituambie; je, inaweza kutuongezea hela ili tuweze kumalizia *OPD* yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pale hawana Hospitali ya Wilaya na wameanza programu ya ujenzi wa *OPD*, lakini sasa hivi tunafanya *needs assessment* katika maeneo yote ambayo majengo yalianza bado hayajakamilika. Ndiyo maana katika harakati zetu sasa hivi tunakamilisha Kilolo, Mvomero lakini tunaenda kule Siha ninaamini kwamba Uyui. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mchakato tunaofanya hivi sasa na wataalam wangu pale ofisini tutaangalia nini tufanye, lengo kubwa tuikamilishe hospitali yetu ya Uyui na wale Wanyamwezi wa Tabora pale waweze kupata huduma kama Wanyamwezi wengine hapa Tanzania. (*Makofi*)

Na. 40

Mpango wa Elimu Bure

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y MHE. YOSEPHER F. KOMBA) aliuliza:-

Ni dhamira ya Serikali kutekeleza mpango wa elimu bure kuanzia chekechea hadi kidato cha nne, lakini mpango huu una changamoto ambazo zisipotatuliwa zitasababisha kushuka kwa ubora wa elimu.

(a) Je, ni nini tamko la Serikali juu ya wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza kwa kigezo cha kutofaulu kwa kiwango cha kianzia alama 100 na kuendelea?

(b) Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha ujenzi wa maabara unakamilika kwa wakati?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la Serikali ni kwamba mwanafunzi anahesabiwa kufaulu mtihani wa Taifa wa darasa la saba endapo atapata alama kuanzia 100 hadi 250 katika masomo yote aliyoayafanya. Hata hivyo, wanafunzi walio na alama chini ya 100 huhesabika kuwa ni miongoni mwa waliokosa sifa za kuijunga na kidato cha kwanza katika shule za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wanafunzi walioshindwa kufikia alama 100 na kuendelea, hushauriwa kuijunga na mfumo usio rasmi wa Elimu Masafa (*Open Distance Learning*) unaosimamiwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, vyuo vya ufundi au shule za sekondari za binafsi. Wanafunzi wanaojunga na mfumo huo wa elimu hawamo katika utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa elimu msingi bila malipo, lakini wanafunzi wanaosoma katika utaratibu huo watakaofaulu mtihani wa Taifa wa kidato cha nne huchaguliwa kuijunga na kidato cha tano katika shule za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii la (b); ujenzi wa maabara katika Halmashauri zote unaendelea ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia masomo ya sayansi. Kati ya maabara 10,387 zinazohitajika nchini, ujenzi wa maabara 6,287 sawa na asilimia 60.5 ya mahitaji umekamilika.

Nazikumbusha Halmashauri zote kukamilisha mapema ujenzi unaoendelea kwa kushirikisha wadau na nguvu za wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sera ya Elimu Bure imewasaidia baadhi ya wazazi wasio na uwezo kuandikisha watoto shulen, lakini wakati huo huo bado kuna michango kadhaa inayoendelea kwa baadhi ya shule na michango hii imerudisha nyuma morali ya wazazi kuchangia kwa juhudi katika maendeleo mbalimbali ya shule.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa elimu kwa wananchi kwamba sera ni elimu bila ada na siyo elimu bure ili kuwafanya wananchi waweze kuchangia kwa nguvu kama illiyokuwa zamani? (*Makof*)

Swali la pili, shule za Sekondari za Keni, Shimbi na Bustani katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ni shule ambazo zimejengwa kwa mtindo wa ghorofa kwa sababu ya uhaba wa ardhi katika Wilaya ya Rombo na sasa zina muda karibu wa zaidi ya miaka 10 wananchi wameshindwa kuzikamilisha.

Je, Serikali ipo tayari katika bajeti ijayo katika bajeti ijayo kuzipokea hizi shule na kuzikamilisha ili kuweza kuunga mkono nguvu za wananchi katika jithada zao za kufanya maendeleo mengine kama kumalizia maabara?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Upendo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubalina na Mheshimiwa Selasini kwamba kuna michango ambayo inaruhusiwa. Lakini michango ile ina utaratibu kwamba ili kusudi mchango uweze kukubalika kisheria ni lazima Kamati ya Shule au bodi ya shule iwe imeujadili na kupeleka kwa wadau ambaeo ni wazazi,

wakipitisha wanaomba kibali kwa Mkuu wa Mkoa, wakipata kibali basi hapo wanaweza wakaendelea na kuchangishana. Huo ni utaratibu ambao ni mzuri, namshauri Mheshimiwa Mbunge autumie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili, sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu tupo tayari kukaa na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujadili namna ambavyo tunaweza tukaboresha utaratibu wa kuzikamilisha hizi shule ambazo anazzungumzia. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Upendo, halafu Mheshimiwa Waitara.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Katika suala la elimu bure, moja ya changamoto ni pamoja na utoro unaowakabili hasa watoto wa kike. Sasa ningependa kujua Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali sasa ina mpango gani kuhakikisha ya kwamba watoto wa kike wanaoingia shuleni wanabaki shuleni kwa kumaliza, kwa Serikali kuweka pesa za ruzuku kwa ajili ya *sanitary pads* (vifaa vya hedhi) kuziongeza katika *capitation fund* ili kuweza kupunguza suala la utoro mashulen. Sasa Serikali ina mkakati gani katika bajeti ijayo kuongeza pesa hizo ili watoto wetu waweze kupata pedi hizo bure mashulen? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makubaliano ya Jumuiya ya *East Africa* nadhani ni mionganoni mwa jambo ambalo lilikuwa likijadiliwa sana hasa tatizo kubwa la watoto wasichana wanapokosa hivi vifaa kwa ajili ya kujikumu wakiwa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tulichukue hili kwa sababu ni jambo la msingi basi tukifika kwenye mchakato wa bajeti sisi sote tushirikiane kwa pamoja tuangalie nini

tufanye ili mradi kuhakikisha kwamba tuweze kusaidia vijana wetu watulie masomoni na wapate elimu vizuri. Kwa hiyo, tunalichukua kama mchango mzuri katika mchakato tutakuja tutaijadili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Mponda.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba niulize swalii dogo la nyongeza.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Elimu ametoa kauli akisema watoto wakitaka kuolewa wawe na cheti cha kumaliza *form four*, wakati huo huo Serikali ilisema wale wanafunzi ambao wanapata ujauzito wakiwa shuleni wasiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa nipate kauli ya Serikali katika mkanganyiko huu, nini hasa ni kauli ya Serikali sahihi. Vipi wanafunzi ambao wanapata mimba wakiwa shuleni na hawaendelei kwa mfumo wa shule, lakini na kauli ya Waziri ya kusema anayetaka kuolewa awe na cheti cha *form four*? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) -MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa majibu sahihi kwa Mheshimiwa Waitara pamoja na Watanzania wote waliopata mkanganyiko kuhusu kauli hiyo ni kwamba, nilisema Sera Mpya ya Elimu ya mwaka 2014 huko tunakoelekea inabadilisha mfumo wa sasa wa elimu kwenda kwenye mfumo mpya ambao utahitaji mtoto aanze chekechea mwaka mmoja, asome shule ya msingi miaka sita, shule ya sekondari miaka minne na hii itakuwa ni lazima kwa ye yeyote atakayeanza darasa la kwanza hadi amalizie *form four*. Kwa hiyo, nikasema kwamba tutakapofika wakati huo, kithibitisho muhimu kwamba huyu mtoto sasa amemalizie *form four* ni *school leaving certificate*, wakati huo siyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Waitara huo ni uafanuzi sahihi kabisa wa sera mpya. Sasa hivi tunaandaa utaratibu na maandalizi ikiwepo pamoja na miundombinu ili tuweze hatimae kuitekeleza hiyo sera muda utakapofika. Kwa hiyo, usiwe na mkanganyiko ndugu yangu Waitara. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Mponda.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la msingi Waziri amezungumzia kwamba baadhi ya Halmashauri tayari wameshamaliza ujenzi wa maabara katika shule za sekondari na mojawapo ya Halmashauri hii ni Halmashauri ya Malinyi tumeshamaliza karibu asilimia 90 ya maabara ya masomo ya sayansi katika shule za sekondari na baadhi ya majengo haya sasa hivi yanaanza kuharibiwa na wadudu wau ndege aina ya popo.

Je, ni lini Serikali watakamilisha utaratibu wa kipeleka vifaa ili maabara hizo zianze kutumika rasmi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba tuliweza kununua vifaa kwa ajili ya maabara zaidi ya 1,000, tumeweza kuvisambaza. Ninafahamu Mheshimiwa Dkt. Mponda hata tulivyofika kule kwako Malinyi tuliona kweli ultioa *concern* hiyo.

Kwa hiyo, tutafanya kila liwezekanalo kuona jinsi ya upelekaji wa vifaa. Hata hivyo, katika ile shule ambayo ulisema ina changamoto kubwa, kabla ya mwezi wa pili nadhani tutafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba shule ile tunaiboresha, wananchi wa Malinyi ambao wana changamoto kubwa sana waweze kupata elimu vizuri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Chikota.

Na. 41

Hitaji la Maafisa Ugani

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Ili kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo, ujuzi na maarifa ya watalaam wa kilimo unatakiwa uwafikie wakulima mara kwa mara.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa kibali cha kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha na kuwapeleka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa baada ya uteuzi, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani kubwa aliyooonesha juu yangu, wananchi wa Wilaya ya Newala na kwa hakika wananchi wote wa Mkoa wa Mtwara, wamepokea uteuzi wake kwa shangwe kubwa. Na mimi nataka nichukue nafasi hii kumuahidi Rais nitatekeleza majukumu yangu ya kumsaidia bila upendeleo wala woga na siku zote nitamuomba Mwenyezi Mungu anisaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa njiblu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuleta mapinduzi ya kweli ya kilimo, ujuzi na maarifa ya watalaam wa kilimo unatakiwa uwafikie wakulima mara kwa mara. Serikali imekuwa ikitoa vibali vya ajira za Maafisa Ugani katika Mamlaka za Serikali

za Mitaa kila mwaka wa fedha kutegemea uwezo wake wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa kati ya mwaka 2013/2014 hadi 2016/2017 jumla ya Maafisa Ugani 5,710 walijiriwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetoea kibali cha kuajiri Maafisa Ugani 1,487. Aidha, Serikali itaendelea kutoa nafasi za ajira kwa Maafisa Ugani kadri ya mahitaji na uwezo wa bajeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upungufu huo wa Maafisa Ugani ni mkubwa sana kwenye Halmashauri ambazo zimeanzishwa hivi karibuni, kama Halmashauri ya Mji wa Nanyamba; je, Serikali ina mpango gani wa upendeleo kwa mamlaka hizi mpya za Serikali za Mitaa ambazo zimeanzishwa hivi karibuni?

Swali langu la pili, ukiangalia takwimu za ajira zilizotolewa hivi karibuni kwa Maafisa Ugani, na kwa kuwa nchi yetu ina takribani vijiji zaidi ya 12,000 utaona kwamba kuna vijiji vingi sana vinakosa Maafisa Ugani.

Je, Serikali ina mpango gani au mkakati gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba kila kijiji katika nchi yetu kinakuwa na Afisa Ugani ili kuleta mapinduzi ya kweli katika kilimo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Utumishi inatambua kwamba Mamlaka mpya za Serikali za Mitaa zilizoanzishwa zinahitaji upendeleo mpya, hasa katika kupanga watumishi. Nataka nimuahidi kwamba siyo Nanyamba tu, Nanyamba ni Mamlaka mpya ya Serikali za Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Mji wa Newala ni mpya, Halmashauri ya Mji wa Tarime ni mpya, Halmashauri ya Mafinga ni mpya, maeneo yale yote ambayo tumeanzisha Halmashauri mpya najua wakati wa kugawana watumishi zile mamlaka mpya hazikupata watumishi wengi. Kwa hiyo, nitakachofanya ni kuhakikisha zile mamlaka mpya zote zinapata watumishi wa kutosha ili zilingane, kama ni upungufu ulingane na zile mamlaka zilizokuwepo kabla.

Swali lake la pilli, ni kweli kwamba vijiji vingi havina hawa Maafisa Ugani, hili limetokea kwa sababu muda mrefu katika nchi yetu, vile vyuo vinavyofundisha vyeti vyaa kilimo vilikuwa vimesimama, lakini baadae vimefufuliwa, sasa hivi kazi kubwa inaendelea. Nataka nimhakikishie kwamba tutaananza programu maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba vyuo vile wanachukua wanafunzi wengi zaidi ili wanapomaliza waweze kuajiriwa na Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Qambalo ajiandae Mheshimiwa Ritta.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na umuhimu wa watumishi katika kada hii ya Maafisa Ugani kama kweli tunataka kuleta mapinduzi ya kilimo kwenye nchi yetu. Jambo ambalo tunalionia sasa hivi ni kwamba kutokana na kutokuajiriwa kwa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wa kutosha, baadhi ya watumishi katika kada hii ya kilimo sasa ndio wamekaimishwa zile ofisi za Kata kwa maana ya kuwa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata.

Je, ni lini Serikali itaajiri watumishi katika kada hiyo ya utendaji ili watumishi hawa muhimu wa eneo la kilimo warudi kufanya kazi ya kilimo na wananchi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pale mahali ambapo Maafisa Watendaji wa Kata hawapo, Maafisa Ugani wamekaimishwa nafasi hizo, hii imetokana na upungufu wa kutotosheleza Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleze Bunge lako Tukufu, kazi moja wapo ya Afisa Mtendaji wa Kata ni kusukuma maendeleo ndani ya kata, watu waliofanya vizuri sana katika shughuli hii ni Walimu, Maafisa Kilimo, Mabibi Maendeleo, kwa hiyo pale ambapo Afisa Kilimo anakaimishwa Kata siyo makosa, ni nafasi nzuri ya kumuangalia keshokutwa huenda akawekwa moja kwa moja. Jambo la msingi hapa ni kwamba Wizara yangu inakubali kwamba kuna haja ya kulifanya kazi suala hili kuhakikisha kwamba Kata zetu zote na vijiji vyetu vinakuwa na Maafisa Watendaji wa kudumu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ritta, ajiandae Mheshimiwa Ghasia.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa uhaba wa Maafisa Ugani uko sawasawa kabisa na uhaba wa wataalam wa mifugo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Maafisa Mifugo wa kutosha ili wananchi wasaidiwe haki katika Halmashauri zetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Ajiandae Mheshimiwa Ghasia, atafuatiwa na Innocent.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itashughulikia tatizo la uhaba wa Maafisa Ugani sambamba na tatizo la Maafisa wa Mifugo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ghasia, ajiandae Mheshimiwa Innocent, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kuuliza swali la nyongeza kwa kaka yangu, Mheshimiwa Kapteni Mkuchika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watumishi katika sekta ya kilimo ni sawasawa sana au zaidi ya katika sekta ya afya. Sasa hivi maeneo mengi, hasa vijijini, kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi katika sekta ya afya.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuajiri watumishi wa sekta ya afya ili kunusuru maisha ya Watanzania, hasa akina mama na watoto? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, anataka kujua ni lini tu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba maeneo muhimu ambayo wananchi wanategemea kupata huduma ni upande wa afya, maji, hayo ni mambo yanayogusa maisha ya kila siku pamoa na elimu na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote Serikali inapoajiri imekuwa ikiweka umuhimu mkubwa sana upande wa watumishi wa afya, kwa sababu Waziri wa Utumishi anaajiri hawa Maafisa Afya baada ya kuwa tayari wameshafunzwa na kuhitimamu, nataka niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba nitazungumza na Waziri mwenzangu wa Elimu na Wizara ya Afya wapate mafunzo watumishi wengi zaidi katika fani ya afya ili wakazibe mapengo haya yaliyopo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Innocent, ajiandae Mheshimiwa Zacharia.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na kwamba wananchi wana haki ya kupata huduma ya watumishi, hasa walimu, wauguzi na watendaji wa vijiji na kata, pia jitihada nzuri ya Serikali inayoifanya ya kipeleka fedha za maendeleo vijijini inahitaji watumishi hawa waweze kusimamia miradi hii. Kwa upande wa Karagwe kuna *shortage* kubwa ya Walimu wasiopungua 850, kuna *shortage* kubwa ya wauguzi.

Je, nini tamko la Serikali, maana kila mwaka wa fedha Serikali inasema itapanga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuhakikisha tunakuwa na watumishi wa kutosha. Nini tamko la Serikali kuhusu hii *shortage* ya watumishi ya sasa hususan Wilaya ya Karagwe? Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, wote wanataka kujua ni lini tu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa walimu na matabibu na wataalam wa idara ya afya na imekuwa ikichukua hatua kuona kwamba tunaziba mapengo haya. Kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaanza sekondari zetu za kata uhaba wa walimu ulikuwa mkubwa sana, lakini Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwepo walimu wa kutosha imefanya jitihada ya kuajiri walimu wengi na hivi sasa katika shule zetu za sekondari, hali ya walimu imekuwa nafuu ukiondoa labda mapungufu makubwa yaliyopo katika upande wa walimu wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi ya kudumu ninamuahidi tu kwamba Serikali itaendelea na kasi ileile ya

kuajiri watumishi wa afya na elimu ili wananchi wetu wapate huduma ya afya bora, ili watoto wetu wapate elimu inayojitosheleza. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Waziri kwa kuteuliwa kwake pamoa na Mawaziri wengine wote.

Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Serikali ilikuwa na nia njema ya kuajiri watumishi 52,000; je, Serikali sasa itatekeleza mpango ule wakati gani ili vijana wetu waliopo mitaani waweze kupata nafasi ya ajira?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baada ya mchujo wa watumishi hewa, Mheshimiwa Rais ametoa idhini, Serikali imeidhinisha waajiriwe watumishi wapya 15,000, hilo zoezi linafanyika. Pia katika mwaka huu wa fedha kuna kibali cha kuajiri watumishi 52,000, zoezi hilo litaendelea, nataka nihakikishe kwamba nafasi na fedha za kuwalipa zipo, kazi hiyo itatekelezwa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante.

Na. 42

Kushindwa kwa Mpango wa MKURABITA

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Mpango wa MKURABITA ni muhimu katika kuwalettea wananchi maendeleo lakini unakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa fedha na hivyo kushindwa kuendesha shughuli za urasimishajji kwa ufanisi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mfuko wa urasimishaji utakaokuwa maalum katika Serikali za Mitaa ili kutatua tatizo la ukosefu wa fedha za kuendeleza shughuli za urasimishaji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la ndugu yangu, mdogo wangu, somo yangu, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa MKURABITA ni muhimu katika kuwaletaa wananchi maendeleo, lakini mpango huu unakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa fedha na hivyo kushindwa kuendesha shughuli za urasimishaji kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania ulianzishwa na Serikali kwa lengo la kuwapa nguvu ya kiuchumi wananchi kwa kuwawezesha kumiliki ardhi na kuendesha biashara katika mfumo rasmi na wa kisasa unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa tatizo la upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za urasimishaji na ndio maana Serikali imedhamiria kuanzisha Mfuko Maalum wa Urasimishaji utakaowezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya urasimishaji bila vikwazo. Mfumo utakaotumika ni kwa Serikali kuititia MKURABITA kuweka fedha za dhamana katika taasisi za fedha zilizokubalika ili kuwawezesha Halmashauri kukopa na hivyo kuendesha shughuli zake za urasimishaji. Kwa kutumia mfumo huu urasimishaji utakuwa nafuu, haraka na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA kwa kushirikiana na Benki ya NMB imekamilisha utaratibu wa utekelezaji wa

miradi ya majaribio katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri za Wilaya za Mbozi na Momba Mkoani Songwe. Baada ya majaribio haya ambayo yamepangwa kufanyika kwa miaka miwili, utekelezaji utaanza nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 243, fedha ambayo itatumika kama dhamana kwa ajili ya mikopo ambayo itakopwa na Halmashauri ambazo zitatekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, urejeshwaji wa mikopo hii utatokana na michango ya wananchi wenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, nina maswali mawili.

Swali la kwanza, kwa kuwa MKURABITA katika Wilaya ya Mpwapwa walichagua vijiji viwili; Kijiji cha Inzomvu na Kijiji cha Pwaga, lakini kwa upande wa Kijiji cha Pwaga mambo ni mazuri, mradi ulitekelezwa, masijala ilijengwa na wananchi walipewa Hati za Kimila. Lakini katika Kijiji cha Inzomvu hakuna kilichofanyika, baada ya kupima mashamba wananchi walipewa mafaili tu wakaenda nayo majumbani, hakuna chochote na ofisi ya masijala haipo.

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwamba ipo haja sasa ya Serikali kuleta muswada hapa ili tubadilishe chombo hiki MKURABITA ambao unategemea zaidi fedha za mfadhili na fedha za Serikali ni kidogo sana ili tubadilishe uwe mfuko wa urasimishaji ili wadau wengi waweze kuchangia na chombo hiki kiwe na fedha za kutosha ili wananchi wengi waweze kunufaika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa

Mwenyekiti, nimefurahi kusikia kwamba Mpwapwa iliingia katika majaribio, walipata vijiji viwili, kijiji kimoja kinafanya vizuri kingine hakijafanya vizuri. Nimuombe tu ndugu yangu, Mheshimiwa George Malima Lubeleje apange muda anaona yeye inafaa ili mimi na yeye twende katika kijiji hicho ambacho kimesahauliwa na mimi nikajifunze nikajue kimetokea nini, nichukue hatua ili vijiji hivyo pacha viweze kufanana katika utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kwamba kuletwe muswada utakaobadilisha chombo hiki, Serikali inapokea rai hii, lakini nataka nieleze kwamba kama nilivyosema tangu mwanzo tunakusudia kuanzisha Mfuko Maalum wa Urasimishaji, wakati wa kuanzisha mfuko maalum wa urasimishaji ikionekana haja iko ya kubadili sheria, suala hilo litazingatiwa na taratibu za kubadilisha sheria zinafuata ngazi kwa ngazi, itatekelezwa kadri Serikali itakapoona inafaa.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye.

Na. 43

Upatikanaji wa Maji ya Kudumu- Mkoa wa Kigoma.

MHE. KIZA H. MAYEYE aliuliza:-

Mkoa wa Kigoma umebarikiwa kuwa na Ziwa Tanganyika, Mto Malagarasi na vyanzo vingine vya maji lakini Mkoa huu unakabiliwa na changamoto kubwa ya maji.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Kigoma hususan katika Jimbo la Kigoma Kaskazini katika kuhakikisha wanapata maji ya kudumu ya kwenye mabomba?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la

Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inaendelea kutekeleza miradi wa maji vijiji katika Halmashauri ya Wilaya Kigoma iliyopo Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2017 jumla ya miradi mitatu ya maji ya Nyarubanda, Kagongo na Nkungwe imekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji. Mradi mmoja wa Kalinzi upo katika hatua za mwisho na utekelezaji wake umefika asilimia 90. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri hiyo imetengewa shilingi milioni 649.8 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ya maji vijiji.

Vilevile Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelijiji imeanza utekelezaji wa mradi ya maji katika vijiji vya Halmashauri za Mkoa wa Kigoma utakaogharimu shilingi bilioni 20.6 na itatekelezwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2017 hadi 2021. Mradi huo utanufaisha wakazi 207,785 katika vijiji 26 vya kipaumbele katika Halmashauri za Mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mijini, Serikali inatekeleza mradi wa maji Mjini Kigoma kwa gharama ya *Euro* milioni 16.32. Mradi huo unahusisha ujenzi wa chanzo cha maji ukingoni mwa Ziwa Tanganyika eneo la *Amani Beach* chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 42 kwa siku, ikilinganishwa na lita milioni 12 zinazozalishwa sasa. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa matanki matano yenye ujazo wa lita milioni mbili kila moja na tanki moja lenye ujazo wa lita 500,000; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilometra 22 na mabomba ya kusambaza maji urefu wa kilometra 132, ujenzi wa vioski 70 vya kuchotea maji katika maeneo mbalimbali.

Aidha, katika kuboresha huduma ya usafi wa mazingira, mabwawa ya kutibu majitaka yenye uwezo wa kutibu mita za ujazo 150 kwa siku yatajengwa pamoja na ununuzi wa gari la kunyonya na kusafirisha majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Oktoba 2017, kwa ujumla utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 76 na unatarajiwu kukamilika mwezi Disemba 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza upatikanaji wa majisafi na salama kutoka asilimia 69 za sasa hadi kufikia asilimia 100.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiza.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, ni lini sasa Serikali mtatimiza ahadi yenu na kutekeleza mradi huu wa Maji katika Mji ya Manispaa ya Kigoma Mjini kufika katika Mji Mdogo wa Mwandiga?

(b) Serikali haioni sasa ni muda muafaka maji haya ya Ziwa Tanganyika kwenda katika Wilaya ya Kasulu? Ahsante. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi na hongereni Wabunge Viti Maalum wapya, mnauliza maswali mazuri. (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji kwa Mji wa Mwandiga unategemeana kabisa na utekelezaji wa mradi huu mkubwa ambao utakamilika mwezi huu Disemba. Mradi huu utazalisha lita milioni 42 na mahitaji ya Mji wa Kigoma ni lita milioni 20. Kwa hiyo, kutakuwa na maji ya kiasi kikubwa ambayo tutaweza kuyapeleka katika Mji wa Mwandiga. Kikubwa nataka niwahakikishie wananchi wa Mwandiga subira yavuta kheri na kheri itapatikana katika upatikanaji wa maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili kuhusu

suala la upatikanaji wa maji katika Mji wa Kasulu nataka nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani. Serikali imefanya kazi kubwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu mkubwa wa maji, sasa hivi Mji wa Kasulu upo mionganoni mwa miji 17 ambayo kupitia fedha za India utapata maji. Kikubwa tumsubiri Mhandisi Mshauri atatushauri vipi ili tupate maji ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Kasulu wanapata maji kwa wakati. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Nape halafu Mheshimiwa Mbatia.

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Wilaya ya Urambo na Kaliua na Serikali imekuwa ikituambia kwamba imekamilisha mchakato wote wa kutoa maji Mto Malagarasi kupeleka Kaliua na Urambo, fedha tu ndiyo bado hazijapatikana toka mwaka jana walituambia fedha hizo zitapatikana.

Je, *statusya* kupata pesa kupeleka maji katika Wilaya ya Urambo na Kaliua ikoje mpaka sasa kwa sababu hali ni mbaya sana kwa wananchi hao? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunao mradi wa usanifu unakamilika wa kutoa maji Malagarasi kupitia Kaliua kuja Urambo hadi Tabora, pia Mheshimiwa Rais ametuagiza kwamba huu mradi unaotoa maji Solwa kutoka Ziwa Victoria kupeleka Tabora wakati unaendelea tayari tumeshaagiza Mamlaka yetu ya Maji ya Tabora iangalie uwezekano wa kuweka mabomba mengine kutoka matanki ya Tabora kupeleka Urambo na ikiwezekana yafike mpaka Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie Mheshimiwa Munde kwamba Serikali inafanya kazi kuhakikisha Kaliua na Urambo wanapata maji safi na salama. (*Makofii*).

MWENYEKITI: Mheshimiwa, Nape Nnauye, ajiandae Mheshimiwa Mbatia na ajiandae Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa maji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara bado ni mbaya sana na aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji ambaye sasa ni Waziri wa Maji alipotembelea Mikoa ya Lindi na Mtwara alikagua baadhi ya miradi ambayo inaendelea katika Jimbo la Mtama, Mradi wa Maji wa Nyangamara na pengine hakufika lakini Mradi wa Maji wa Namangale na alituhaidi kwamba *certificates* za miradi hiyo zikifika Wizarani mara moja pesa zitalipwa, mpaka sasa huu ni mwezi wa pili au wa tatu *certificates* hizo zimefika Wizarani na hazijalipwa.

Je, ni lini Serikali italipa pesa hizi za hawa wakandarasi ili miradi hii ipate kukamilika wananchi wangu wapate maji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha na Mipango jana ametupatia shilingi bilioni 12. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba hizo *certificates* kama zimeshaletwa wiki iiao tutahakikisha tumezilipa ili mkandarasi aendelee kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa James Mbatia, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Shekilindi ajiandae.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maji nchini kwa

ujumla siyo nzuri na lengo Namba 6 la ajenda ya 2020/2030 ni maji, upatikanaji wa maji safi, salama kwa wote duniani na Tanzania ni mwanachama. Katika Jimbo la Vunjo sehemu za kata....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbatia muda wetu ni mdogo tuende moja kwa moja kwenye shida ya Jimbo lako.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Katika Kata ya Mwamba Kusini na Mwika Kusini hali ya maji ni mbaya sana na wananchi wanunuua maji ndoo moja kwa shilingi 500.

Je, Serikali inachukuliaje jambo hili kwa dharura ili upatikanaji wa maji uweze kupatikana kwa haraka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa maji nchi ni nzuri kuitia programu ya maendeleo ya sekta ya maji awamu ya kwanza. Tulilenga kutekeleza miradi 1,810, tayari tumeshatekeleza miradi 1,433, tumejenga vituo vya kuchotea maji 117,000 na vituo vyote vingetoa maji vijiji sasa hivi tungkuwa na asilimia 79 ya upatikanaji wa maji safi na salama. Kutokana na mabadiliko kidogo ya tabianchi vyanzo vingi vya maji kukauka sasa hivi hiyo asilimia kidogo imeshuka, lakini tayari tumejipanga kuhakikisha maeneo yote ambayo hayatoi maji tumetenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu tulionao ili hayo maeneo yaweze kupatiwa vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Vunjo Mheshimiwa Mbunge naomba tukutane, tujadili ili tuone ni namna gani tutatoa kitu cha dharura kuhakikisha wale wananchi wanapata maji.

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa. Mheshimiwa Kuchauka, ajiandae Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Chumi.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kutokamilika kwa miradi ya maji katika Halmashauri zetu kumekuwa ni tatizo sugu, niliwahi kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wakati huo ambaye sasa ndiyo Waziri alisema pesa Wizarani zipo ila watu wapeleke *certificate*. Ninasikitika kumwambia kwamba hapa ninayo makabrashi ambayo ni *copy* ya hizo *certificate* ambazo zimeshafika kwenye Wizara yake sasa ni zaidi ya mwaka mzima hizo pesa hazijawahi kutolewa, na kuna miradi kadhaa katika vijiji vya Kipule, Ngongowele pamoja na Mikunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali ni lini miradi hii itakamilika ili wananchi wa vijiji hivi waweze kupata maji. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *certificate*, ni masula ya kiutendaji Mheshimiwa Mbunge, ninaomba baada ya Bunge hili leo tukutane, twende kwa watendaji tukaangalie *certificate* kama zipo, kama nilivyosema kwamba tayari nina fedha ili wiki ijayo tuweze kulipa.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Shekilindi, ajiandae Mheshimiwa Chumi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza Wilaya ya Lushoto ina vyanzo vingi sana vya maji lakini wananchi wa Lushoto hawana maji safi na salama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumtua mama ndoo kichwani hasa akina mama wa Makanya, Kilole, Kwekanga, Kwemakame, Ngulwi, Ubiri, Handeni na Miegeo? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Mheshimiwa najua Naibu wako ni midadi ungemwachia achia naye

kidogo, maana majibu anayo mazuri. Mheshimiwa Waziri basi endelea.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea Lushoto nikakuta hilo tatizo na nikamuelekeza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Tanga aweze kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri yake, hadi jana nimepiga simu tayari wamekamilisha taratibu za manunuzi, Baada ya siku 14 mikataba itasainiwa, utekelezaji uanze.

Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba maeneo yote ya Halmashauri yako yatapata maji.

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wetu ni mdogo najua kuna kero kubwa ya maji, muda tulio bakiwa nao ni nusu saa tu. Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mafinga ni kati ya miji inayokuwa kwa kasi sana hapa nchi na hivyo uhitaji wa maji umekuwa ukiongezeka kwa kasi. Kutokana na jitihada mbalimbali ambazo wananchi wa Mafinga wanajituma na uwekezaji katika mazo ya misitu.

Je, Serikali, iko tayari lini kutupa kibali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi ya mwaka huu wa fedha wa 2017/2018?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri mpya lakini *data* kibao.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, lakini nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Mheshimiwa Cosato Chumi kwa kazi kubwa anazozifanya na namna anavyofuatatilia ili wananchi wake wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Wizara

imeshatoa kibali kwa mradi wa Mji wa Bumilianga ili kuhamkisha kwamba wananchi wanapata maji. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKTI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ardhi Mheshimiwa Lucia Michaeli Mlowe.

Na. 44

**Serikali Kuendesha Zoezi la Mipango Miji
na Matumizi Bora ya Ardhi**

MHE. LUCIA M. MLOWE aliuliza:-

Msongamano wa magari, ujenzi holela, miundombinu duni ya maji taka na kadhalika katika miji mikubwa hapa nchini vinatokana na udhaifu wa upangaji wa matumizi bora ya ardhi (*poor land use planning*).

Je, Serikali imejiandaa vipi kuendesha zoezi la Mipango Miji na matumizi bora ya ardhi katika miji mipya ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Njombe?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI** aliujibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu Namba 7(1) cha Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 kinaelekeza kuwa jukumu la upangaji na uendelezaji miji lipo chini ya mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa Miji, Wilaya na Mamlaka za Miji Midogo. Kutokana na umuhimu wa kuwa na Miji iliyopangwa kiuchumi na kijamii, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo uandaaji wa mipango kabambe itakayotumika kuongoza,

kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa Miji pamoja na urasimishaji wa makazi yasiyopangwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Hadi kufikia Oktoba 20, 2017 maandalizi ya mipango kapambe ya miji 29 nchini ilikuwa imefikia katika hatua mbalimbali. Maeneo hayo ambayo tayari mipango yake ipo katika hatua mbalimbali ni Majji ya Mwanza, Da es Salaam, Arusha na Tanga na kwa upande wa Manispaa tunayo Mtwara - Mikindani, Iringa, Musoma, Tabora, Singida, Sumbawanga, Songea, Shinyanga, Morogoro, Lindi, Bukoba, Moshi, Mpanda na Kigoma Ujiji. Kwa upande wa miji midogo ni Kibaha, Korogwe, Njombe, Bariadi, Geita, Babati, Ifakara, Mahenge, Malinyi, Tunduma na Mafinga. Kati ya maeneo hayo, mipango kabambe kwa Manispaa ya Mtwara - Mikindani, Musoma, Iringa na Singida imeshaidhinishwa na kuzinduliwa na hivyo imeanza kutumika rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa mipango kabambe hufanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo makampuni ya upangaji na upimaji ardhi yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria, wamiliki wa ardhi, taasisi za Serikali, watu binafsi na asasi za kiraia pamoja na taasisi, zinatoa huduma mbalimbali za miundombinu kama vile *TANESCO*, *TANROADS* na Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka. Utekelezaji wa mipango hiyo husaidia kutatua changamoto zilizopo na hatimae kuwa na miji iliyopangwa na yenye mtandao mzuri wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango kabambe wa Mji wa Njombe unaandaliwa na Kampuni ya *CRM Land Consult* ya Dar es Salaam kupitia programu ya *Urban Local Government Strengthening Program* iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hadi sasa rasimu ya kwanza ya mpango kabambe ya mji huo imeandaliwa na hatua inayofuata ni kuwasilisha rasimu hiyo kwenye mikutano ya wadau kwa ajili ya kupokea maoni na mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa mamlaka za upangaji ambazo hazina mipango kabambe, kuanza

maandalizi ya mipango hiyo pamoja na kongeza kasi ya kupanga maeneo mapya, kurasimisha makazi yasiyopangwa na kudhibiti uendelezaji holela kwa kushirikiana na makampuni yaliyosajiliwa kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlowe.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, wananchi wapatao 200 wa Makambako Kata ya Kivavi, Mtaa wa Mashujaa waliondolewa katika maeneo yao mwaka 1997 bila kupewa fidia, kwa ajili ya kupisha ujenzi wa soko la kimataifa, wamefuatilia wananchi hawa lakini hadi leo hakuna majibu. Pia kuna wananchi wa Idofi waliondolewa maeneo yao kwa ajili ya kupisha ujenzi wa mizani hadi leo hawajapata fidia.

Je, Serikali inampanga gani wa kuwalipa wananchi hawa fidia zao?

Swali la pili, kwa kuwa kila Halmashauri kuna Maafisa Mipango Miji. Je, ni kwa nini wananchi wanajenga sehemu zisizo sahihi na Serikali inawaangalia tu mwisho wa siku wanaanza bomoa bomoa? Naomba kupata majibu (*Makofii*).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na sehemu yake ya kwanza wananchi 200 wa Makambako na wale wa Kidozi kwamba walipisha miradi ya Serikali na mpaka leo hawajalipwa fidia. Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mlowe kwamba mara pesa zitapopatikana watalipwa, kwa sababu Serikali inatambua kwamba ililitwaa lile eneo kwa ajili ya matumizi ya Serikali, kwa hiyo, asiwe na wasiwasi pesa ikipatikana watalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anaongelea habari ya maafisa kwamba watu wanajenga ovyo na wanaangalia na hakuna hatua zinazochukuliwa baadae wanakuja kuwabomolea. Naomba nitoe rai tu kwa sababu pia ni sehemu ya Halmashauri na tunakaa katika vikao vyetu vya Halmashauri kwa maana ya Baraza la Madiwani, haya yanapotokea ni wajibu wetu pia kutoa maonyo kwa wale ambaao wamepewa wajibu huo wa kufanya kazi lakini hawasimamii sawasawa. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge atakapokuwa amekaa katika Baraza lake la Madiwani wajaribu kuwakumbusha hasa wale watendaji ambaao hawatimizi wajibu wao vizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuiliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na kazi nzuri na jitihada za Serikali katika kuhakikisha miji inapangwa na zoezi zima la urasimishaji wa makazi ikiwemo upimaji shirikishi, naomba tu kujua Serikali inayo mkakati gani kuhakikisha kwamba pamoja na upimaji huu unaofanyika sasa ile gharama ya *premium* inaonekana kuwa mzigo mkubwa kwa wananchi na matokeo yake wanashindwa kufikia hatua ya kupewa hati miliki, hivyo inawapelekea kubaki katika maeneo ambayo yamepimwa bila hati hizo.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuondoa kabisa hizi asilimia 2.5 zilizopunguzwa japo ilikuwa Saba ikapunguzwa, nini mkakati wa Serikali kuondoa hizi lakini kuongeza muda wa upimaji shirikishi ili wananchi wengi zaidi waweze kupimiwa kuhakikisha maeneo yao yote yamekamilika? Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, ni lini tu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuititia Bunge hili Tukufu kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Mabula kwa

sababu jana pia wakati anachangia Mpango wa Maendeleo amezungumzia suala la kuwajali sana wananchi na hasa katika suala zima la urasimishaji na mpango unaoendelea. Ametupa changamoto kama Wizara na sisi tunamshukuru na tumeona iko haja kweli ya kuangalia hawa wananchi ambao walitumia nguvu zao kujenga katika maeneo ambayo pengine hatukuwa makini katika kuwahi kupanga na wao wakavamia, basi tumesema kwa sababu hoja ni kupunguziwa mzigo, tumelichukua suala lake kuondoa *premium* na kabla ya mwisho wa mwezi huu tutakuwa tumempa jibu.

Je, ni lini zoezi hili litaendelea, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa maeneo yale ambayo yanarasimishwa na yamekwishaanza kwa mwaka huu tutavumilia mpaka mwisho wa mwaka huu wa fedha. Baada ya mwaka wa fedha tuna imani na mipango mijii katika maeneo hayo, mipango kabambe katika maeneo hayo itakuwa tayari kwahiylo ukomo wao itakuwa ni mwisho wa mwaka wa fedha mwaka huu 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Angelina Malembeka.

Na. 45

Upimaji wa Ardhi katika Taasisi za Umma

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA aliuliza:-

Kutokana na uvamizi wa ardhi katika maeneo ya mashule, masoko na zahanati.

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha upimaji wa maeneo hayo?

(b) Je, kutokana na ukubwa wa gharama za upimaji, kwa nini zoezi la upimaji lisitolewe bure kwa taasisi za umma kuititia Halmashauri hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya shule, soko, zahanati, vituo vya afya, hospitali, vyuo, ofisi za Serikali, vituo vya polisi, mahakama, maeneo ya majeshi, hifadhi za misitu na wanyama na maeneo ya makumbusho hutengwa maalum kwa ajili ya matumizi ya umma na shughuli mbalimbali za Serikali. Maeneo yote haya yapo chini ya usimamizi na uangalizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa au Serikali Kuu. Hata hivyo, maeneo mengi kati ya hayo yamekuwa yakismamiwa na taasisi za Serikali bila kupimwa wala kuwa na hatimiliki badala yake yamekuwa yakimilishwa kwa utaratibu wa kupewa *government allocation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu pamoja na kwamba umekuwa ukifanywa kwa nia njema, umetoa mwanya kwa wananchi wenye nia ovu kuyavamia, kuyamega na kuyaendeleza maeneo ya Serikali kinyume na utaratibu. Ili kuhakikisha kuwa changamoto ya uvamizi wa maeneo ya umma unakomeshwa, Serikali kuititia Wizara yangu iliagiza kuwa maeneo yote ya umma, yapimwe na yamilishwa kwa taasisi husika kuititia barua yenyewe Kumb. Na. AB225/30/305/01 ya tarehe 7 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuitikia wito huu baadhi ya taasisi za Serikali ikiwemo *TBA*, Hazina na *TANROADS* zinaendelea kuyatambua maeneo yake na kuyamilishwa maeneo wanayoyasimamia. Nitoe rai kwa Wakuu wote wa taasisi za umma kuhakikisha wanakamilisha zoezi hili mapema na kwa maeneo ambayo yamevamiwa ni vema wavamizi wakaondoka kwa hiari yao na wasisubiri mkondo wa sheria uwakumbe. Aidha, nampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Tabora na timu yake kwa kutekeleza agizo la Waziri

kwa vitendo na ni vema Wakuu wote wa Mikoa wengine wakachukua hatua ili kuondoa wavamizi kwenye maeneo yote ya umma.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama elekezi za huduma za upimaji ambazo kwa mara ya mwisho zilifanyiwa mapitio mwaka 2016 siyo kubwa kama inavyodhaniwa kwa kuwa upimaji wa ardhi hufanywa kwa misingi ya kurejesha gharama pakee. Gharama hizo hujumuisha vifaa vya upimaji, shajara, usafiri, matengenezo ya vifaa na mawasiliano ya kitaalam. Aidha, kukamilika kwa mtando wa upimaji (*Taref 11*) tutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za upimaji nchini.

Mheshimia Mwenyekiti, natoa rai kwa taasisi zote za Serikali nchini kuhakikisha zinapima na kumilikishwa maeneo yao ili kuwa na mlliki salama kwa kuwa ulinzi wa ardhi wanayomilikishwa ni jukumu la taasisi husika. Aidha, taasisi zote za umma nchini zinahimizwa kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuharakisha upimaji wa maeneo yote wanayoyasimamia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malembeka.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Angelina mwenzangu, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa naibu Waziri amekiri kuwa wananchi wanavamia na kuyamega maeneo ya Serikali kinyume na utaratibu; na kwa kuwa ametoa rai wananchi waondoke maeneo hayo kabla sheria hajachukua mkondo wake, sasa isije ikawa kwa wananchi kilio, kwa watendaji vigelele.

Je, Serikali ina kauli gani juu ya watendaji ambao wanalipwa mshahara kwa kazi ya upimaji na katika maeneo yao hawajafanya lolote hadi sasa?

Swali la pili, kwa kuwa katika majibu ya msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema gharama elekezi za huduma ya upimaji siyo kubwa kama inavyoonekana au inavyodhaniwa.

Je, kwa nini gharama hizo zisiwekwe wazi ili wananchi na taasisi nyingine wafahamu na kuzitambua na waweze kujipanga kwa ajili ya kulipia? Ahsante.(*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante. Swali la kwanza ameulizia habari ya adhabu kwa watendaji ambao wanafanya makosa na tunaadhibu pengine wananchi. Kama nilivyomjibu muulizaji wa swali namba 44 majukumu na uwajibishaji yako chini ya mamlaka husika hasa katika maeneo yetu kwenye Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, haya yanapobainika basi tuyachukulie hatua papo hapo ili tusiweze kuwafanya wananchi waumie zaidi kwa makosa ya watendaji wetu.

Swali la pili, ametaka kuwekekewa gharama za upimaji wazi. Naomba niseme tu tutazitoa na tutawagawia Waheshimiwa Wabunge wote, lakini kwa kifupi tu nikianza kuzungumzia habari ya miji kwenye Mamlaka za Miji na Manispaa katika gharama za upimaji kuanzia *square meter* moja mpaka *square meter* 400 gharama yake kwa maeneo ya *residential* ni shilingi 65 lakini maeneo ya *commercial* ni shilingi 350 kwa *square meter*, kwenye *industrial* ni shilingi 450 na kwenye maeneo ya *social services* ni shilingi 150. Kwa miji yetu ya kwaida kwenye *township* ni shilingi 200 kwa makazi, maeneo ya biashara ni shilingi 300, maeneo ya viwanda 350 na maeneo ya *services* ni shilingi 100. Vivyo hivyo kwenye *trading center* ni shilingi 100 kwa makazi, shilingi 200 kwa *commercial*, shilingi 200 tena kwa *industrial* na shilingi 100 kwa *services*. Kwa sababu mlolongo pia unategemeana na ukubwa wa kiwanja vina-range kuanzia shilingi 300,000 mpaka milioni 14 kutegemeana na ukubwa kuanzia hekari

moja mpaka 10 ni shilingi milioni tatu, zinakwenda zinaongezeka kadri ya ukubwa, tutaziandaa na tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge wote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shanagzi, Mheshimiwa Komu halafu Mheshimiwa Mbarouk na Mheshimiwa Umbulla.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba la *Mnazi Estate* kule Lushoto - Mlalo limevamiwa kwa sababu Mmiliki ambae alikuwa anendelea kulimiliki ameshindwa kuliendesha. Je, pamoja na mchakato ambao tulikuwa tumeuanza wa kufuta, Serikali imefika hatua gani ya kumuondoa mmiliki katika ardhi hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Waziri mhusika.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye kijiji cha Mnazi kuna Kampuni inatiwa *Lemash Enterprise* ambayo ilikuwa inamiliiki shamba la Mkonge lenye hekta 1,275 lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kutokana na jitihada zake za kuondoa kero ya wananchi na katika kutekeleza *spirit* ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli walitimiza wajibu wao na nataka kumhakikishia kwamba na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli naye ametimiza wajibu wake. Tarehe 4 Septemba, 2017 shamba hilo limefutwa rasmi na mmiliki ameshaambiwa, nimeshachukua hatua ya kulitangaza kwenye Gazeti la Serikali kwa *order* ya Rais na hivi sasa nimeshamwandikia Mkuu wa Mkoa wa Tanga ili atupe mapendekezo mazuri zaidi ya namna ya kulitumia shamba hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nakuomba Mheshimiwa Shangazi kwa kuwa umelianza, basi naomba ushirikiane na Mkuu wa Mkoa wa Tanga kulimalizia mlete mapendekezo mazuri yatakayowezesha kutumika shamba

hilo kuinua uchumi wa wananchi wa Mnazi. Tungependa shamba hili liendele kuwa shamba la Mkonge lakini ninyi watu wa Tanga muamue nani aendesha kilimo hicho kwa ajili ya kuungeza tija ya ajira na uchumi wa Taifa. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Komu atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi vijijini kuna mashamba ambayo toka mwaka 1968 yalitaifishwa na kimsingi ni mashamba ya umma, lakini baada ya kutaifishwa na kupewa Vyama vya Ushirika yamekuwa yakigawanywa kwa taasisi mbalimbali kwa ajili ya shughuli za wananchi. Sasa hizo taasisi zilitaka kupima hayo mashamba sasa kulingana na shughuli ambazo zinafanyika inakuwa vigumu kwa sababu tayari kuna hati ambazo zilikuwepo toka wakati huo, ikiwa ni pamoja na eneo kama la Uru Seminari ambalo nilishalifikisha kwa Mheshimiwa Waziri.

Naomba kujua kutoka kwenye Serikalini ni lini Serikali itakwenda kufanya upimaji upya ili kutoa hati kulingana na matumizi ambayo yapo sasa hivi katika yale mashamba katika Kata zote hizo?

MWENYEKITI: Mheshimwia Waziri ni lini muda wetu umekwisha jaribuni kuwa na majibu mafupi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mkoa wa Kilimanjaro na mashamba ya ushirika ni tatizo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamna mashamba haya yalikuwa ni ya *settlers*, uamuzi wa Baba wa Taifa yalichukuliwa yakapewa Vyama vya Ushirika na mashamba haya ni mengi sana Mkoa wa Kilimanjaro ambayo yalimilikishwa Vyama vya Ushirika. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo nimeshamwandikia lakini

tunazungumza nia njema zaidi ya kuhakiki upya mashamba yanayomilikiwa na Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro hivi sasa. Ni kweli Vyama vya Ushirika zamani vilipewa, lakini leo matumizi yake ya vyama vya ushirika na ushirika wenyewe ni tofauti na madhumuni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Mkoa wa Kilimanjaro maana hoja hii siyo ya Mheshimiwa Mbunge peke yake, Wabunge wote wa Kilimanjaro mashamba haya yanawahusu. Watuachie bado tuko kwenye mazungumzo na Wizara ya Kilimo ambaye ndiyo Msajili wa Vyama vya Ushirika ili tuone namna gani njema ya kuyahuisha mashamba yote ya ushirika ya Mkoa wa Kilimanjaro ili yawe na tija kwa wananchi wote kulingana na mazingira ya sasa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji letu la Tanga kuna upimaji unaoendelea katika eneo la Amboni kwa ajili ya kuongeza Kiwanda cha Saruji cha Sinoma cha Wachina. Katika maeneo yale kuna tatizo kubwa la kwamba, wananchi wenyе mashamba yao wanaambiwa watalipwa fidia ya mazao ya muda mrefu tu na mazao ya muda mfupi kama mahindi, mihogo na mengineyo hayatalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inalifahamu hilo na utaratibu huu ni utaratibu wa sheria gani inayotumika kulipa mazao ya muda mrefu, na pia pana maji koto au *sulphur water* pale katika eneo la Amboni ambayo ni kama tunu kwa mambo ya utalii.

Je, Serikali inafanya juhudи gani kuhakikisha ile *sulphur bath* itaendelea kuwepo ambayo iliendelezwa na Galanos lakini pia na wananchi wenyе mzao mafupi nao watalipwa fidia yao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mhusika kwa kifupi sana *please*.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni la Tanga. Walioamua kufanya haya ni Halmashauri ya Jiji la Tanga kwenye shamba hili. ningemuomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kazi hii hata tathmini ya pale imesimamiwa na kufanywa na Wathamini waliopo kwenye Jiji la Tanga na upitishaji wa viwango huu ulikuwa shirkishi na maelekezo haya yametolewa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba, unajua ni rahisi kufikiri kwamba Waziri akiwa hapa Dodoma anaweza akajua na akalitolea uafanuzi kila jambo lakini jambo hili ni shirkishi limefanywa na Watendaji wenyewe Mamlaka ya Kisheria ya kutenda wa Jiji la Tanga kwahiylo kama halikufanyika vizuri, wale wananchi wanajua Bungeni hapa mwaka huu mmetunga Sheria ya Bodi ya Mfuko wa Fidia. Ninawaomba waisome, Waheshimiwa Wabunge muwasidie wananchi hawa wakate rufaa kwenye Bodi ya Mfuko wa Fidia ili iweze kufikiaria vinginevyo, lakini mimi kama aziri hapa siwezi kusimama nikatengua uamuzi halali uliofanywa na Halmashauri ya Jiji la Tanga. Hivyo, naomba wafuate hiyo sheria. (*Makofii*)

Na. 46

Huduma ya Matibabu ya Saratani - Hospitali ya Bugando

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Kutokana na msongamano mkubwa wa wagonjwa wa saratani katika Hospitali ya *Ocean Road* pamoja na gharama kwa ndugu wa wagonjwa ya kuwaleta na kuwauguza ndugu zao.

Je, Serikali haioni haja ya kuanza kutoa huduma hiyo katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza leo nasimama hapa toka niteuliwe na Mheshimiwa Rais, naomba na mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini na kunipa majukumu zaidi kwenye Serikali yake, pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega Vijijiini, Wilaya ya Nzega na Mkoa wetu wa Tabora kwa ujumla kwa ushirikiano ambao wameendelea kunipa. Napenda kusema tu kwa wote kwamba kwa hakika sitowaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa wenyewe Saratani ili kusogeza huduma hizi karibu zaidi na wananchi na kupunguza msongamano katika Hospitali ya *Ocean Road*, pia kupunguza gharama kwa wagonjwa na ndugu. Kwa sasa Serikali inakamilisha maandalizi ya kuanzisha matibabu ya saratani kwa mionzi katika Hospitali ya Bugando ambapo baadhi ya majengo kwa ajili ya huduma husika yamekamilika, yakiwemo jengo maalum ambalo ni kwa ajili ya kudhibiti mionzi, ambapo ukuta wake umejengwa kwa zege nene la mita moja (*bunkers*), jengo la kutolea huduma za mionzi, baadhi ya wataalam wapo na baadhi ya mashine za matibabu kwa mionzi zimeshanunuliwa zikiwemo *Cobalt 60*na *CT Simulator*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha *brachytherapy* na *immobilization devices* zinatarajiwa kuwasili mwezi Disemba, 2017. Kwa sasa huduma za tiba ya saratani zinazopatikana Bungando ni zile za matibabu yasiyo ya mionzi (*chemotherapy*) na zilianza mwezi Januari mwaka 2009, kufuatia sera ya Serikali ya kutoa huduma hizo kikanda. Takwimu zinaonyesha

kuwa, kwa kipindi cha mwaka 2009 - 2017 hospitali imetoa matibabu kwa wagonjwa 39,300 kati yao 12,200 wakiwa ni wapya, sawa na wastani wa waginjwa 1,500 kwa mwaka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudini nzuri za Serikali, takwimu zinaonyesha kuwa, asilimia 60 ya wagonjwa wanaohudumiwa Hospitali ya *Ocean Road* wanatoka Kanda ya Ziwa, lakini katika huduma zinazotolewa kwa sasa katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando zipo changamoto kubwa ikiwemo uhaba wa fedha wakati wa ku-service ile mashine. Hospitali yenyelewe haijitoshelezi na kusababisha huduma hiyo kusitishwa wakisubiri fedha na kuendelea kuleta usumbufu kwa wagonjwa katika Hospitali ya *Ocean Road*. Je, Serikali haionti haja ya kupeleka ruzuku ya kutosha katika kitengo cha saratani kilichopo Bugando?

Swali langu la pili, tafiti zinaonesha kuwa maji yaliyoachwa kwenye gari lilitopo kwenye jua na yakakaa kwa muda mrefu katika vyombo vya plastiki inaonyesha inapopata joto kuna *chemical* zinatoka kwenye plastiki aina ya *dioxin* ambazo zinaonyesha kuna uwezekano wa kupata saratani hususani saratani ya matiti. Je, Wizara ina mikakati gani ya kutoa elimu kwa wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, na wewe ni mtaalamu wa afya vilevile.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza kuhusu ruzuku kuongezwa kwa ajili ya kituo cha tiba ya saratani kilichopo Kanda ya Ziwa kwa maana ya Hospitali ya Rufaa ya Bugando ndiyo kwanza kimeanza kufanya kazi, kwa hiyo, tunatarajia uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo zitajitokeza mpaka pale ambapo kita-stabilize. Kwa hivyo, ninaomba niichukue hii kama changamoto na tutatazama changamoto hii inasababishwa na nini ili wakati wa

mchakato wa bajeti inayokuja, tuone ni kwa kiasi gani tunahitaji kuongeza ruzuku kwenye kituo hiki ili kiweze kutoa huduma bora zaidi katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili ambalo linahusu *plastics* ambazo zinatumika kuwekea maji ambayo yakikaa kwenye juu kwa muda mrefu inasemekana yanaweza yakasababisha saratani, hili ni jambo ambalo limekuwa likisemwa kwenye mitandao mara nyingi lakini halina ukweli wowote ule na naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kwamba Serikali iko makini na haiwezi kuruhusu kitu chochote kile ambacho kinauzwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kikawa na madhara kikaingia kwenye soko, kwa sababu tunafanya uchunguzi pia tunafanya udhibiti wa bidhaa zote ambazo zinaenda kutumika kwa wananchi kupitia taasisi yetu ya *Tanzania Foods and Drugs Authority (TFDA)* - (Mamlaka ya Chakula na Dawa) ambapo mambo yote haya yakisemwa ama yakizungumzwa kwenye jamii huwa tunayafanyia utafiti wa kimaabara na hatimaye kuthibitisha kama yana ukweli ama hayana ukweli ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili analolisema Mheshimiwa Komanya tulikwishalifanya kazi na tukabaini ni uzushi na halina ukweli wowote ule na kwa hivyo hakuna sababu ya kuendelea kuwatia wasiwasi wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Hospitali ya *Ocean Road* ambayo ndiyo maarufu na inafanya kazi kubwa ya kuhudumia wagonjwa hawa wa saratani ndiyo hospitali ya siku nyingi na miundombinu yake pia ni ya kizamani lakini idadi ya wanaopata huduma hapo imeongezeka maradufu. Mbali na hayo hospitali ile haifiki

kirahisi kwa sababu iko pembedi na vituo au barabara za usafiri wa umma kwa maana ya daladala. Hivyo, wananchi wanatakiwa kutembea umbali mrefu kwa zaidi ya kilometra moja kufika hospitalini pale umbali huu si rafiki kwa mgonjwa au watu wanopeleka wagonjwa hospitali. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hospitali nyingine kubwa ya kisasa jijini Dar es Salaam ili kuzihamisha huduma hizi za magonjwa ya saratani ziweze kufanyika katika kituo kimoja kikubwa na cha kisasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu anataka kujua ni lini tu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hatuna mpango kwa kweli wa kujenga kituo kingine cha kutoa tiba ya saratani katika Jiji la Dar es Salaam, kwa sababu kituo cha *Ocean Road* kinajitosheleza na kinajitosheleza kwa maana ya kutoa huduma kwa Kanda nzima ya Mashariki na hata wagonjwa wanaotokea Kanda ya Kati wanaweza wakapata huduma zao pale *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni moja kituo kile hakipaswi kuwa kama hospitali ya kwenda kila siku, kile kituo ni kituo cha rufaa. Kwa sasa kilikuwa ni kituo pekee cha rufaa cha Kitaifa lakini kwakuwa toka tumeingia Awamu ya Tano tumeanzisha utaratibu wa kufungua vituo vingine kwenye *satellites*/kwenye Kanda zote kwa maana ya Kanda ya Kusini pale Mbeya, Kanda ya Ziwa pale Bugando na Kanda ya Kaskazini pale *KCMC* ndio maana sasa tunakichukulia kituo hiki cha *Ocean Road* kama cha Kanda hii ya Mashariki na Kanda zozote zilizo karibu na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ile ya saratani inayotolewa pale ni ya rufaa ni huduma ya ngazi ya juu kabisa, kwa hivyo kwa vyovypote vile hatuwezi kusambaza huduma hizi kila sehemu kwamba tuweke na upande mwingine, hapana. Hospitali kubwa zipo nyingi Dar es Salaam ikiwemo ile mpya ya Mloganzila ambayo itatoa

huduma nyingine zozote pembedi lakini siyo huduma za saratani kwa sababu gharama za kuanzisha kituo cha saratani ni kubwa sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante tumekuelewa. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Maliasili Mheshimiwa Richard Philip Mbogo.

Na. 47

**Kubadili Mipaka ya Hifadhi za Misitu kwa
Mujibu wa Sheria ya Misitu**

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

Katika mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa Mkoa wa Katavi uliofanywa na Halmashauri ya Mpanda mwaka 2004 kwa kushirikisha ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wizara, zililipwa sehemu za Hifadhi za Misitu *North East Mpanda (JB94)* na Msanginia (*JB215*) na ramani mbalimbali kuidhinishwa ikiwemo 48870, 48893 na 40250.

Je, ni lini Serikali itabadili mipaka hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ya 2002 (Namba 14) Kifungu cha 28?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kufika siku hii ya leo. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuniamini na kunitfea katika nafasi hii. Tatu, nimshukuru Mheshimiwa Spika pamoja na uongozi mzima wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wenyeviti wa Kamati nilizokuwa Mjumbe kwa malezi yao ambayo wameyatoa kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa

Maliasili na Utalii naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misitu wa hifadhi wa Mpanda *North East* na Msangimya ni misitu ya Serikali inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Misitu wa *North East* Mpanda umehifadhiwa kwa tangazo la Serikali Na. 296 la mwaka 1949. Aidha, Misitu wa Msangimya umehifadhiwa kwa Tangazo la Serikali Na. 447 la mwaka 1954 na inasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 Sura ya 323.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ilipima maeneo ya Hifadhi ya Misitu wa *Mpanda North East* na Msangimya kupitia ufadhilli wa Shirika la Africare chini ya mradi wa *Ugalla Ecosystem* ili kuanzisha maeneo ya usimamizi wa Wanyamapori (*Wildlife Management Area-WMA*) na makazi pamoja na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji. Baada ya upimaji huo ramani 48870, 48893 na 40250 zilichorwa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya nia njema iliyokuwepo ya kuwapatia wananchi makazi yaliyopimwa kwa mujibu wa sheria na uanzishwaji wa maeneo ya usimamizi wa wanyamapori (*WMA*) na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji, utaratibu huu haukuzingatia Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009. Kwa mujibu wa kifungu cha 31(1) cha Sheria ya Wanyamapori, *WMA* zote zinaanzishwa kwenye misitu iliyoko kwenye ardhi ya kijiji au ardhi ya ujumla na siyo kwenye misitu ya Hifadhi ya Serikali Kuu. Aidha, mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji inafanyika kwenye ardhi ya kijiji husika na siyo kwenye misitu iliyohifadhiwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ardhi ya msitu wa hifadhi uweze kutumika kwa matumizi mengine, Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 katika kifungu cha 29 inatoa utaratibu wa kisheria wa kufuta hadhi ya msitu wa hifadhi ambapo Waziri wa Maliasili na Utalii anaweza kufuta sehemu ya msitu

au msitu wote wa hifadhi baada ya kujiridhisha kuna umuhimu ya kufanya hivyo. Mara baada ya mchakato huu kukamilika ndipo ardhi ya msitu itatumika kwa matumizi na shughuli zingine za kibinadamu mbali na uhifadhi. Aidha, Waziri wa Maliasili na Utalii atatoa maamuzi hayo baada ya kushauriana na Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Misitu (*National Forestry Advisory Committee*) ambayo inatajwa katika Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 katika Kifungu cha 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mchakato wa kupima sehemu ya misitu ya hifadhi niliyoeleza hapo juu umefanyika kinyume cha sheria na taratibu zilizopo, hadhi ya misitu hiyo ya hifadhi inaendelea kubaki kisheria kama ilivyoainishwa kwa mujibu wa matangazo ya Serikali niliyoyataja hapo juu. Aidha, Serikali itaangalia kama kunaweza kuwa na uwezekano wa maeneo hayo kutolewa kwa ajili ya matumizi mengine kwa mujibu wa sheria, lakini ikiweka kipaumbele kwanza kitatolewa kwa maslahi mapana ya Taifa na kwa kufuata ushauri utakaotolewa na Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Misitu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Pamoja na majibu ya Serikali, ningependa niikumbushe Serikali kwamba wakati Halmashauri ya Wilaya Mpanda inafanya mpango wa matumizi bora ya ardhi ilizingatia mahitaji ya wananchi pamoja na maendeleo yao kwa wakati huo, kwa sasa hivi tunavyozungumza Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi idadi yake ya wananchi imeongezeka. Haya matangazo ya Serikali, Tangazo Na. 447 ya mwaka 1954 Na. 296 ya mwaka 1949 hayaendani na uhalisia na hali ilivyo chini kutokana na ramani hizi kuidhinishwa na Wizara ya Ardhi mwaka 2008 na zilianza kuidhinishwa na ngazi ya Mkoa mpaka na Wizara ya Ardhi kwa Kamishna wa Upimaji na Ramani. Kwa sasa hivi tunaenda kwenye nchi ya viwanda na maeneo mengi yanahitaji wakulima kwa ajili ya kulima mazao mbalimbali

na Mkoa wa Katavi tuna mkakati wa kuanzisha zao la korosho. Kulingana na matangazo ya Serikali yanatofautiana na ramani zilivyo, uhalisia na mahitaji ya wananchi. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari hii Kamati ya Ushauri ya Taifa juu ya Misitu iambatane na Mbunge wa Jimbo la Nsimbo baada ya Mkutano huu wa Tisa kwenda kuangalia hali halisi ili waweze kumshauri Waziri na waweze kubadilisha mipaka kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Misitu ya mwaka 2002?

Swali la pili, kutokana na uhitaji mkubwa wananchi kwa maeneo haya na masika tayari imekwishaanza na tunajua Waziri wa Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 yeye ndiye mwenye dhamana ya kutoa kauli. Je, yuko tayari kuwaruhusu wananchi katika Kijiji cha Matandarani na Igongwe Kata ya Isalike waweze kupata maeneo ya kujihifadhi kwa kulima, wakati Kamati ya ushauri ikiendelea kupitia maeneo na kuweza kumshauri Waziri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, mko tayari kwenda naye? Ni hilo tu ndiyo jambo kubwa.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuko tayari baada ya Mkutano huu wa Tisa kumalizika Kamati ya Ushauri itapita maeneo yote ambayo yana migogoro nchi nzima ili iweze kumshauri Mheshimiwa Waziri na aweze kutoa maamuzi sahihi.

Swali la pili, kuhusu kulima ni kweli wananchi wale nimefika katika lile eneo wana matatizo mengi, lakini ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tulipokaa na Mheshimiwa *DC* pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri walikubali kwamba wametenga eneo la ekari zaidi ya 700 ambalo sasa linatolewa kwa wananchi wale ili waweze kuendelea na hizo shughuli. Kwa hiyo, hatutaweza kuruhusu kwa sasa hivi waendelee na shughuli hizo kwa sababu tayari wameshaondolewa na ukiwaruhusu kupanda zao la korosho ambalo ni la muda mrefu mpaka lije lianzu kuvunwa itakuwa ni muda mrefu sana, kwa hiyo tutakachokifanya ni kuwapeleka katika hayo maeneo ambayo tayari

yameshatengwa na Serikali ili waendelee na shughuli zao zile ambazo zipo.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe.

Na. 48

25% ya Ada ya Uwindaji - Kitalu cha *Kigosi North*

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Katika Wilaya ya Mbogwe kuna Kitalu cha *Kigosi North* kilichopo katika Pori la Akiba la Kigosi.

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kulipa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe asilimia 25 ya ada ya uwindaji?

(b) Je, ni lini Serikali italitengeneza greda lililoko Kifura Kibondo Makao Makuu ya Mapori ya Kigosi Moyowosi ili lisaidie matengenezo ya barabara ndani ya mapori haya?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imekuwa na utaratibu wa kutoa fedha kiasi cha asilimia 25 kwenye Halmashauri za Wilaya zinatokana na malipo ya ada ya wanyamapori (*game fees*) wanazowinda kwenye maeneo yanayopakana na Wilaya husika kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitalu cha *Kigosi North* kimekuwa kikitumika kwa ajili ya utafiti wa madini uliokuwa unafanywa na Kampuni ya *TANZAM* na siyo kwa shughuli za

uwindaji wa kitalii. Hali hiyo inafanya Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe isipate fedha za asilimia 25 kwa ajili ya uwindaji wa kitalii katika kitalu hicho. Kitalu cha *Kigosi East* ndiyo kitalu kilichotengwa kwa shughuli za uwindaji wa kitalii kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2018. Hata hivyo, mwekezaji katika kitalu hicho amejaribu kuleta wageni mara mbili mwaka 2013 na 2014 kwa ajili ya kuwinda lakini hakuweza kuwinda kutokana na kuwepo kwa ng'ombe wengi badala ya wanyamapori katika kitalu hicho. Kwa sababu hiyo, hakuna wanyamapori waliowindwa kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2016 kutokana na kuwepo kwa ng'ombe na hivyo kitalu husika kurudishwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jitahada za Serikali za kuondoa mifugo katika maeneo yote ya hifadhi, ni wazi kuwa mazingira ya asili pamoja na wanyamapori watarejea na hivyo kuwezesha kitalu hicho kutumika kwa uwindaji wa kitalii kuanza kufanyika. Kufanyika kwa uwindaji wa kitalii katika kitalu hicho kutawezesha upatikanaji wa fedha ambazo zitaweza kuanza kuwasilishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe. Wizara yangu inatoa wito kwa Wilaya zote zenye uvamizi wa mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kuhakikisha mifugo inaondolewa ili kurejesha hadhi ya vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutengeneza greda, Wizara yangu tayari imeshatengeneza greda liliopo Kifura katika Pori la Akiba Moyowosi Kigosi na sasa linafanya kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Augustino Manyanda.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hiki kitalu kimetolewa kwa ajili mambo ya utafiti wa madini lakini kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 ya Wanyamapori inazuia kufanyika kwa utafiti katika maeneo ya hifadhi. Je, ni taratibu zippi ambazo Serikali

imetumia kukigawa hiki kitalu ili kifanyiwe mambo ya utafiti wakati sheria hairuhusu?

Swali la pili, kwa kuwa mapori haya yana changamoto mbalimbali, je, Naibu Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi pindi Bunge litakapomiliza shughuli zake ili aweze kuja kuziona himo changamoto zinazoyakabili haya mapori na kuweza kuzitatua?

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi sana muda wetu umekwisha Waheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mbunge kwa kazi kubwa amekuwa akifanya katika kuwatetea wananchi wake wa Jimbo la Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TANZAM* ambaye alipewa kitalu hicho, kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 kifungu cha 20(2)kinazuia kabisa shughuli zote za utafiti wa madini ya aina zote kufanyika katika maeneo ya hifadhi. Hata hivyo, kifungu hicho cha 20(3)kinatoa mamlaka kwamba ni aina tatu tu za madini zinaruhusiwa kufanyiwa utafiti, madini hayo ni uranium, gesi na mafuta. Kufuatana na mwekezaji aliyekuwa amepewa hiki kitalu yeye alikuwa anafanya utafiti wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba pamoja na leseni ya huyu mwekezaji ilimalizika tereha 31 Desember 2014, baada ya kumalizika, tarehe 1 Juni, 2016 Serikali ilimuandikia barua ya kumuomba aondoke katika eneo na aondoe vitu vyote lakini hadi leo bado mwekezaji yule yupo opale na ameweeka vifaa vyake wakati hana leseni na ilishapita. Tarehe 28 Aprili, 2017 alikumbushwa juu ya suala hili na mpaka sasa hivi bado hajasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kutoa siku saba, yule mwekezaji aondoe hivyo vitu vyote, kwa sababu viko pale kinyume na taratibu na sheria iliyopo. (*Makofii*)

Baada ya kumalizika, tarehe 1 Juni, 2016 Serikali ilimuandikia barua ya kumuomba aondoke katika eneo na aondoe vitu vyote lakini hadi leo bado mwekezaji yule yupo opale na ameweka vifaa vyake wakati hana leseni na ilishapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Aprili, 2017 alikumbushwa juu ya hili suala na mpaka sasa hivi bado hajasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kutoa siku saba, yule mwekezaji aondoe hivyo vitu vyote kwa sababu viko pale kinyume na taratibu na Sheria iliyopo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab Mbunge wa Muheza.

Na. 49

Uuzaji wa Vitalu vya Miti kwa Njia ya Mnada Muheza

MHE.BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Vitalu vya miti ya tiki – Lunguza Muheza huuzwa kwa njia ya mnada hali inayosababisha viwanda vidogo vidogo vya Muheza kukosa miti.

(a) Je, ni lini Serikali itahakikisha wenye viwanda katika maeneo hayo wanapata vitalu ili kulinda ajira za wanavijiji?

(b) Je, kwa nini wanaopata vitalu wasichane magogo hayo hapo Wilayani ili kulinda viwanda vidogo vidogo vya Muheza?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi

Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye biashara ya miti ya misaji, njia mbili ambao ni mnada na makubaliano binafsi hutumika. Mbinu mbalimbali zimekuwa zikitumika katika kuuza miti ya misaji ili kuongeza bei ya miti kwa kutumia ushindani wa bei iliyopo sokoni. Hivyo, ili kupata bei ya soko, mbinu inayotumiwa ni pamoja na kuuza kiasi kidogo cha ujazo wa miti ya kuvuna kwa njia ya mnada. Hivyo, asilimia 30 ya malighafi inayotarajiwा kuvunwa katika shamba husika huuzwa kwa utaratibu huu. Njia hii inasaidia kubaini nguvu ya soko na kuongeza mapato ya Serikali. Njia ya makubaliano binafsi hutumika pia katika uuzaji wa miti mara baada ya bei ya soko kupatikana katika mnada. Hivyo asilimia 70 huuzwa kwa makubaliano binafsi ili kutoa fursa kwa wadau wengi zaidi kushiriki kwenye biashara hiyo. Utaratibu huu kwa kiasi kikubwa umewawezesha wenye viwanda wanaoshindwa kununua kupertia njia ya mnada kupata malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza wigo wa soko la ndani, Wizara imeanzisha utaratibu utakaowawezesha wanunuzi wengi wa miti ya misaji walioko nchini kunufaika. Utaratibu huu unawalenga wale wote wenye viwanda vinavyotengeneza samani vilivyopo nchini. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2017/2018 asilimia 10 kati ya asilimia 70 ya ujazo wa miti uliotengwa kwa ajili ya kuuzwa kwa njia ya makubaliano binafsi utauzwa kwa watengenezaji wa samani ndani ya nchi ili kuongeza thamani ya mazao yao na kuongeza ajira. Matangazo ya mauzo ya miti hufanyika kwa kubandika katika mbao za matangazo na kutolewa katika magazeti kwa muda wa siku 14 kabla ya mauzo. Wenye nia ya kuvuna na wenye kumiliki mashine za kupasua magogo ikiwemo wana vijiji wanaozunguka shamba letu la miti la Mtibwa na Longuza hupewa matangazo hayo kuhusu mnada huo ili nao waweze kujitokeza katika kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulinda viwanda vya ndani na kuongeza ajira kwa Watanzania, uchakataji wa magogo yanayovunwa katika mashamba ya miti hufanyika ndani ya

nchi. Baada ya kuuziwa malighafi kutoka katika mashamba ya miti, uchakataji hufanywa na mteja mwenyewe kulingana na mahali alipoweka kiwanda chake. Sheria na mwongozo wa uvunaji wa mazao ya misitu haimlazimishi mwenye kiwanda kujenga kiwanda mahali malighafi inapopatikana.

Nashauri Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kuhimiza Halmashauri zetu ziweke mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa viwanda vidogo na vikubwa katika maeneo yaliyo karibu na mashamba ya miti ili kuongeza ajira kwa wananchi wanaoishi karibu na mashamba hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza utaratibu huo ambao wa kuwauzia watu binafsi kwa makubaliano kwa asilimia 70 na huu wa asilimia 30 kwa kupeleka kwenye mnada hautumiki kabisa. Labda wanatumia asilimia 100 wanapeleka kwenye mnada. Kitendo hiki kimefanya vile viwanda vidogo vidogo Muheza pale, karibu viwanda kumi vyote vimekufa na ajira ambayo kila kiwanda kilikuwa kinachukua labda watu kutoka 100 – 150 wote kukosa kazi.

Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, kwa nini wasirudishe ule utaratibu ambao ulikuwepo wa hiyo asilimia 70 kwa makubaliano ili wale wenye viwanda vidogo vidogo ambao wanatunza ile misitu(tiki) pale waweze kupata ajira na kuendelea kupata morali ya kuanza kutunza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwa nini hata wale ambao wanunuwa kwa mnada ambao utakuta anakuja tajiri mmoja ananunuwa mitiki yote pale. Sasa ni kwa nini na yeye asilazimishwe kutengeneza kiwanda cha kukata ile mitiki pale pale Muheza kwa sababu hayo ni madaraka ambayo anayo Waziri kufuatana na *regulations* ambazo anazitengeneza? Nakushukuru Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, muda wetu umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba ukiuza kwa njia ya mnada wananchi wengi wanakuwa hawana uwezo wa kushinda ndiyo maana tumeweka utaratibu kwamba ni asilimia 30 ndiyo itakayouzwa kwenye mnada. Asilimia 30 itategemeana na makubaliano binafsi, maana yake tunafuata bei ile iliyokuwa na mnada, tunaangalia viwanda vyote vilivyoko katika eneo husika. Wale wote wanaohitaji wanapeleka maombi na wanapatiwa ili waweze kujijengea uwezo na kuweza kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la pili ambalo amesema kwamba tumshauri huyu atakayekuwa ameshinda aweze kuwekeza katika eneo husika mimi nafikiri ni ushauri mzuri. Tatalifanyia kazi mara tutakapopata muda husika.Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Wizara ya Madini Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga kwa niaba, Mheshimiwa Kiswaga.

Na. 50

**Kuzifutua Leseni Kampuni za Wachimbaji Wasiofungua
Migodi**

**MHE. KISWAGA B. DESTERY (K.n.y. MHE. NJALU D.
SILANGA) aliuliza:-**

Maeneo mengi yamefanyiwa utafiti na kampuni za kigeni kwa muda mrefu bila kufikia hatua ya kufungua migodi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifutia leseni kampuni hizo na kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo?

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwanza kabisa na mimi kwa sababu nimesimama hapa kwa mara yangu ya kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii kufika hapa leo. Vilevile nimshukuru pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuniamini na kuniweka katika Wizara hii mpya. Vilevile nimshukuru Mheshimiwa Spika, Wabunge wote na Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa malezi yao mazuri na kunifikisha hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo napenda sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga liloulizwa na Mheshimiwa Kiswaga ambaye ni Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kanuni zake inatambua umiliki wa leseni za utafutaji mkubwa wa madini na uchimbaji mdogo wa madini inayotolewa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kama ilivyorekebishwa mwaka 2017, leseni za utafutaji wa madini aina ya metali, viwandani na nishati (makaa ya mawe na urani) hutolewa kwa muda wa miaka minne ya awali na kuhuishwa kwa mara ya kwanza kwa miaka mitatu na mara ya pili kwa miaka miwili. Hivyo leseni ya utafutaji mkubwa wa madini ya aina hizo hubaki hai kwa kipindi cha miaka tisa. Aidha, leseni za utafutaji wa madini na vito na ujenzi hutolewa kwa mwaka mmoja na haziwezi kuhuishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo mmiliki wa leseni atashindwa kuendesha shughuli za utafutaji wa madini, leseni yake hufutwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Marekebisho yake ya mwaka 2017. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017 jumla ya leseni 423 za utafutaji wa madini zilifutwa ambapo mwaka 2014/2015 zilifutwa leseni 2013, mwaka 2015/2016 zilifutwa leseni 155 na mwaka 2016/2017 zilifutwa leseni 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la leseni liliolofutwa hutathminiwa na Wakala wa Jiolojia yaani *Geological Survey of Tanzania (GST)* kwa ajili ya kutengwa kwa wachimbaji wadogo endapo litaonekana kuwa na mashapo yenyе tija. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017 jumla ya maeneo 19 yenyе ukubwa wa jumla takriban hekta 69,652.88 yalitengwa kwa wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia na kujadiliana na kampuni zilizomiliki leseni za utafutaji wa madini ili kuona uwezekano wa kuachia baadhi ya maeneo yanayofaa kwa uchimbaji mdogo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali.

Kwa kuwa Serikali imekiri kufuta leseni 423 yenyе eneo la hekta 69,652.88; je, Serikali iko tayari kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo eneo hili ambalo limefanyiwa utafiti ili waweze kujiajiri na kujipatia ajira na waweze kulipa kodi stahiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, Serikali iko tayari kuwanunulia vifaa vinavyohusiana na wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kukodisha kuliko ilivyo sasa wanachimba bila utaalalm na vifaa vinavyostahili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Waheshimiwa tutakuwa hatuna tena maswali ya nyongeza kutokana na muda.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la kwanza ni kwamba Serikali iko tayari kuwasaidia wachimbaji wadogo. Imekwisha kutenga maeneo 11 ambayo yana jumla ya hekari 38.9 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, kwa maeneo haya ambayo yamesharudishwa Serikalini, Serikali itaendelea kufanya

mpango wa kuweza kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kuchimba na wao waweze kupata faida na waweze kunufaika na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wachimbaji wadogo kuitia ruzuku iliyokuwa inapitia *SMMRP* ambayo ilikuwa inatoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo na wadau wengine wa uchimbaji iliweza kutoa fedha ili kuweza kuwasaidia wadau waweze kununua vifaa kwa ajili ya uchorongaji, kufanya utafiti na kuweza kusaidia wale wachimbaji wengine wadogo wadogo kwa kukodisha. Lakini vilevile *STAMICO* ambayo iko chini ya Wizara ya Madini pamoja na *GST* na yenye we ina juhudzi za dhati kabisa kununua vifaa ambavyo wachimbaji wadogo watakuwa wanakodisha ili waweze kujua mashapu yaliyopo ni mashapu ambayo yana faida ambayo wanaweza wakachimba na wakapata uchimbaji wa tija ili kujiondoa katika ule uchimbaji amba wanachimba kwa kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali iko pamoja na wachimbaji wadogo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa. Ahsante. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, kwa niaba yake, Mheshimiwa Mchengerwa.

Na. 51

Hitaji la Transfoma Maeneo ya Munguatosha na Hondogo

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA (K.n.y. MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE) aliuliza:-

Maeneo ya Munguatosha na Hondogo ni baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji transfoma ili umeme uwake.

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kupeleka transfoma katika maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Hondogo kimewekwa katika mradi wa *REA Awamu ya III* kupitia Mradi wa *Densification* Awamu ya Kwanza ulioanza mwezi Machi, 2017 unaotekelawa na kampuni ya *STEG*. Mkandarasi tayari amesimamisha nguzo 111 na kuvuta waya wenye urefu wa kilometra 4.5. Hatua inayofuata ni ufungaji wa transforma yenye uwezo wa kVA 50 itakayofanyika mwishoni mwaka mwezi Novemba, 2017. Wateja wapatao 65 wanatarajiwaa kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitongoji cha Munguatosha kilichopo katika Kijiji cha Makore kimejumuishwa na kitapatiwa umeme kupitia *REA awamu ya III* chini ya *Grid extension* utakaotekelawa na kampuni ya *Sengerema Engineering Group Limited*.

Kazi ya kupeleka umeme katika Kitongoji cha Munguatosha inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra mbili, ufungaji wa transforma yenye uwezo wa kVA 50 pamoja na kuunganisha wateja wapatao 46. Utekelezaji wa mradi huu uliana mwezi Julai, 2017 na utakamilika mwezi Juni, 2019.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kilio kikubwa sana cha mahitaji ya umeme Kata ya Mkange pale Chalinze ukizingatia kuwa sehemu hii inachangia kwenye uchumi wetu wa Taifa hususan katika Wilaya ya Bagamoyo, pia na Halmashauri ya Chalinze na Tanzania kwa ujumla hususan katika viwanda pamoja na utalii.

Je, Serikali inajipangaje kusaidia wananchi pamoja na wawekezaji wa viwanda umeme ili kupunguza ukali wa maisha wa eneo hili la Kata ya Mkange? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa *Stiglers Gorge* unadhamiria kuikomboa nchi yetu katika umeme hususan katika viwanda vinavyojengwa pamoja na treni hii ya umeme.

Je, Serikali inawaachaje wananchi wa Jimbo la Rufiji ambao wametunza bwawa hili pamoja na Mto Rufiji kwa miaka mingi sana hususan wakazi wa Kata ya Mwaseni, Kipugira, Ngorongo na Mkongwa? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Hilo swali umechomekea lakini Waziri lijibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Mchengerwa na naomba nimpongeze kwa jitihada zake za kufuatilia changamoto mbalimbali za nishati katika jimbo lake pamoja na muuliza swali la msingi. Ameuliza swali juu ya mahitaji ya umeme kwenye Kata ya Mkange iliyoko Jimbo la Chalinze na ni kweli Kata hii ya Mkange imepakana na Mbuga ya Saadani.

Naomba nimtaarifu kwamba katika mradi ambao unaendelea wa *Urban Peri Urban Edification Project of Coast Region* na Kigamboni – Kata ya Mkange itapata umeme kuititia Miono. Kwa hiyo, naomba nimtaarifu kwamba Serikali imezingatia na kwa kuwa ina dhamira kwamba kila kijiji ifikapo 2020/2021 kipate umeme kwa hiyo Kata ya Mkange itapata umeme kuititia Miono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameulizia suala la *Stiglers Gorge*. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu ni kweli Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kwa dhati kuongeza upatikanaji wa nishati nchini kwetu na imedhamiria kwa dhati kutekeleza mradi huu ambao utaongeza megawati 2100, *tenderimeshatangazwa* na zaidi ya makampuni...

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Pwani eneo la Rufiji Kata alizotaja Mwaseni na Ngorongo ni Kata ambazo ni kweli zimetunza bwawa hili na zitafaidika kwanza kupitia upatikanaji wa nishati hii ya umeme lakini pia kupitia ajira ambazo zitapatikana kipindi cha ujenzi wa bwawa hili, lakini tatu, Wilaya hii ya Rufiji imekuwa ikikumbwa na mafuriko ya mara kwa mara. Kupitia ujenzi wa bwawa hili ni dhahiri kwamba ule uhifadhi wa maji utasaidia kuzuia masuala ya mafuriko katika maeneo haya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ahsante!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: ...lakini langu lingine pia ujenzi wa bwawa hili litasaidia shughuli za kilimo cha umwagiliaji kwa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Watanzania muamini mradi huu unatekelezwa kwa pesa za ndani za nchi yetu. (*Makofii/Vigelegele*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Pascal Haonga.

Na. 52

Vigezo Vinavyotumika Kupata Mikopo Elimu ya Juu

MHE. PASCAL Y. HAONGA aliuliza:-

Kigezo kimojawapo cha kuwanyima mkopo waombaji wa mkopo ya elimu ya juu ni kama muombaji alisoma shule za binafsi.

(a) Je, Serikali haioni kuwa baadhi ya wanafunzi hulipiwa ada ya shule za binafsi na ndugu, jamaa, marafiki na *NGO's* hivyo wanafunzi hao wanapofikia elimu ya juu hushindwa kumudu gharama za elimu hiyo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kufuta kigezo hicho ili kuwapatia waombaji wa mikopo haki yao ya kupata elimu ya juu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga Mbunge wa Mbozi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa za msingi za kupata mkopo wa elimu ya juu zinaainishwa katika kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya 2004 (Sura ya 178) ya Sheria za Tanzania kama ifuatavyo; awe Mtanzania, awe amedahiliwa kwenye chuo kinachotambulika, awe ameomba mkopo kwa njia ya mtandao, awe hana chanzo kingine cha kugharamia elimu yake. Mbali na sheria, vigezo vingine ni uyatima, ulemavu, uhitaji na mahitaji ya rasilimalwatu kwa ajili ya vipaumbele vya maendeleo vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuwasilisha maombi ya mkopo wa elimu ya juu muombaji hutakiwa kuwasilisha taarifa muhimu zikiwepo shule au vyuo alivyosoma kabla ya kuijunga na elimu ya juu. Bodi ya Mikopo hutumia taarifa hizi ili pamoja na mambo mengine kubaini historia ya uchangiaji wa ghamama za elimu katika ngazi ya sekondari au chuo ili kumpangia mkopo stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale inapothbitika kwa maandishi kwamba mwanafunzi husika alisaidiwa au kufadhiliwa na ufadhilli huo umekoma Bodi ya Mikopo huwakopesha kwa kuzingatia hali zao za kiuchumi kwa wakati huo. Kwa mfano, katika mwaka wa masomo wa 2016/2017 jumla ya wanafunzi 719 waliothibitika kufadhiliwa au kusaidiwa katika masomo yao ya sekondari walipata mkopo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCHAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, siku za hivi karibuni tumeisikia Bodi ya Mikopo imeongeza masharti au vigezo vipyta kwa wakopaji, kwa mfano wale viongozi wanaojaza fomu za maadili ya viongozi wa umma wakiwepo Madiwani nao pia ni mionganini mwa watu ambao watoto wao wananyimwa mikopo. Kwa kuwa tunajua kabisa kwamba Madiwani hawana mishahara na wanategemea posho ambayo ni kidogo sana je, Serikali haioni kwamba, huu ni unyanyasaji ambao kwa namna yoyote hauvumiliki na hitakiwi kuufumbia macho unaofanywa na Bodi ya Mikopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, siku za hivi karibuni wote tunajua kabisa kwamba Bodi ya Mikopo imeongeza makato kwa wanufaika wa mikopo. Kwa mfano awali ilionekana kwamba, wanufaika wa mkopo walikuwa wanalipa wanarejesha asilimia nane ya mkopo waliokuwa wamekopa kwa maana ya makato ya asilimia nane, lakini kwa sasa wanakatwa asilimia 15. Hali hii imesababisha wale wanufaika wa mkopo kama walimu na watumishi mbalimbali ambao walikuwa wamebakisha fedha kidogo ambazo walikuwa wanapata mwisho wa mwezi, leo hawana mshahara hata kidogo na kuna watumishi wanaacha kazi. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kurudi kwenye asilimia nane ya makato, ili angalao watumishi hawa waliocha kazi waweze kurudi makazini na maisha yaweze kwenda vizuri? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alivyosema kwamba katika mwaka huu wa masomo kuna vigezo vimeongezwa kwa ajili ya watu ambao hawastahili kupata mikopo, ikiwa ni pamoja na viongozi wa umma wanaojaza fomu za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa umma. Lengo

la kufanya hivyo ni kwamba, tunajaribu kuhakikisha kwamba mkopo ule unatumika kwa wale ambaao hawana uwezo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuhusu Madiwani kama wana uwezo au hawana uwezo tunajaribu kuangalia kipato chao wanachowenza kupata kwa mwaka na kulinganisha na Watanzania wengine wengi ambaao hawana kipato kabisa. Kwa hiyo, lengo ifahamike tu ni kwamba ni kujaribu kutoa fursa kwa wale ambaao hali yao ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hitaji la sasa la kwamba waombaji wa mikopo ambaao wanatakiwa kurudisha wanakatwa asilimia 10 inatoka kwenye mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba mkopo ule ukishachukua kigezo cha pekee cha kwamba unatakiwa kurudisha fedha ni kwamba wewe umekopa, maana yake ilitakiwa pale unapomaliza shule uanze kurudisha.

Sasa kwa muda mrefu sana ule mkopo umekuwa unashindwa kuwanufaisha watu wengi kwa sababu watu wengi hawarudishi na ndio maana sasa tumelazimisha kwamba, ni lazima kwamba, mtu ambaye atakuwa amepata ajira aweze kulipa kwa asilimia 15 ya mshahara wake, lakini vilevile kuna kigezo kingine ambacho tumeweka kwamba, tunatoa kipindi cha mpito au *grace period* ya miezi 24 toka mwanafunzi amalize shule, lakini baada ya hapo kama hajaanza kulipa tunaanza vilevile kutoza riba ya asilimia 10. Lengo ni kwamba tunahitaji kuufanya mfuko ule uwendelevu ili wananchi wengi waweze.

Waheshimiwa Wabunge nafahamu kuna baadhi ambaao nao wanadaiwa mikopo, katika siku hizi za karibuni tunakuja na orodha ya wale ambaao ni wadaiwa sugu. Kwa hiyo, nawaombeni ushirikiano...

MWENYEKITI: Mheshimiwa waandikie barua, inatosha.

Tunaendelea Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini.

Na. 53

Kushuka kwa Uzalishaji wa Zao la Kahawa

MHE. MARTIN M. MSUHA aliuliza:-

Kwa takwimu za miaka ya hivi karibuni uzalishaji wa kahawa Wilayani Mbinga umeonekana kushuka kwa mkulima mmoja mmoja (*out growers*). Na sababu mojawapo ya kushuka kwa uzalishaji huo ni kuzeeka kwa miti ya kahawa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea wakulima wa Mbinga mbegu mpya ili kuinua uzalishaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mnada wa kahawa Wilayani Mbinga, badala ya minada hiyo kuendelea kufanyika Moshi?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupiga marufuku kabisa uuzaaji wa kahawa mbichi ikiwa shambani, maarufu kama "magoma" Wilayani Mbinga?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martin Msuha, Mbunge wa Mbinga, swali lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali wa kuwapelekea wakulima wa Mbinga mbegu mpya ili kuinua uzalishaji ni kwa kutekeleza mpango mkakati wa kuendeleza zao la kahawa kwa miaka kumi (2011 – 2021). Katika mpango huo utafiti na usambazaji wa miche bora, ili kuondokana na miche yenye tija duni na ilio zeeka ni mojawapo ya kipaumbele. Utekelezaji wake unafanyika kwa kushirikiana na wadau, hususan *Tanzania Coffee Research Institute*

(*TaCRI*). Kituo cha utafiti na uzalishaji miche cha Ugano kilichoko Wilayani Mbinga katika mwaka 2016/2017 kilizalisha na kusambaza miche bora ya kahawa 270,869 na kazi inaendelea. Aidha, Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa (*Tanzania Coffee Development Fund*) umefadhili na kupunguza bei kutoka shilingi 300 kwa mche mmoja hadi shilingi 150 kwa vituo vyote nchini vilivyoko chini ya *TaCRI* ili miche hiyo isambae kwa kasi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada wa kahawa huendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Kahawa Namba 23 ya mwaka 2001. Serikali haina mpango wa kuanzisha Soko la Mnada wa Kahawa - Mbinga au mahali pengine nchini kwa sababu, uwepo wa miundombinu ya mashine ya kielektroniki ya kuendesha mnada iliyopo Moshi, maabara ya kuonjea kahawa, wataalam wa kuendesha mnada hu, gharama za mnunuzi ambapo atalazimika kwenda katika kila mnada, kama utawekwa kila mahali ambapo kahawa inazalishwa uzoefu unaonesha kuwa nchi nyngi duniani huweka mnada sehemu moja tu, ili kurahisisha uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tangu kuanzishwa kwake kabla ya uhuru mnada uliwekwa Moshi kwa kuwa ndiko kulikua na wanunuzi na biashara ukilinganisha na maeneo kama Kagera, ingawa uzalishaji unafikia hadi asilimia 40 ya nchi nzima. Mnada unauza kahawa ikiwa kwenye maeneo ya uzalishaji kwa mfano kule Mbinga na Mbeya, n.k. KInachopelekwa Moshi ni sampuli tu kwa ajili ya uonjaji.

Aidha, Serikali imeanzisha soko la bidhaa (*Commodity Exchange*) ili kupunguza gharama za uendeshaji wa masoko ya mazao ikiwemo kahawa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu Namba 29(ii) cha Kanuni za Kahawa 2013, ni kosa kwa mtu yeoyote kununua matunda ya kahawa (*ripe cherry*) kwa hiyo, Serikali inakataza biashara ya kahawa mbichi. Naomba nitoe agizo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbinga na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla, wote kwa pamoja na wahusika wengine wote kwamba, hairuhusiwi kabisa uuzaaji wa kahawa mbichi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martin.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, jambo mojawapo linaloyumbisha uzalishaji wa kahawa hususan Mbanga, ni kutokuwa na bei ya uhakika mwaka hadi mwaka. Je, Serikali haionti umuhimu wa kuanzisha mfuko wa kuimarisha bei ya mazao hususan kahawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi baada ya mkutano huu, ili akajionee mwenyewe ni jinsi gani utekelezaji na uzambazaji wa miche mipya ya kahawa unavyofanyika na Kituo cha *TaCRI* - Ugano, kama ilivyojibwa kwenye swali la msingi? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimponeze sana Mheshimiwa Mbunge wa jimbo hilo kwa ajinsi ambavyo anafuatilia kwa ukaribu sana katika zao zima hili la kahawa katika Jimbo lake. Lakini nikija katika swali lake la (a) ni kwamba, sisi kama Wizara kupitia Bodi ya Kahawa tunatoa bei elekezi kwa wakulima wale wadogowadogo wote kwa maana ya kwamba, *farm gate market* kwamba wawe wanapata bei elekezi kupitia njia ya mtandao wa simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tumegundua kwamba, njia hii ya mtandao wa simu iko *more effective* ukilinganisha na ile minada mingine, lakini hii tunaifanya kila wiki. Lingine naomba nitoe rai hata kwa wakulima wale wadogowadogo wote katika mashamba kwamba, wanapaswa wazingatie sana ubora wa zao hili la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine vilevile kule Moshi ambako tunafanya mnada, huu mnada kule Moshi hatuwezi tukafanya kwa bei elekezi kwa sababu, mnada wa kule unategemea sana soko la dunia na kwa maana hiyo, soko la dunia inategemea na wakati wa ile *market price* iliyoko wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kuongozananae kwenda kujithibitishia zao la kahawa. Ahsante.

MWENYEKITI: Hilo la mwisho ndio muhimu, muende wote hilo.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Swali la maji limetuchukulia muda mwingu sana. Sasa ni muda wa matangazo, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni 30 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, ambao ni vijana wawakilishi kutoka Wilaya za Kibaha, Temeke, Mtwara, Ilala, Lindi na Kilombero wanaojishughulisha na Mradi wa Uvezeshaji Vijana Kiuchumi unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya na kusimamiwa na Shirika la *Plan International*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna wageni 108 wa Mheshimiwa Antony Mavunde Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu ambao ni wanafunzi 103 wa kidato cha sita na walimu watano kutoka *Dodoma Secondary School* Mkoa wa Dodoma. Karibuni Dodoma. (*Makofi*)

Kuna wageni kumi wa Waheshimiwa Wabunge Edward Mwalongo na Joram Hongoli, ambao ni walimu nane na wanafunzi wawili kutoka Mkoa wa Njombe. Karibuni Bungeni. (*Makofi*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Jitu Soni (Mbunge), ambao ni watendaji walioko masomoni, wanatokea Babati, Mkoa wa Manyara. Karibuni. (*Makof*)

Wageni 36 wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ambao ni viongozi na wachezaji wa timu kutoka Mkoa wa Mara, wakiongozwa na Ndugu Issa Salote. Karibuni Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Joyce Sokombi anaomba kumtambulisha mgeni wake anaitwa Lucy Miliga kutoka Iringa, karibu. (*Makof*)

Kuna tangazo Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa Mbunge, Jimbo la Amani anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa uongozi wa *Fantasy Village* unawaallika Waheshimiwa Wabunge wote kwenye sherehe ya uwekaji wa jiwe la msingi la Hoteli ya *Fantasy Village* iliyopo Msalato Senje, kwa Mwinyi, kesho siku ya Jumamosi, tarehe 11 Novemba, saa 04:00 asubuhi katika viwanja vya hoteli hiyo. Aidha, mgeni rasmi katika sherehe hiyo ni Mheshimiwa Job Yustino Ngugai Mbunge, Spika, wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mnaombwa wote kuhudhuria bila kukosa. Karibuni sana, ahsanteni. (*Makof*)

Tangazo la semina; Waheshimiwa kesho Jumamosi, tarehe 11 Novemba, kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli kwa mwaka 2017 (*The National Shipping Agency Bill, 2017*). Semina hiyo, itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 04:30 asubuhi. Na Jumapili, terehe 12 Novemba, 2017 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu Kampuni ya *Maxcom Africa Plc, Max Malipo*. Semina hiyo pia itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa na itaanza saa 05:00 asubuhi, Wabunge wote mnakaribishwa.

Katibu.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:
Hoja za Serikali.

MWENYEKITI: Ngoja, ngoja.

MHE. MBUNGE FULANI: Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chumi pamoja na Msigwa, wawili tu leo.

Mheshimiwa Amina, kaa *please*.

Waheshimiwa saa 5:15 asubuhi hii, saa nyingine maswali yanakuwa mengi ya nyongeza yanatuchukulia muda mwingi sana kwa hiyo, tuvumilliane.

Mheshimiwa Chumi.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa naomba Muongozo kutokana na jambo lililotkea leo kutoka swalii namba 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taasisi moja imetoa matangazo ya kwamba wanafunzi waliokosa mikopo watapata mikopo *wa-apply* kwenye hiyo taasisi na *application fee* ni shilingi 30,000.

Sasa nilipenda kufahamu u-*genuine* wa hii taasisi, *what suppose* watoto wakalipa hiyo shilingi 30,000, *let say* wamelipa watoto 10,000, wamepata karibu milioni 300, halafu mwisho wa siku taasisi ikaja kutoa mikopo kwa watu kumi. Kwa hiyo, nilitaka nifahamu Muongozo wa Serikali *how genuine is that* taasisi inayotaka kutoa mikopo? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nimesimama hapa kwa Kanuni ya 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imechoma vifaranga 6,000 vya mfanyabiashara wa Kitanzania alivyovinunua kutika Kenya kinyume kabisa na *Wildlife Act* ya 2008 ya Haki za Wanyama. Na kama vile haitoshi ng'ombe wa Kenya 1,300 waliokuja Tanzania walitaifishwa na Serikali wakanadiwa kwa wastani wa ng'ombe mmoja kunadiwa kwa shilingi 71,000. Na hivi karibuni tumemsikia Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Amina Mohamed, akilalamika juu ya mahusiano mabaya ya kidiplomasia ambayo tunayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimnukuu Rais Kikwete wakati anaondoka madarakani, ilikuwa tarehe 6...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, nenda kwenye hoja moja kwa moja.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio naenda, naomba univumilie kidogo, samahani. Ilikuwa tarehe 06/10/2015 alisema; "Naondoka nikiwa naacha uhusiano wa Kenya na Tanzania ukiwa mzuri kuliko wakati mwenginee wowote, nina uhakika hautabadilika labda tupate mpumbavu kwelikweli na wa ajabu sana, ambapo kwa Tanzania watu wapo wachache sana wa aina hiyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mahusiano na nchi jirani ni ya muhimu kwa ajili ya biashara na matengamano ya kimahusiano. Jambo hili limekera sana na linaharibu mahusiano yetu na Kenya. Na Wakenya wamekamata ng'ombe 4,000 lakini kwa sababu ya mahusiano wanaona wasiwanadi kama ambavyo tumefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba hili jambo tulijadili kama jambo la dharura, ili tujenge mahusiano na nchi

nyingine kwa ajili ya ustawi wa jamii yetu. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kaeni kwanza. Bunge hili linaendeshwa kwa Kanuni Mheshimiwa Msigwa, Waheshimiwa Wabunge. Mambo ambayo Kanuni uliyotumia ni jambo lillilotokea mapema Bungeni, ambalo umekiuka Kanuni hiyo. Umeleta jambo nje ya Kanuni hiyo, saa nyingine huwa tunavumilia sababu tunataka Wabunge tunapowakubalia linapohusu majimboni mwenu, ili na ninyi mpumue, ili wapiga kura wenu wawasikie namna mnavyowatetea.

Sasa Mwongozo huu, hoja yako wewe...

MBUNGE FULANI: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Aah, sasa si ndio nakuja na nini.

MBUNGE FULANI: (*Hapa hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Sawa. Sasa mimi sijalionia kama lina udharura kwa kipindi hiki. Nitakuomba ulichukue ulipeleke kwenye Kamati inayohusika, ili wakalijadili wao na wao watakuwa majibu.

Waeshimiwa Wabunge, hili suala la elimu Serikali hebu lijibuni.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kutoa ufanuzi kuhusiana na taasisi ambayo inajita Mfuko wa Elimu ya Juu (*Tanzania Social Support Foundation*) ambayo ni kweli imekuwa ikitoa matangazo kwamba inatoa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Wizara yangu haiitambui hiyo taasisi na nieleze kwa masikitiko kwamba nimepewa gazeti sasa hivi ambalo linaonesha tangazo kwamba hii taasisi inawatangazia wanafunzi na

inawachaji shilingi 30,000 na wanasema watakuwa na mukutano ambao mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Elimu, Profesa Joyce Ndalichako. Sitiambui hii taasisi, hawajanikaribisha na tarehe ya huo mukutano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kutoa tahadhari kwa Watanzania kwamba wawe makini kwa sababu unapoona mtu anatumia jina lako kabla hata hajafika kwako, ni jambo ambalo kama Serikali niseme tumelipokea totalifanyia kazi, ili kujuu uhalali wake. Na kwa kipindi hiki nitoe tahadhari kwa watu ambao wataamua kulipa hizo shilingi 30,000, wafanye lakini wajue kwamba Serikali haihusiki na jambo hili. Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na
Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2018/2019**

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:
Kamati ya Mipango.

KAMATI YA MIPANGO

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Tukae.

Waheshimiwa tunaanza na ratibab yetu ya Mipango na tunaanza na Mheshimiwa Nape, ajiandae Mheshimiwa Turkey.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2018/2019. Pamoja na kazi nzuri na jitihada kubwa ambayo inafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuleta maendeleo katika nchi yetu. nimepongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji kwa wizara kwa kazi mnayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umeletwa hapa ili tuuboresheshe, tutoe mawazo yetu ambayo yanaweza kutumika kuboresha ili tufikie lengo la kuleta maendeleo katika nchi yetu. Na mimi nina amini Waziri na wenzake watatusikiliza na watachukua mawazo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma haya mapendekezo ya Mpango, utagundua humu ndani imenorodheshwa miradi mikubwa ya aina mbili; unaweza uka-group unavyoweza lakini iko ya aina mbili. Iko miradi ambayo ni ya kihuduma, miradi ambayo inahusiana na maji, afya, elimu, utawala na maeneo mengine. Miradi ambayo kwa asili yake haiendeshwi kibiashara, lakini upande wa pili kuna miradi ambayo kwa asili yake inaweza kuwekezwa na kuendeshwa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu mgawanyo wa aina hizi mbili za miradi, niliposoma nilishtuka kidogo kuona Serikali inapendekeza kuwekeza pesa za Serikali kwenye miradi ambayo inaweza kuendeshwa kibiashara. Nilitegemea miradi hii tungeruhusu sekta binafsi, tukatengeneza mazingira mazuri ya sekta binafsi kuwekeza kwenye miradi hii badala ya kuchukua pesa za Serikali na kuipeleka kule kwa sababu madhara yake ni makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mpango huu utatekelezwa kama ulivyo, miradi hii inakwenda kuua uchumi wa nchi yetu. Nitatoa mfano, miradi hii mikubwa ambayo ninaizungumzia ni miradi kama ya uzalishaji wa umeme na hapa imekuwa ikizungumzwa *Stiegler's Gorge* kwa mfano, miradi ya ujenzi wa reli, uboreshaji wa Shirika la Ndege, mraidi

wa bandari na baadhi ya barabara ni miradi ambayo kwa asili yake inaweza kuwekezwa kibashara, kuendeshwa kibashara na ikajilipa kibashara. Sababu ya kuchukua hela za Serikali kupeleka kwenye miradi hii kwa kweli sijaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ya miradi hii kwanza ni miradi mikubwa sana, lakini ya pili kwa ukubwa wake ni miradi ambayo ina gharama kubwa; ukiingalia ni mabilioni kadhaa ya dola kwa asili yake, lakini sifa ya tatu miradi hii niliyoitolea mfano hapa ni miradi ambayo uwekezaji wake utachukua muda mrefu na hivyo *payback period* yake ni ya muda mrefu sana. Sio miradi ya kulipa kesho, ni miradi ambayo itachukua muda mrefu kwa vyovypote vile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi siipindi miradi hii naomba niweke rekodi vizuri isipokuwa ninapingana na mapendekezo ya Serikali ya namna ya kuiwekeza na kuindesha miradi hii kwa kutumia pesa za Serikali. Tafsiri ya uamuzi wa kutumia pesa za Serikali kwenye miradi hii ni hii ifuatayo:-

Moja, itailazimisha Serikali kukopa hela nyingi kwa vyovypote vile kwa sababu ni miradi mikubwa, gharama yake ni kubwa, kwa hiyo ni lazima Serikali iende ikakope. Serikali ikienda kukopa na kwa sababu miradi hii inachukua muda mrefu, maana yake ni moja tutaanza kulipa deni hilo lilitokopwa kabla ya miradi hii haljaanza kulipa faida kwa nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tafsiri yake ni kwamba tutachukua hela kwenye maeneo mengine tuilipie deni miradi hii. Hapo maana yake ni kwamba tutaendelea kufunga mikanda muda mrefu, sasa tunafunga mkanda kwa nini? Ndio maana nahoji kwa nini Serikali inafikiri kwamba kuwekeza pesa za Serikali kwenye miradi ambayo ingeweza kuwekezwa kibashara na sekta binafsi ni jambo la tija kwa uchumi wa nchi yetu, mimi nadhani hapana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovypote vile ukichukua pesa za maeneo mengine maana yake utaathiri maeneo

hayo, maana yake utaathiri miradi ile ya huduma kama maji, afya, elimu na utawala na mtafika mahali hata malimbikizo ya wafanyakazi itashindikana kulipa kwa sababu tunachukua pesa za Serikali kuzipeleka kwenye miradi ambayo ingeweza kuijendesha kibiashara. Kwa hiyo, mimi nadhani hili la kwanza sio sahihi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna madhara makubwa kwa Deni la Taifa kuchukua hela za Serikali ambazo nyingi kama nilivyosema itabidi tuzikope kuziwekeza kwenye miradi hii. Na hapa Waheshimiwa Wabunge nataka twende kwa takwimu vizuri kwa mahesabu na ndipo hapa ninapohoji uzalendo wa wachumi wetu kuishauri Serikali na Mheshimiwa Rais kuwekeza hela za Serikali kwenye miradi hii, hapa mimi napata taabu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti uliyotupa hapa Mheshimiwa Waziri, deni letu la taifa limefikia dola bilioni 26 ambayo ni sawa na asilimia 32 ya ustahimilivu wa deni la taifa. Ukomo ni asilimia 56, sasa kama 26 imetupeleka kwenye 32 unahitaji dola bilioni 45 kufikia ukomo wa asilimia 56 ambayo ni mwisho wa kukopesheka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa twende tuchukue mfano wa miradi mitatu, acha miradi mingine yote kwamba hatukukopa, hatukukopa maji ambayo tunachukua hela za wahindi, hatukukopa kwenye barabara, elimu na wala kwenye umeme na maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu chukua miradi mitatu; mradi wa kwanza ni mradi wa ujenzi wa reli ya kati ambao kwa tathmini yake unaweza ukagharimu *approximately* dola bilioni 15, ziweke dola bilioni 15, chukua mradi wa *Stiegler's Gorge* wa uzalishaji wa umeme ambao kama ninavyosema leo ukikohoa wawekezaji wanakuja, tunataka kuweka hela za Serikali, dola bilioni tano, jumla 15 na tano unapata dola bilioni 20. Halafu chukua uboreshaji wa Shirika la Ndege, kwa ujumla wake mpaka umalize karibu dola bilioni moja kwa hiyo unazungumzia dola bilioni 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama una dola bilioni 26 deni la taifa ukijumlisha dola bilioni 21 maana yake unazungumzia dola bilioni 47 na ukomo wetu ni dola bilioni 45, kwa vyoyote vile hii ime-*burst*. (*Makofi*)

Sasa kama inakwenda ku-*burst* maana yake tunakwenda kutokopesheka, kama tusipokopesheka ina maana gani kwa uchumi wetu? Kwa nini tunataka kung'ang'aniza kuchukua hela ya Serikali na tumeanza kwenye reli na ndege tumeweka na kwenye *Stiegler's* na kwenyewe tunakwenda, mwisho wake uitakuwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hebu tufikirie upya, hii *thinking* ya kwamba sekta binafsi tunaiandika kwenye makaratasi kwamba ndio itakayotekeleza mpango huu, lakini kimsingi kwa matendo yetu tumeiweka pambeni, kwa nini tusiitumie? Awamu ya Pili ya Mzee Mwinyi walanza kuiruhusu sekta binafsi na akatengeneza mazingira, inawezekana kuna mapungufu yake lakini sekta binafsi ilianza kupata mwanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Nne Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Rais wa sasa Magufuli alikuwa Waziri wa Ujenzi. Wakati wake waliruhusu wakandarasi kutoka sekta binafsi wakachukua mikopo ya benki, wakaanzisha makampuni, leo hii tunavyoongea hawa watu *mortgagezao* zinauzwa. Na zinauzwa kwa kuwa wana madeni wanaidai Serikali, lakini Serikali imeamua kuanza kuchukua mkondo wa shughuli zake za ujenzi kutekelezwa na Serikali yenywewe. Kwa hiyo, hawa tuliowatengeneza kwa miaka yote tunawakosesha hela sasa, *they are starving and they are dying*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango wako mzuri ndio lakini hebu rudini kwenye *thinking* ya kuruhusu sekta binafsi kufanya kote, duniani kote mambo yanakwenda hivyo. Jana mmesikia mifano hapa na Mheshimiwa Spika alitoa mfano, Warusi ambao walikuwa waumini wakubwa wa ujamaa wameruhusu sekta binafsi mpaka viwanja vy

ndege; sisi leo kiwanja chetu cha ndege pale karibu dola bilioni 560 hivi, hela nydingi kweli. Hivi tungeruhusu watu binafsi wakawekeza nani asingekuja pale, kwa vyovoyote inalipa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi kama *Stiegler's gorge* pamoja na kwamba nauunga mkono, sina hakika kama tumefanya tathmini ya madhara yake ambayo yanatokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea kuuzunguka mradi wenyewe. Tuna miradi mingine ya maji hapa nchini ambayoo yote ina-*prove failure*; tumechukua tahadhari gani katika mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu wa kuamini kwamba Serikali itafanya kazi ya kuzalisha umeme wenyewe, ndio utaratibu unaotesa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Tumevunja Mkataba wa *Symbion* tunasema tutawekeza mitambo wenyewe pale, leo Lindi na Mtwara tunakaa mpaka siku tatu au nne umeme hakuna, maisha yanasisimama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kama hali hiyo ingekuwa inatokea Dar es Salaam kwamba mnakaa siku tatu/nne umeme hakuna Serikali mngevumilia? Hawa watu wanavumilia hali mbaya lakini kwa sababu gani, tunataka kuwekeza wenyewe kwa kutumia pesa za Serikali kwenye suala la kuzalisha umeme. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali ibaki kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji badala ya sisi wenyewe kwenda, tunatumia hela hii kidogo kwa uchumi huu mchanga tunataka tuwekeze kwenye miradi mikubwa. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mahesabu ya kawaida kabisa Mheshimiwa Waziri, mipango hii inakwenda kuua uchumi wa nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilitegemea hebu tufikirie upya pesa kidogo tuliyonayo twendeni tukaboreshe maslahi ya wafanyakazi, twendeni tukawekeze kwenye maji, afya na maeneo mengine ya huduma badala

ya kuichukua na kupeleka kwenda kuwekeza kwenye miradi ambayo inaweza ikajiendesha kibashara. Kila siku sisi tunapeleka sura mbaya, tunaanza kuonekana kama vile hatutaki sekta binafsi ifanye kazi katika nchi yetu. Utaratibu huu mbaya utaua uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Nape. Mheshimiwa Turkey ajiandae Mheshimiwa Mgimwa.

MHE. SALIM HASSAN TURKY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nashukuru kupata fursa leo ya kuweza kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya, sote tu wazima na tupo katika Bunge hili tukijenga Taifa letu. Pia nachukua fursa hili kumpongeza Rais wetu kwa kufanya maamuzi magumu ya kuongoza Taifa hili na kwa kweli anastahili kila sifa kwa nia yake njema ya kutaka kuifanyia Tanzania ya leo iwe ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nataka niingie kwenye Mpango. Huu Mpango ni mzuri sana lakini kwa kweli *heading* yake ina matatizo tena ina matatizo makubwa sana. na matatizo yake Mpango unasema ni maendeleo ya Taifa lakini nikitazama tafsiri ya taifa siikuti Taifa bila ya Zanzibar. Katika mpango huu hakuna sehemu hata moja iliyotaja Wazanzibar na kwa kweli Mpango huu kwa njia moja au nyingine umetudhalilisha Wazanzibar kama vile hatustahili kupangiwa chochote katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kama ni kosa basi nafikiri lirekebishwe kwa kuandikwa kwamba Mpango wa Maendeleo wa Tanzania Bara au uandikwe Mpango wa Taifa basi na Taifa la Zanzibar liwekwe katika Mpango huu lakini zero hakuna chochote. Hakuna mahali ilipoandikwa Pembä, Unguja wala Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili sijui kama limefanywa kwa makusudi na kama limefanywa kwa

makusudi basi naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha awatazame sana watendaji wake kwa sababu yeye ni msimamizi wa sera pengine hakuwa na *timenzuri* ya kusoma, lakini kwa kweli hili limetuangusha sana Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba kuna watendaji wa Serikali ambao kwa kweli hawaitendei haki Zanzibar na hasa katika mambo ya kufanya biashara baina ya Zanzibar na Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati zilizopita tulipata bahati ya kutembelea mipaka yetu, tulikwenda mpaka wa Sirari tukaona wafanyabiashara wadogo sana kila mfanyabiashara ana baiskeli ya *rally* nzuri madhubuti, lakini kazi yake yeye akiamka asubuhi anasukuma baiskeli kupita *boarderanakwenda* zake Kenya anachukua dumu la mafuta analeta, akimaliza kinachotakiwa Kenya anakichukua kwa baiskeli anaenda zake anapeleka na hakuna anayemuuliza kwa sababu ni mwananchi anayeishi maeneo yale, kwa hivyo, biashara hiyo inafanyika kwa baiskeli lakini unaweza kukuta ikifika jioni basi *canter* zima mtu kapenyeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi upande wa Zanzibar, leo miaka saba mimi nipo katika Bunge hili, kuna jambo moja dogo sana ambalo linatudumaza sisi Wazanzibar nalo ni lile la *longroom* pale Dar es Salaam. Wafanyabiashara wanaokuja sasa hivi kama mnavyojua Zanzibar inasifiwa kitalii, tuna utalii wa nje na wa ndani. Hawa watalii wa nje wakija kutembea Zanzibar mtu akinunua chochote Zanzibar akifika *longroom* pale akionesha risiti anaambiwa hapana tuoneshe na *document* ya *importation* ya kitu hiki, hivi kweli tunatendewa haki jamani Wazanzibari na Waziri wa Fedha upo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninaomba sana lishughulikiwe kama wewe kweli ni muumini wa haki basi hili naomba ulisimamie Wazanzibar wasinyanyaswe pale. Mtu akija na *tv* moja ni biashara ni sawa sawa na mtu ambaye amenunua Morogoro akaja Dar es Salaam. Sasa leo ninashangaa leo watu wakienda wakinunua kitu kidogo

Zanzibar akipita pale inakuwa kesi kubwa sana. Kwa hivyo, hilo ninaomba safari hii angalau tuhakikishe adha hii hii ndogo basi lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha hilo, tunazungumzia uhusiano wa mapato baina ya wananchi kulipa mapato na Serikali kupokea mapato. Lakini *TRA* ilipoanzishwa kulikuwa na kauli mbiu inatumika kwamba sisi ni *partners* katika maendeleo ya nchi yetu, sasa hivi tafsiri hiyo inaondoka. *TRA* sasa hivi wamekuwa ni watu wa bunduki, watu wa kutumia nguvu, wanaingia kila mfanyakishara anatafirika. Wewe mwenyewe ulitoa tafsiri katika mwaka uliopita ulisema maduka 4,000 yamefungwa, hiyo ni kwa sababu ya ukali wa *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo yanazungumzika, Serikali hii ilipoingia madarakani, Serikali iliyopita ililengeza mambo mengi sana, ninyi mmeingia mmekaza, mna haki ya kufanya hivyo, hakuna tatizo. Lakini kwa nini mnawaadhibu hawa kwa awamu iliyopita na awamu hiyo wewe Waziri, Rais wetu, sote tulishiriki, tulikuwemo katika Serikali iliyopita. Na sote kama kuna makosa yalitokea basi sisi pia ni wakosa wa Serikali iliyopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali hii ilishaamua kwamba twende vingine, basi tukubaliane kwamba twende kwa mwendo tunaotakiwa. Sasa tusiambiwe kwa makosa ya Serikali iliyopita, Serikali hii naiheshimu sana na tunataka tufanye kazi kwa pamoja na tuitekelezee kila wanachokitaka, tutakaza miguu tutafuata. Sisi *private sector* tunaamini kabisa mpango wa Rais wetu Dkt. Magufuli wa kutaka kuendeleza viwanda ni mzuri sana na utafuzu kwa nguvu zote, na yeye ana nia njema kabisa, lakini watendaji wetu wanatuangusha. Naomba Mheshimiwa Waziri hili ulisimamie kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nalo ni muhimu, wakati wa awamu zote zilizopita, biashara baina ya Bara na Visiwani, sisi Visiwani tunaitegemea Bara kwa asilimia 90 kwa maisha yetu ya kila siku Zanzibar. Unacho sema wewe sisi tunanunua Bara ndiyo tunapeleka Zanzibar. Lakini

awamu zote zilizopita kulikuwa na ulegevu fulani pale bandarini Wazanzibari waweze kuleta bidhaa zao ziuzike, sasa hivi awamu hii imetu-*tag*sisi Wazanzibari ni wezi, hatutaki kufanya wa biashara, biashara yetu ni kuiba tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutoptana na fursa ambazo tulikuwa tukipewa na awamu zilizopita, naiomba awamu hii kwa sababu wamekaza kamba sasa wakubaliane na hii hoja ambayo naiomba kwako wewe Waziri kwa kuitia Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mazingira ya kufanya biashara Zanzibar na Bara ni mawili tofauti kabisa katika *East Africa* nzima. Sisi leo kama tutaagiza mzigo kutoka nje, tukauleta Zanzibar, basi tutalipa kodi pale, tutaushusha mzigo Zanzibar, utaenda zake *godown*, atakuja mteja ataununua mzigo ule utapakiwa tena kutoka *godown* utakuja bandarini utapakiwa katika vyombo utakuja Bara, utapakuliwa, utakaguliwa, halafu upakuliwe tena ndiyo ufike sokoni, angalia safari zako hizi zote zilizopita, ni gharama mno kwa kufanya biashara Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar kama tunavyojua, miaka yote nenda rudi ndicho kituo cha kufanya biashara na sisi sote nguvu zetu tuko katika kuendeleza Zanzibar iwe kituo cha biashara. Na hili nataka niombe sana Serikali yetu, tusione kwamba Wazanzibari ni wakorofi, tuone ni ndugu zetu ambao tunataka tushikamane nao, leo uchumi wa Zanzibar ukikua ndiyo uchumi wa Bara unakua. Haiwezekani uchumi wa Zanzibar ukawa mzuri wa Bara ukawa chini. Bado *BOT* ndiyo *regulator*wetu, haiwezekani uchumi ukawa wa upande mmoja na wa upande mwingine usiwe, uchumi wetu utakuwa chini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kutoptana na hilo, naomba sana hizi tozo za *TRA* kwa maana ya *duty, sales tax* na nini zilizoko katika Muungano wetu, kwa Zanzibar tufikiriwe angalau tushushiwe. Kwa Zanzibar, kama Dar es Salaam ni *25 percent*, basi Zanzibar iwe *25 percent* lakini *database* ile ile ikubalike. Mtu akishalipa kodi pale basi sawa iwe mzigo

ule kutoka Zanzibar kuja Bara iwe ni rahisi wala hakuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi tunavyofanyiana ni sawasawa na mfanyakishara mkubwa kumuua mdogo. Uchumi wa Zanzibar huwezi ukaulinganisha na uchumi wa Bara. Kwa maana hiyo, mtazame kwamba katika kutekeleza ni kwamba lazima kila mtu alipe kodi kwa uhakika wake na uhalali wake. Basi sasa tuangalie kodi zetu nazo ziwe rafiki kwa pande zote mbili. Hiyo inakuwa ni *double taxation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba sana Wizara ya Fedha ilitazame ni kwamba awamu iliyopita ukienda *TRA* kodi watu walikuwa wakilipa basi mara nyingi sana ni ile kodi ya chini kabisa mtu ndiyo bei anayotiliwa analipa, ukiingia sokoni bidhaa zinauzika, au analipa kodi bei ambayo hata katika *database* halipo, lakini inapitishwa watu wanalipa.

Awamu hii *Ma Sha Allah* imekuja vizuri sana mna-*collect* kodi vizuri sana, lakini kilichotokea, watu badala ya kutazama *database* bei za chini au za kati, wamekwenda kuzivamia za juu kabisa. Kilichotokea ni mfumuko wa bei kwa Tanzania nzima, vitu vyetu sisi vimeduwa ghali. Na kama unajua soko la Kariakoo ndiyo *centre* ya kulisha; Burundi, Rwanda na Kongo wote wanunua Kariakoo, bidhaa nyingi sana pale. Na ninaamini karibu asilimia 30 mpaka 40 ya kodi inatokana na Kariakoo. Lakini leo maduka yale yote yamekufa kwa sababu ya kodi kutozwa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Seriikali yangu ni kwamba hizi tozo tusitafute hiyo njia ya panya isiwepo, lakini hizi kodi angalau zitazame pale *database* bei ya chini. Kitakachofanya sasa hivi biashara hizi zinakuwa tena kwa nguvu sana, lakini sio Tanzania, watu wanakwenda kununua Kenya, soko hili la Rwanda, Burundi, Kongo, sasa hivi mambo yote watu wanakwenda kununua Mombasa, Nairobi, ndipo inapofanyika biashara hii. Tulioumia ni sisi Watanzania, biashara imeanguka kwetu, kwa hiyo hili nalo litazamwe. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Mgimwa ajiandae Mheshimiwa Anthony Komu kwa dakika saba na nusu.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa afya nipate nafasi ya kuchangia kwenye ajenda hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na Naibu Waziri na wasaidizi wao kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara yao. Lakini namshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Mpango, amesema kwenye maandiko yake kwamba atatuzingatia na kuufanya kazi ushauri wetu. Nakuomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, haya tunayozungumza kama Wabunge wenzako uyachukue na kuyafanya kazi kama ulivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unaanza kujielekeza kwenye hali ya kiuchumi. Mheshimiwa Dkt. Mpango amesema uchumi wa Tanzania unakua, ni kweli kwa maelezo yake uchumi wa Tanzania unakua. Lakini unapotaka kuangalia vigezo vya kukua kwa uchumi, lazima tuangalie na hali halisi ya Mtanzania, je, iko sawa, inaenda sambamba na ukuaji wa uchumi anaouzungumza Mheshimiwa Dkt. Mpango? Ukiangalia utaona mambo yako tofauti, tunazungumza uchumi unakua, lakini hali za Watanzania zinaendelea kuwa mbaya siku baada ya siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwa hiyo inawezekana vigezo ulivovitumia kusema uchumi wa Tanzania unakuwa ni tofauti na vile ambavyo tunavifikiria sisi. Kwa mfano, kupata hela ni tatizo, lakini leo hii ukipata pesa unaweza ukashindwa hata kujua umetumia kununua nini, *purchasing power* inazidi kushuka siku baada ya siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie, tuko kwenye *inflation period* au *deflation period*. Kwenye *deflation period* kama upatikanaji wa pesa unakuwa mgumu, *automatically* unawasaidia wale waliokuwa na pesa kidogo kuweza kununua vitu vingi katika *circulation*, lakini mtu anakuwa na hela ndogo aliyopata, uki-*change shilingi* 10,000 hata hujui imefanya nini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango mimi nakuomba uliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tujiangalie, tupo kwenye *depression* au tuko kwenye *recession period*. Hayo mambo yote mawili tunatakiwa tuyaangalie kwa wakati mmoja...

MWENYEKITI: Anaitwa Dkt. Mpango, siyo Dkt. Mpango.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Dkt. Mpango, tupo kwenye *depression* au tuko kwenye *recession period*, mimi naona kama tunakwenda kwenye *depression*, tunatoka kwenye *recession* kwenda kwenye *depression*. Kwa hiyo ninamuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango aliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi kwenye suala la *bureau de change*, lakini bado tuna tatizo kwenye *dollarization*, bado matumizi ya *dollarization* yanaendelea kutawala katika nchi hii na shilingi ya Tanzania inaendelea kushuka siku baada ya siku. Sasa unatuambia uchumi unapanda, shilingi inashuka, uki-*compare* unaona hapa kuna tatizo. Kwa hiyo, vigezo ambavyo Mheshimiwa Dkt. Mpango amevizungumza tunaona haviendani na hali halisi ambayo iko mtaani. Kwa hiyo namuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango aangalie na haya mambo ambayo yanawahusu Watanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika *document* yake hii ya Mpango mzima hawajazungumzia hali halisi ya wakulima ambao nchi hii asilimia 67 mpaka 72 ni ya wakulima. Kwa hiyo, unakuta mpango mzima wa maendeleo wa nchi

hii umewaweka kando wakulima na hawa wakulima ndiyo wanaotuweka hapa madarakani. Kwa hiyo, ninaona hapa kwenye eneo la kilimo kwa ujumla kuna tatizo. Kwa hiyo namuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango aliangalie na hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuliahidi kwamba tutatengeneza Kiwanda cha Mbolea hapa nchini kule Mtwara lakini mpaka leo kiwanda hicho hakijatengenezwa. Kingeweza kutengenezwa kiwanda kile cha mbolea kule Mtwara nina uhakika mbolea ingekuwa chini kuliko ilivyo sasa hivi. Tulikuwa tumekwenda kwenye mpango wa *bulk procurement*, bei imeshuka kidogo, lakini tungekuwa tumetengeneza kiwanda chetu hapa nchini bei ingekuwa chini zaidi na nina uhakika kwamba haya ambayo wakulima na Wabunge wengi tunalalamikia yasingekuwa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tunajuliza, kwa nini wenzetu wa Zambia wanauzu gunia la mahindi shilingi 20,000 kwa nini sisi tunauza shilingi 35,000? Kwa hiyo tuna maana kwamba mbolea kule iko *cheap* zaidi kuliko kwetu, lakini sisi tuna *access* ya kutengeneza mbolea hapa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata ule uchumi wa viwanda ambao ndugu yangu, Mheshimiwa Jafo, anauzungumzia sana, tunaomba uliangalie eneo hili *sensitive* la wakulima kwamba kile kiwanda cha mbolea tulichokizungumzia ambayo *raw material/tunayo* ya kutosha kule Mtwara kingeanza *as soon as possible* tuwasaidie wakulima walio wengi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi namuomba sana Waziri wa Fedha atakapokuja atuambie kile kiwanda ambacho tumekivumilia miaka mingi kwa nini mpaka leo hakijaanzishwa na sababu zippi zinazopelekea kutokuanzishwa kwake. Sasa matokeo yake ni kwamba kila siku tunakuja na miradi mipyä ambayo haina tija. Unaanza mradi wa zamani *to a level* fulani unafika unauacha unakuja kwenye mradi mipyä. Kwa hiyo hapa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la mahindi, na mimi nataka *declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Kwenye kilimo tumelizungumzia na bahati nzuri leo Mheshimiwa Waziri amelizungumza na baadhi ya Wabunge wanaotoka kwenye maeneo hayo. Kamati yetu tulikaa na Mheshimiwa Waziri siku tatu kuzungumzia tatizo la mahindi, tumbaku na mbaazi na tukatoa *directive* kwamba Mheshimiwa Waziri aje hapa kwenye Bunge lako Tukufu aeleze mkakati wa Serikali kuhusu mahindi yatauzwaje, mbaazi itauzwaje na tumbaku itauzwaje, lakini amekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi Wajumbe wa Kamati tulikuwa tunategemea yale ambayo yanaulizwa na Waheshimiwa Wabunge yangekuwa yameshazungumzwa hapa Bungeni kabla na Wabunge wakatoa maazimio ya pamoja. Kwa hiyo, wakulima wetu wanakwenda mwezi wa 11 wanaanza kupanda mahindi, hawajui nini wafanye hata kama tumekubaliana leo kwamba tunataka kufungua masoko, bado ni tatizo. Aje hapa kwenye Bunge lako Tukufu atoe tamko la Serikali kwamba kuanzia leo watu wauze mahindi yao popote wanapotaka ili waweze kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme, kama nilivyosema hapo awali, kila siku Serikali ina mawazo mapya. Tulikuwa tunategemea tutatengeneza umeme kwa kutumia makaa ya mawe, wenzetu wa Mchuchuma, Ngaka, Kiwira. Lakini mpango huu upo zaidi ya miaka 30, sasa tukijuliza kwa nini tunaenda kwenye mipango mingine wakati mpango huu ambao ulikuwa umeshaanza tumeuacha. Kwa hiyo unakuta hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakisema kuna baadhi ya miradi imekuwa *biased*, watu wanaamua kwenda kwenye miradi mingine wanaacha miradi mingine, hili litatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini wameamua kuacha mradi wa umeme. *Sweden* kuputia Kampuni yao *SIDA Grand* walikubali kutoa hela, dola milioni 60, kwa ajili ya kusaidia kutengeneza

transmission line ya kutoka Makambako mpaka Ngaka, lakini Serikali imekaa kimya. Na tatizo la pale ni *transmission line* tu na umeme ule ni *cheaper* kuliko umeme mwingine wowote. Kwa hiyo, tunataka kwenda kwenye vyanzo vingine vya umeme wakati tulikuwa tunaweza kupata umeme wa rahisi ambaao Serikali ilikuwa haiingizi hela yoyote kama alivyosema Mheshimiwa Nape pale, kwa nini twende kuingiza hela kwenye miradi ambayo haina tija katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba tuangalie na mje na majibu kwa nini mradi wa umeme wa Ngaka mpaka sasa hivi haujaanza kazi. Kwa nini mradi wa uchimbaji wa chuma mpaka sasa hivi haujaanza kazi kule Liganga. Hii inakatisha tamaa sana, tunaona kwamba kuna baadhi ya maeneo wanapewa *priorityya* hali ya juu na kuna baadhi ya maeneo hawapewi kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye maeneo ya barabara, tunatakiwa tuendelee kufungua barabara. Kuna barabara ya kutoka Kinyanambo A kwenda Isalavanu, Madibira mpaka Rujewa, ni barabara imezungumzwa karibu katika awamu tano. Toka mwaka 2000 ile barabara inazungumzwa, na ni barabara muhimu sana kiuchumi. Kwa watu wanaotoka Mbeya wakiamua kukatisha kwenye barabara ile wanapunguza zaidi ya kilometra 75 kuliko wakipita barabara ile ya kupitia Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye uchumi hili ni jambo zuri sana. Lakini kila siku wanasema tutaanza kesho au kesho kutwa, lakini ukianglia katika mpango wake na ile barabara *is very sensitive*, inapitia kwenye mbuga za wanyama, inapitia kwenye maeneo ya kilimo kikubwa cha mpunga, inapitia kwenye kilimo kikubwa cha mahindi, inapitia kwenye maeneo ya madini, wameiacha haijaanza kushughulikiwa. Kwa hiyo kuna walakini hapa.

La pili, unakuta barabara ya kutoka Mafinga kwenda Mtiri mpaka Mgololo. Barabara ile ina zaidi ya viwanda vikubwa kumi ambavyo vinatoa kodi zaidi ya shilingi bilioni 50 lakini Serikali haitaki kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa

hiyo, hili ni tatizo; watu ambao wanachangia hela nydingi kwenye nchi hii wanasa haulika. Kwa hiyo, mimi namuomba sana Mheshimiwa Waziri mipango yake awe anaangalia na watu wana-*contribute* nini katika Taifa hili, sio ajielekeze kwenye maeneo tu ambayo anayaona yeye. Watu wanachangia hela nydingi kwenye Mpango wa Taifa lakini matokeo yake ni kwamba hatupeleki kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanikiwa kwenye eneo la umeme lakini bado kwenye eneo la maji. Mheshimiwa Waziri amezungumzia eneo la maji Dar es Salaam tu, ina maana watu wa Tanzania wengi wanakaa Dar es Salaam. Katika Mpango wake mzima ameonesha kwamba maji yanatakiwa yaende kwa wingi katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwa nini kwenye Mikoa, Wilaya, Vijiji na Majimbo mengine yasiende? Kwa hiyo kama tulivyofanya kwenye maazimio ya Bunge lilllopita kwamba tuli-*ringfence* kwa ajili ya kupata umeme wa uhakika, sasa hivi nguvu zetu zielekezwa kwenye eneo la maji ili maji yapatikane katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Kamati yetu tumependeleza hata Bunge lilllopita tuongeze shilingi 50 kwenye kila lita ya mafuta ili maji yaende kwenye maeneo yaliyokuwa mengi, lakini tukikwambia utasema kwamba tutaongeza *inflation rate*, hatuwezi kuongeza *inflation rate* kwa utaratibu huo. Kwa sababu sisi kama Wabunge tumekubali na tutakuwa tayari kwenda kutetea hoja zetu, kwamba tuna sababu za msingi za kuongeza shilingi 50 kwenye maji ili maji yaende kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Antony Komu kwa dakika saba na nusu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia huu Mpango ambalo ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa sehemu ile kwenye hotuba ya Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, ambapo anazungumza kwenye ukurasa wa tano juu ya kuweka nguvu kwenye maeneo ambayo yanawahu su watu walio wengi. Anasema tuweke nguvu kwenye maeneo hayo ambayo ni kilimo, uvuvi, pembejeo na mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachojiliza na ambacho mimi naona kwamba ni shida kubwa sana katika huu Mpango ni uhalisia wa hilo tamko ambalo ameliweka hapa na mambo ambayo yanafanyika. Kwa sababu tunapaswa tuijiliza tukienda kwenye kilimo tuna mikakati gani ambayo inashikika ya kufanya mapinduzi ya kilimo, uhalisia hauko hivyo. Na kama hatutarekebisha hali hii kwa kweli tutaedelea kubaki watu wa kusema maneno tu na hakuna kitu ambacho kitakuwa kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mabonde makubwa, tuna mabonde tisa ambayo ni Rufiji, Kihansi, Pwani na kadhalika. Lakini ukijiuliza kuna mipango gani ya makusudi ya Serikali ambayo inafanya haya mabonde yaweze kuleta mapinduzi ya kilimo, ukweli ni hakuna. Na nimeangalia kwenye ukurasa wa 19 wa hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango anasema katika utekelezaji wa bajeti iliyopita wameweza kutenga vyanzo vya maji 78 na kutangaza kwamba haya ni maeneo tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni utani, kwa sababu kwa taarifa ambayo sisi tulipata kwenye Kamati yetu ya Mazingira, Bonde la Kihansi peke yake lina vyanzo 901, katika vyanzo hivyo ni asilimia 27 tu ambayo imeshatambuliwa, kuwekewa mipaka na kutangazwa kama ni maeneo ambayo ni tengefu. Maana yake kuna maeneo zaidi ya 600 hayajafanyiwa chochote na maana yake ni kwamba hayawazi kutumika vizuri kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya kilimo. Kwa hiyo, katika hali kama hii unaweza ukasema kwamba hatuko *serious* na hatumaanishi haya ambayo tunayasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati yetu vilevile ya mazingira tulianzisha hapa Mfuko wa Mazingira na ukazinduliwa na Mheshimiwa Rais na wako watu wa muhimu nawenye uwezo mkubwa sana kwenye ule Mfuko wa Mazingira. Lakini mfuko huu ilitengewa shilimhi bilioni mbili mpaka leo tunavyozungumza, Serikali imetoa shilingi milioni 34 tu kwa ajili ya huo Mfuko wa Mazingira, sasa katika hali kama hiyo tunapigaje hatua. Ukienda kuangalia kwenye eneo hilo la kilimo tuna Benki inaitwa ya Kilimo hapa, hiyo Banki ya Kilimo inafanya nini, Serikali imeipa nguvu kiasi gani ili iweze kufanya mapinduzi ya kilimo katika nchi hii, nimeangalia wametoa mikopo ya kama shilingi bilioni 6.5 kwa watu 2000 na kitu maana yake ni wastani wa kama shilingi milioni 2.6 kwa mtu mmoja. Tunaweza tukafanya mapinduzi ya kilimo katika nchi hii kwa stahili ya namna hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Moshi kulikuwepo na mradi unaitwa *Moshi Lower Irrigation Scheme* ambao huu uligharamiwa na Wajapani, baada ya Wajapani kuondoka ekari ambazo zilikuwa zimekwishatayarishwa na kujengewa miundombinu zilikuwa 1,100 na zilikuwa na uwezo wa kuhudumia watu zaidi ya 4,500 leo hii tunapozungumza kutokana na uchakavu, kutokana na mabadiliko ya tabianchi leo ni ekari 417 tu ambazo zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wazi kwamba tunarudi nyuma hatupigi hatua na kama Serikali haitachukua hatua za makusudi za kuwekeza kwenye maeneo kama haya na kuangalia maeneo ya miradi ya namna hiyo katika nchi nzima tutaendelea kuwa maskini na hatuwezi kufanya hatua yoyote. Tukienda kwenye uchumi wa viwanda, ni lazima tukubaliane na watu wengi hapa wamezungumza kwamba tunataka kujenga uchumi wa aina gani, uchumi wa kijamaa au wa kibepari au wa kati, kwa sababu ukiangalia tunazungumza kuwa tunataka kujenga uchumi wa viwanda lakini unaona kwamba Serikali bado inarudi kule ambapo tulishatoka miaka mingi. Leo hii Serikali inamiliki *TTCL* kwa 100%, leo hii Serikali inamiliki kiwanda cha *General Tyre* kwa 100%, leo hii *TBA* inafanya kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi wajibu ule wa Serikali ambao tunauzungumza wa kujenga mazingira wenzeshi, unaendanaje na hali kama hii? Lakini tunazungumza uchumi wa viwanda tumetenga maaneo kwa miaka mingi EPZ na ZSS, na baada ya kuyatenga hakuna hatua za makusudi na uwekezaji wa makusudi katika hayo maeneo kwa ajili ya kujenga miundombinu, kwa ajili ya kuyafanya yale mazingira yaweze kuwa wezeshi, kwa ajili ya kulipa fidia hakuna hatua ambazo za kulizisha. Matokeo yake ni kwamba tunatarajia wawekezaji waje, wajenge barabara, waweke umeme na waweze kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atuambie ni mtu exposed sana na sina matatizo naye, ni wapi hapa duniani hata kule China ambapo ardhi ilitengwa halafu...

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante dakika saba na nusu, Mheshimiwa Pascal Haonga kwa dakika saba na nusu.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi naomba niweze kuchangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote...

MWENYEKITI: Ajiandae Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi naomba niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa Ndugu yangu Tundu Lissu kwa yale ambayo yalimkuta na nitoe pole na niseme tu kwamba hata niliposikia jana kuna baadhi ya Wabunge wenzetu wachahé wanaanza kuleta vijembe kwenye suala kama hili kwa kweli liliniumiza sana. Lakini niseme tu kwamba siku zote matatizo hayana itikadi na matatizo yanaweza kumkuta mtu ye yote yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie kwenye Mapendeleko ya Mpango, tunafahamu wote kwamba kwenye hili kablasha tuliopewa na ndugu hapa Dkt. Mpango ukweli ni kwamba amezungumza vitu vingi sana kuhusu viwanda, kilimo na mambo mengine, lakini hatuwezi kupata viwanda bila kujali kilimo. Wenzangu wamezungumza mengi sana na jana niwapongeze waliotangulia kuzungumza kuhusu kilimo, lakini ukweli unapozungumza habari ya viwanda huwezi kuacha kilimo na ukakiweka pembedni, historia inaonesha nchi zote ambazo leo zina viwanda, nchi kama China na nchi nyininge nydingi ambazo leo zimeendelea ni kwa sababu walifanya mapinduzi katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania tunafahamu kwamba tunapotaka kufika mwaka 2020/2025 tunasema kwamba nataka Serikali hii iwe angalau wananchi wake wale na uchumi wa kati, uchumi ambao utaendeshwa kwa kutegemea viwanda. Lakini ukweli je, ni kwa sasa? Kwa sababu kwa muda huu ukiangalia kama lengo ni kupata malighafi kwa mfano kwenye viwanda vyetu ni kweli lazima tuangalie kilimo, lakini kwa sasa hali ilivyo wananchi wetu wamezalisha sana na wanalia kila kona hawana masoko ya mazao yao na viwanda vyaya kuweza kuwa-*accommodate* hayo mazao, kuweza kusindika mazao hayo hazipo. Kwenye hili tumebugi sana na hili niweze kusema kwamba tumerudi nyuma na wanachi wetu wanateseka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakulima wote waliolima tumbaku wanalia, wanalia wote waliolima mahindi na hivi ninavyozungumza Kanda za Nyanda za Juu Kusini katika Mkoa wa Songwe, Mkoa Mbeya, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Ruvuma na mikoa mingine wanalia sana, mahindi yamekaa ndani, hakuna ayenunua yale mahindi, hivyo viwanda mlivyosemakwamba tupate malighafi kwa ajili ya kusindika mazao yetu tuonyesheni basi viwanda hivyo wakulima wetu wakauze mazao hayo kwenye hivyo viwanda basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya kwelikweli amezungumza vizuri ndugu yangu jana mmoja, leo mkulima

anayelima ananunua mbolea bei kubwa, anakodi shamba bei kubwa, ananunua mbegu bei kubwa, lakini mwisho wa siku tunakuja kumfungia mipaka eti asiuze mahindi nje ya nchi lakini pa kuuza wakati huo Serikali haitoonyeshi tukauze wapi. Dhambi hii ambayo inatendwa na Serikali yetu na viongozi wa Chama cha Mapinduzi lazima niwe muwazi hapa jambo hili kama hamuwezi mkajadili kwenye *caucus* zenu mnajadili mambo mengine wananchi wetu msimu wa kulima ndio huu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni baya sana na mwaka 2019/2020 hili jambo litawaghali mu na mjiandae kuondoka, kwaheri Chama cha Mapinduzi kwa sababu suala hili wameshindwa kujadili mambo ya msingi, wanajadili mambo mengine wanaacha suala hili la wakulima wetu. Mimi niseme kwamba leo tunazungumza 60% ya chakula kinachozalishwa nchini kinatoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, mkulima huyo hawezi kununua mbolea bila kuuza mahindi, hawezi kusomesha watoto bila kuuza mahindi, hawezi kufanya jambo lolote lile bila kuuza mahindi, leo wakulima hawa wanalamika mimi naamini hasira hizi na machozi haya mwaka 2019/2020 wajiandae hao waliosababisha na Serikali hii na Chama cha Mapinduzi wala sio Serikali ya CHADEMA, wala sio ya CUF. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua wako wakulima pia wa tumbaku wanalamika, wako wakulima wa mbaazi wanalamika, wakulima wa korosho wenye wanasema bei imekuwa nzuri, lakini kiukweli bado hata wa korosho hao pia wamekopwa, bado hawajalipwa. Kiukweli kabisa tusipokuwa makini kwenye suala la kilimo mimi naamni kabisa Watanzania wengi watarudi nyuma kwasababu kilimo ndo kinaajiri 70% na kuendelea ya Watanzania walio wengi.

Naomba nzungumzie jambo lingine linalohusu utawala bora. Leo tumezungumza kuhusu utawala bora lakini ukweli ni kwamba viongozi wengi wanaotuhumiwa na rushwa kama ma-*DC* leo wanapandishwa vyeo wanakuwa Wakuu wa Mikoa. Hivi unawezaje kumpandisha cheo mtu ambaye alikuwa *DC* unampa Ukuu wa Mkoa anathumiwa kwa rushwa

na ushahidi upo, TAKUKURU wameenda wamnachunguza kila kitu, kila mtu ameona kabla TAKUKURU hawatoa majibu leo Rais anaenda kumpa DC kuwa Mkuu wa Mkoa anayetuhumiwa kwa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hakuna utawala bora na hapa hali ni mbaya kweli kweli kama tutakuwa tuna-*promote* wanaoharibu nchi yetu, kwa kweli najua kabisa kwamba utawala bora, dhana ya utawala bora tuiondoe kabisa kwenye awamu hii ya tano. Lakini leo tunafahamu wote wanapozungumzia utawala bora tunafahamu misingi ya utawala bora ni pamoja na uwazi, leo Ndugu yangu Mpango hapo tumeambiwa Serkali imeokota vichwa nya treni pale Dar es Salaam bandarini, hivi ni kweli Serikali haijui ni kwamba vile vichwa nya treni vimetoka wapi. Uwazi uko wapi kwenye utawala bora lazima kuna uwazi, uwazi uko wapi, halafu vile vichwa nya treni vinajullikana vimeandikwa kabisa na majina. Sasa haya mambo leo Serikali inataka kununua vile vichwa nya treni, inanunua kutoka kwa nani inafanya biashara na nani, ni suala ambalo lazima tujue kabisa kwamba utawala bora ni tatizo ni janga kubwa nana na Dkt. Mpango ulichokizungumza kwenye ile kablasha kuhusu utawala bora, umezungumza tu kidogo tu mahakama sijui kujenga kufanya nini vitu vingi sana nya msingi ilitakiwa tuwaeleze Watanzania vinakaa vipi. Kwa hiyo kiukweli kwenye hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante dakika saba na nusu zimekwisha. Mheshimiwa Mbarouk jiandae, ukimaliza wewe ataingia Mheshimiwa Jaku.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika Bunge letu hili tukajadili mambo ya nchi yetu na hususani Mpango

huu wa Maenedeleo wa 2018/2019. Baada ya hapo vilevile pia bado niendelee kushukuru chama changu kwa nafasi nilioipata. Lakini mimi nianze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Serikali yetu imekuwa na mipango sana. Lakini katika mipango hii mingi imekuwa haina tija, na nianze kwa kutoa mfano, tulikuwa na mpango wa MKUKUTA *One, Two and Three* lakini mpaka leo hatujui mpango ule umeashilia wapi. Umetajwa hapa asubuhi MKURABITA bado una matatizo, lakini pia palikuwa na *Big Result Now* hatuelewi imeishia wapi, lakini palikuwa na Kilimo Kwanza, watu wakakopeshwa matreka leo hii taarifa tulizozipata kwenye Kamati yetu imebidi baadhi ya matrekta yakamatwe kwamba watu wameshindwa kulipa.

Lakini pia palikuwa na mpango wa shillingi millioni 50 za vijana kila Wilaya hatujui umeashilia wapi, lakini vilevile palikuwa na mabilioni ya JK nayo haya tukiulizana sijui nani aliyepata. Lakini kama hilo halitoshi bado palikuwa na Mpango wa MMEM wa ujenzi wa shule za msingi na sekondari MMES, lakini bado palikuwa na mpango wa kujenga vituo vyaa afya kila kijiji nao hatujui umeashia wapi. Sasa napata taabu nkuona hii mipango tunayoipanga yote kwanini haina tija Watanzania wanatuelewa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri tu Serikali ni bora iwe na mpango mmoja ambao utakuwa unafuattiliwa na kufanyiwa tathimini kila baada ya mwaka mmoja na nusu kuona kwamba faida iliyopatikana kutokana na mpango huo ni ipi na kama hakuna faida basi mipango tuiache, lakini jambo lingine tumekuwa kukisema kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na 75% ya Watanzania wanaishi vijijini wamejajiri wenywewe kupitia kilimo, lakini tuijangalie kama Taifa ni kweli tunathamini kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu? Hailengii akilini kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Tifa letu lakini ni *theoretically* sio *practically*. Kwa hiyo, mimi niseme tu lazima kama kweli tumeamua kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa tujue vilevile kwamba kilimo ndio kitakachotoa *materi*/ya kwenda

katika Tanzania ya viwanda. Sasa kama kilimo chenyewe tumekipuuza leo tunajadili hapa masuala ya mahindi kukosa bei. Wananchi wameweza kufanya kazi kubwa sana bila ya kuwezeshwa na Serikali kwa mfano katika Mkoa ninaotoka mimi hatutumii pembejeo sisi tunalima kutoptaka na ardhi ambayo ipo na ina rutuba *by nature*. Lakini leo mahindi yamerundikana hayana bei wananchi wameshindwa kusomesha watoto wao, wananchi wanashindwa kuendeleza nyumba zao za kisasa. Serikali ndio inayozuia mahindi hasiuze nje ya nchi, sasa tujitazame tunafanana na nchi za wenzetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahindi yana soko kwamba yanahitajika *Southern Sudan*, mahindi yanahitajika Kenya, mahindi yanahitajika maeneo ya Ethiopia huko, lakini sisi bado tunazuia mahindi yasiuzwe. Mimi niishauri Serikali tuondoe kikwazo kwa uuzaji wa mahindi, kama Serikali wakala wake wa chakula ameshindwa kununua mahindi haya tuwaache wafanyabiashara wenye uwezo, wanunue mahindi wauze katika nchi za nje. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hilo halitoshi pia vilevile mazao kukosa bei mi naweza nikasema ni Serikali haikutaka kutafuta bei ya soko la mahindi. Kwa hiyo, lazima wananchi waache watafute soko wenyewe, haiingii akilini kwa sababu kwa mfano yupo mfanyakibashara mmoja wa mabasi anaitwa Sumry ameama kuaachana na biashara ya mabasi imeingia kwenye kilimo. Sasa hivi kweli anaweza akaamua kulima mahindi ya kula yeye mwenyewe binafsi, kwa ekari ya zaidi 10,000 au 15,000 alizokuwa nazo! Ni wazi anaamua kuingia kwenye kilimo afanye kilimo cha biashara, amevuna mahindi wanamwambia asiyauze, hapa hukumsaidia bali unamrudisha nyuma katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hilo halitoshi, ushauri wangu niseme pamoa na kuwaachia wananchi kutafuta masoko ya mahindi lakini basi tuwawezeshe kama tunaweka vikwazo hivi angalau tuwape mashine za kusaga unga sasa badala ya kupeleka mahindi ghafi, makapi ya mahindi yapaki kuwa vyakula vyaya mifugo kama ng'ombe

wa maziwa lakini wauze unga angalau tumekuwa tumewasidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laini lingine nije katika suala loa uvuvi bahari kuu. Mimi ninatoka Tanga, Tanga tuna bahari kuanzia Jasini karibu na Kenya mpakani huko mpaka Kipumbwi karibu na Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejaaliwa bahari kutoka Jasini mpaka Msimbati lakini ukiwatazama wavuvi wa ukanda wa Pwani ni maskini wa kutupwa hohehahe. Badala ya Serikali kuwasaidia imewarundikia kodi lukuki na ushuru mbalimbali, mimi niseme tu wavuvi tuwasaidie kwanza kwa kuwaondolea hizi ushuru na kodi mbalimbali, kwa mfano, mashua moja inachukua wavuvi 25 mpaka 30 lakini wavuvi hawa 30 kila mmoja anatakiwa awe na leseni ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kwenye basi anayekuwa na leseni dereva peke yake *turn boyhana* leseni wala kondakta hana leseni, kwa nini kwenye vyombo vya uvuvi isiwe mwenye leseni nahodha peke yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tuulizane Waheshimiwa Wabunge katika meli kubwa zinazokukuja kutoka nje kwa mfano ile meli iliyokamata na samaki waliyoitwa samaki wa Magufuli hivi wale watu wa mazingira waliwakamata wakawauliza mpaka mabaharia kwamba walikuwa na leseni ya uvuvi, kwa nini tunawaacha watu wa nje wanufaiki tunawakandamiza Watanzania wazalendo wenzetu wadhalilike na waendelee kuwa maskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri Serikali iondoe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKTI: Ahsante chama chako kina maelekezo wewe nusu na mwenzio nusu, namwita sasa Mheshimiwa Khatib Said.

MHE. KHATIB S. HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia name kusimama hapa mchana wa leo siku tukufu ya Ijumaa ili name niweze kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kuwapongza kwanza Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote walionekana na Mheshimiwa Rais wanafaa kuwa Mawaziri na wamepata uteuzi ule, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Lazaro Nyalandu kwa uamuzi wake mtukufu kabisa wa kuamua kuhamia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati na niwaombe wenzetu pale wenzetu wanapofanya maamuzi wa huko kuja huko au wa huko kuja huko isichukuliwe ni uadui tunabadilishana tu kila jambo na wakati wake, msianze kuwapa majina mabaya mukasema wanarembua macho, ni mafisadi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna orodha ya wote mnaowadhania huku hawafai kuweko huko hawa hawatafaa kuweko huku, kwa hivyo mnabidi muwaeleze mapema kama ninyi hana sifa kuwepo. Msingoje akitoka huko akija huku ndio mnaanza kufichua mabaya yake kichokuwa shinda kukila msikitie hila. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Mpango, kwa mara ya kwanza baada ya Mheshimiwa Spika juzi kuwataka Wabunge wafunguke kuishauri Serikali kuhusiana na Mpango huu nimefurahi kuona kwamba hakukuwa na utofauti bali walikuwa ni Wabunge wote wa Bunge hili kutoa mawazo ya kuionesha Serikali pale inapokosea na inapotakiwa kujirekebisha. Kwa dhati kabisa niwapongeze Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Sugu na wenzao wote ambao haionekani tofauti ya kiiitkadi ya kivyama bali wote tunalenga katika kuilekeza Serikali maana na uhalisia wapi tunataka kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yote kwa dhati, nimwambie Mheshimiwa Mpango, katika mambo yaliyotusikitisha hapa wengine ni pale Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wanaposimama hapa na wakasema kwamba unakaidi kupokea mashauri na maelekezo yao. Sasa kama Kamati ndio wawakilishi wa Bunge zima katika sekta wanayoismamia kwa hivyo unapoanza kuidharau Kamati katika mashauri wanayokupa maana yake ni kwamba hata sisi humu utatupuuza lakini na sisi tunatimiza wajibu wa kusema yale tunayoona yanafaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo dhamira ya Rais wetu na mpango mkuu wa kufufua viwanda hatuoni mafanikio yanayopatikana kama wenzetu walivyosema kwamba kuiachia Serikali kila kitu itekeleze kwa pesa yake hilo jumbo haliwezekani. Hayo ni mashauri ya kutaka *private sector* iingie katika kuendesha biashara ili tukwamuke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mdogo, leo ni mwaka wa 10 Mheshimiwa Mpango tumekuwa tukiimba nyimbo ya kukifufua Kiwanda cha *General Tyre* cha Arusha lakini hebu niambie leo tumefikia wapi?

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara, tumefanya ziara mara kadhaa, tumependekeza mara kadhaa, kama kuna umuhimu wa viwanda vyatya sukari pia katika kiwanda muhimu katika nchi ni kiwanda cha matairi.

Leo hebu niambieni ni Mbunge gani anayefika hapa bila kutumia gari? Gari linakwendaje bila tairi? Mahitaji ya tairi ni makubwa sana. Kama tunashindwa kufufua kiwanda muhimu kama kile ambacho ukiangalia kwa umakini soko la matairi yatakayozalishwa pale ukienda kwenye Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma pekee hawawezi kulibeba soko la matairi yatakayozalishwa pale *General Tyre*, tunataka nini?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda wangu ni mfupi sana, nataka nijielekeze...

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, mmeshagawana.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Dakika tano?

MWENYEKITI: Wakati mmetoa maamuzi alishatumia dakika zako kwa sababu maamuzi yaliletwa yamechelewa, alishatumia dakika zako wewe mbili na nusu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Basi nipe nimalizie.

MWENYEKITI: Nakuomba tafadhali Mheshimiwa Khatib kaa, kama unakwenda kusali nenda kasali ni jambo muhimu hilo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Saada Mkuya, ajiandae Mheshimiwa Jaku.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu katika Ijumaa hii ya leo kupata nafasi hii adhimu ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

pamoja na wasaidizi wake wote kutohana na kasi ya utendaji na utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuchangia Mpango, Mheshimiwa Turky aligusia kidogo *title* ya kitabu hiki ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Taifa hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaundwa na pande mbili. Cha kusikitisha na cha fadhaa kabisa ni kuona hakuna hata eneo moja liliopangiwa mpango angalau tu ikaelekezwa katika upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano na hili nataka niliseme wazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kwako, Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati tunajadili bajeti mwezi Juni, 2017 baadhi ya wenzangu tunaotoka katika upande wa pili wa Jamhuri tulichangia maeneo fulani fulani, lakini kwa masikitiko makubwa hakuna hata eneo moja lilioguswa likajibwa hoja angalau kule upande wa pili wakasikia. Mimi nilichukua hatua ya kwenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha mbona hujajibu angalau basi hoja mbili ili wananchi wa upande mwingine wa Muungano waone kwamba na wao *they are part and parcel* ya Jamhuri ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliniambia muda mchache na majibu yalikuwa mengi. Nilijisikia vibaya kwa sababu kama una *responsibility*ya pande mbili za Jamhuri maana yake angalau ungechukua hoja mbili ukazijibu. Sasa aliniambia kabisa kwamba muda mchache, hoja zilikuwa nyingi kwa hivyo mimi nitakupa *document usome*, *this is exactly* jambo ambalo ameniambia nimesikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachangia hapa na nimeona *tendency*ya Wabunge ambao wanatoka upande mwingine wanachangia. Tuombeni Mungu angalau hoja mbili, tatu zijibwe muda uwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda katika Mpango kuna jambo lingine kabisa la kusikitisha, kwenye eneo la utalii, bishara na masoko, hivi kwa namna gani au kwa namna yoyote unapotaka ku-*promote* utalii unaichaje Zanzibar? Yaani hakuna na haielezeki! Utakuwaje na mpango wa ku-*promote* utalii Tanzania bila kuingiza Zanzibar, haiwezekani! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yanaweza yakawa *very simple* ukisema habari ya Zanzibar majibu yanakuwa *very simple* kwamba hilo siyo jambo la Muungano. Hivi jamani kama kutakuwa kuna Wizara tatu za Muungano kwa nini sisi Wabunge tusiwe watatu tu humu ndani kutoka Zanzibar? Kwa nini tuko 53? Kuna masuala mengine hayahitaji lazima iwe ni Wizara inayoshughulika na Muungano. Kuna *issues* nyingine zinahitaji *coordination* za pande mbili. Kama hii *issue* ya utalii, hivi kweli kutakuwa na programu au *project* yoyote bila kui-*include* Zanzibar? *Is not possible*, haipo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye elimu ya juu, hii imo kwenye jambo la Muungano, *there is nothing*, Waheshimiwa hakuna jambo lolote ambalo limeguswa. Sasa sijui huu Mpango wa Taifa lipi hatujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine kwenye masuala ya habari, utamaduni, sanaa, ustaarabu, burudani na michezo. Sasa hivi tumeona Tanzania inaingia katika ramani ya michezo, lakini hakuna *specific plan* ambayo itaweza ku-*accommodate* angalau kujenga uwezo wa wachezaji wa michezo mbalimbali katika kuitangaza Tanzania, hakuna. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii sanaa ya uigizaji, hawa waigizaji wameachwa kabisa. Toka juzi tunasikia wao wenyewe wamekwenda Kariakoo, sijui wanapambana na wale *piracy* na kadhalika, lakini sisi kama Serikali hakuna mpango wowote wa kuwasaidia wasanii wa Tanzania. Leo *GDP* ya Nigeria imekuwa *rebased* kutokana na *contribution* ya sanaa katika uchumi wao. Sisi tumefanya *rebase* kwa ajili ya kuingiza *sectors* mpya ikiwemo hii ya sanaa lakini hakuna

mpango wa kuendeleza sanaa hii. Kwa hiyo, katika Mpango wetu wa Maendeleo naona hilo limeachwa kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya ushirikiano wa kimataifa, inasikitisha na inashangaza kuona katika eneo muhimu la *diaspora* limeachwa. *Diaspora* Ethiopia wameungana pamoja wanajenga hospitali kubwa kabisa ambayo *ownership* ni karibu asilimia 90 ya Waethiopia wanaoishi nchi za nje, sisi kwetu hakuna jambo lolote ambalo angalau tumeweka *consideration* ya kuangalia *mobilization* ya *resources* kutohana na *diaspora*, hakuna! Vile vyanzo vyetu vya mapato ni vilevile tokea Taifa hili lilipozaliwa.

Mheshimiwa Dkt. Mpango wewe ni mweledi tumeshakuwepo sana katika semina na vikao vya *resource mobilization* lazima tuangalie njia mpya ya kuweza ku-*tap resources* zilitopo ili kuelekeza katika Mpango wetu wa Maendeleo. Kuna *role* ya *diaspora* iko wapi, wenzetu wanai-issue *diaspora bond* na katika *article* moja ya *World Bank*, Tanzania imo kabisa katika nchi ambazo zina *potential* kubwa ya kuweza ku-*mobilize diaspora bond*. Hebu liangalie hili tutapata pesa nyingi. Watanzania wenzetu wapo kule lakini hawaoni kama Serikali ina nia ya kuweza kuwasogeza karibu ili na wao wakasaidia kuchangia maendeleo pamoja na uchumi wa nchi yao kama ambavyo wanafanya wenzetu wa Nigeria, Ethiopia na Uganda. Naomba eneo hili tuliangalie kwa mapana yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, sera ambazo zinakuwa *employed* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zina *effect* hata kule Zanzibar. Tumeona na tunasifu kazi nzuri sana ya Serikali kwenye *list* ya viwanda ambavyo vinaendelea kujengwa na ambavyo vimeshajengwa. Waheshimiwa, *the list is long* lakini hakuna hata sehemu moja tukasema angalau tutashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ku-*tap investors* ambao wataweza kujenga kiwanda kitakachotumia malighafi ya karafuu, hiyo *consideration* hakuna, inasikitisha! Sasa Mpango huu wa Taifa, Taifa lipi bila ya Zanzibar, inasikitisha! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini juu ya hivyo, nimesahau jambo moja, nimepata kuulizia hivi jamani Mheshimiwa Waziri wa Fedha anashughulika na pande mbili za Muungano, *at any point of time* tokea ameteuliwa kuwepo pale ofisini alipata kwenda Zanzibar katika kikao cha kazi, siyo kikao cha kero za Muungano, kikao cha kazi? Nikaambiwa hajafika. Nadhani ni jambo ambalo linasikitisha. Nimeambiwa umekwenda katika vikao vya kero za Muungano, tunashukuru sana kwa sababu *ku-participate* ni katika hatua ya kutatua kero za Muungano, lakini kikao tu cha kuona kwamba kuna mashirikiano baina hizi Wizara mbili, ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano na ya Zanzibar nimeambiwa hatujamuona Mheshimiwa Waziri. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri katika sehemu zako za kazi ni pamoja na Zanzibar uwe unafika angalau usikie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo moja ambalo tulipata faraja kusikia *around two weeks ago* kwamba Makamu wa Rais amezindua Sera ya *Microfinance*, lakini kwenye Mpango na katika maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2018/2019 hakuna sehemu ambapo kuna mkakati maalum wa kuweza kusaidia hizi *microfinance institutions* zikiwemo *SACCOs* pamoja na *VICOBA*. Hizi *institutions* zinasaidia sana hususani akina mama ambao wako vijijiini lakini lazima wawe katika aidha *policy framework* au *legal framework* ili na wao waweze *ku-access* mikopo kutoka katika *banks*. Sasa haijawekewa kitu chochote katika Mpango huu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mheshimiwa Waziri kama nafasi itakuruhusu utakapokuwa unajibu hoja, naomba ujibu pamoja na hili ili wananchi wakusikie hususani wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kwenye *promotion* za utalii kule Zanzibar kuna vivutio, tunajaribu kuweka mambo mbalimbali pamoja na wakati wa *low season* watalii hawaendi lakini sisi tunajaribu kuweka matukio ili tupate *ku-tap*. Tuna *Zanzibar International Film Festival (ZIFF)* pamoja na Sauti za Busara, ni vitu ambavyo angalau basi

vingekuwa *taped* katika haya masuala ya mipango ili kuona kwamba utalii umo katika Mpango wa Taifa kusaidia Zanzibar pamoa na Tanzania lakini imekuwa ni *competition*. Sasa hivi nimesikia kumeanzishwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Jaku, ajiandae Mheshimwa Papian.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kukupongeza kwa dhati kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Bila kuniruhusu nisingeweza kuchangia hoja hii kwa hiyo nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa jithanda anazochukua kwa wananchi wake na kwa jinsi anavyowatumikia. Nichukue fursa hii tena kuwapongeza wale Mawaziri na Naibu Mawaziri waliopanda hivi juzi kwa kupata vyeo hivi na niwape pole waliokuwa wakitegemea, lakini hawajapata nafasi hizi mpaka muda huu. Niwaombe wasikate tamaa, Mwenyezi Mungu siyo Athumani lakini niwaambie tu uteuzi wao huu wanaujua nini maana yake? Uteuzi huu Mheshimiwa Rais allitoa Mawaziri na Naibu Mawaziri ili wamsaidie kutumikia wananchi kinyume chake Mawaziri na Naibu Mawaziri simu mnazifunga, hamuwatumikii wananchi, siyo kitu kizuri. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaziteua Wizara kama Wizara ya Afya wenye matatizo ya afya waende afya, Wizara ya Elimu waende wenye matatizo na elimu, Wizara ya Ardhi waende wenye matatizo ya ardhi lakini kwa masikitiko simu ukimpigia Waziri hapokei, ukimpigia Naibu Waziri hapokei, humu ndani tumo sawasawa haya mambo yanageuka. Aliyeko mbele mnganje nyuma, aliyeko juu msubiri chini atateremka tu. Hivi vyeo ni dhamana na tutakwenda kuulizwa siku ikifika tumewatumikia vipi wananchi. Kuna

milango mitatu ya kuingilia humu ndani ya Bunge hili, kuna Jimbo kutoka Ikulu, kuna Viti Maalum na uchaguzi wa wananchi, hiki chombo kina uzito kutokana na wananchi. Wananchi ndiyo waliopotupa dhamana ya kuja kusema matatizo yao humu ndani. Kuna siku tutakwenda kuulizwa hizi dhamana zetu tumezitumia vipi, haya mambo ya kupita tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika mchango wangu sasa kuhusu *TRA*. Mheshimiwa Waziri kwa masikitiko na unyonge mkubwa sana kitendo ulichokifanya cha kutatua kero ya Kenya na Tanzania kuhusu maziwa na *cigarette* umechukua muda mfupi sana, lakini kero ya Zanzibar bado kila Waziri kinamshinda. Leo Muungano wetu huu tunasema kwa mdomo tu tunataka uendelee kudumu kwa vitendo. Mali inayotoka Uganda, Kenya, Burundi, Zaire, Zambia ikiingia Tanzania wala huulizwi kitu, leo mali inayotoka Zanzibar ukiingia nayo Dar es Salaam utafikiri umeleta unga, huu uonevu wa aina gani? Dkt. Mpango Wazanzibari hamtufanyii haki. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mzanzibar kachukua gauni zake tatu anakuja hapo bandarini anaambiya weka chini, *tvu moja, mbili anaonewa, hii haki ikoje?* Nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Saada Mkuya, kazungumza vizuri sana lakini huu Muungano tunaosema ni wa upande mmoja tu jamani? Tunasema huu Muungano uendelee kudumu na mimi nasema uendelee kudumu, Zanzibar ukiacha zao la karafuu tegemeo kubwa ni biashara. Wenzetu Tanzania Bara *Alhamdulillah*, endeleeni kushukuru tuna madini, mbuga na neema nyingi tunazo lakini leo biashara ile nguo tatu au nne, miche mitatu ya sabuni unasumbuliwa pale mwisho mchele unaonunua pale bandarini unalipishwa pana kimizani kidogo kimewekwa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala siyo la upande mmoja Mheshimiwa Saada kazungumza bado hujafika Zanzibar, mimi nikuombe ufile. Pindipo utakapokusanya mapato Mheshimiwa Rais atakusifu, tuangalie biashara, huku kidogo, huku kidogo, kuku anataga yai moja ukamlazimisha

mayai matatu utamuua, utakosa kuku. Chukua huku kidogo, huku kidogo pishi inajaa lakini kuku yule anataga yai moja, unamlazimisha leo leo atage matatu atakwenda wapi, tutaua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu twende Kariakoo ukaangalie milango ya maduka nani anaitaka saa hizi? Samora mlango ulikuwa unakodishwa bei kubwa sasa hivi milango imefungwa. Fikiri Mheshimiwa Waziri huu ni ushauri wangu wa bure wala sitaki kulipwa mimi. Kaa na wafanyabiashara utazame nini tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muungano Zanzibar tunauhitaji kwa kila hali mionganoni mwao ni mimi kutokana na udogo wetu, lakini mzigo utoke Kenya, Rwanda, Burundi hauulizwi kitu, mzigo ukitoka Zanzibar ukifika hapa aibu. *TRA* ni moja, *formula* yake ni moja, vigezo vyake ni vimoja, Waziri nikuombe kwa masikitiko makubwa, Wanzanzibar ukiacha karafuu wanategemea biashara. Juzi umetatua tatizo la Kenya kwa muda mfupi tu, leo unatuaacha sisi ndugu zako wa damu. Umetatua juzi tu tumekupongeza lakini litatue na hili pia. Taa huwashi nje, unawasha kwanza ndani ya nyumba yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawashaje nje kabla ya kuwashaa ndani huwezi kuona na sadaka sisi tunasema inaanzia nyumbani ndipo utoe nje. Kwa hii kero dada yangu kazungumza sana hapa, fanya uwaite wafanyabiashara, wanafunga milango wanaanza kuondoka. Tembea na kama uko tayari tufuatane nikakuoneshe mlango huu umefungwa, huu umefungwa utahesabu milango mingapi. Tufike wakati tupunguze, tujihurumie jamani mapato tunahitaji wewe kusanya mapato mazuri uone Mheshimiwa Rais atakavyokusifu. Nchi inataka kwenda kwa mapato lakini tukianza kubana kwa marungu, leo watu wananyang'anywa komputa zao wanavamiwa na *TRA*, polisi imekuwa *TRA* sasa hivi watu wanasumbuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri sisi sote humu ndani vyeo vyetu vimoja tunaitwa

Waheshimiwa tofauti tu ni Waziri na Waheshimiwa na haya mambo yanageuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kukaa. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Papian.

MHE. EMMANUEL P. JOHN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza napongeza kwa Mpango mzuri ambao umeletwa na Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa ajili ya kutengeneza dira ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nalotaka kuzungumza ni kuhusu mazao ya kilimo ambayo ni ya biashara, haya mazao ya tumbuku, chai na kahawa, ni mazao ambayo kwa muda mrefu yameshapoteza masoko hayana bei na wakulima wetu wanateseka. Nilitaka kuishauri Serikali kwamba sasa iangalie namna gani haya mazao ya kibiasara yanaweza yakapata masoko ili Serikali iweze kupata kodi, lakini na wakulima wetu waweze kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine nilitaka kushawishi, hili zao la mahindi nilitaka sasa na lenyewe liingie kwenye Mpango kwamba ni zao la biashara. Mkulima anapolima aweze kupata mazao yake, auze anapotaka aendeleee na maisha yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais ameshasema Serikali haina chakula cha kumgawia mtu, wakulima wameshaweka *reserve chakula chao*, chakula kilichopo hii *bumper harvest* iliyopo watu waruhusiwe waweze kupeleka mazao yao wanapotaka. Mtu asije na hoja kwamba tuna mikoa ambayo ina upungufu wa chakula, mwaka huu katikati mwezi wa saba na wa nane watu walikuwa wanachukua mahindi Kilindi na Kiteto kupeleka Shinyanga, leo hayo mahindi hayaendi kama kuna *deficit* Shinyanga kwa nini biashara hii haifanyiki leo? Ruhusuni watu wapeleke mahindi wanapotaka ili waweze kupata faida na waondoke kwenye umaskini.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea kweye kupanda watu wanahitaji mbolea na pembejeo, wapeni nafasi wakauze mazao yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Zambia wamezalisha mahindi mengi sana na kwa Wilaya za kina Mheshimiwa Kandege mazao yana *trespass* kwa njia za kawaida za panya yanaingia hapa. Mazao mengine yanapakiwa pale *border* yanapita yanakwenda upande wa Kenya. Ukiyaangalia yale mahindi ni meupe ni masafi wanapeleka Kenya hatupati kodi. Hivi leo sisi Watanzania wangepakia wakapeleka Kenya nchi yetu ingekusanya kodi. Mheshimwa Mpango unahitaji kukusanya kodi kutoka kwenye haya mahindi yanayokwenda Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gunia la kilo mia Kenya ni 7,500 mpaka 8,000, *it means* unazungumzia karibia shillingi shilingi 140,000. Mheshimiwa Dkt. Mpango ukikusanya pesa ya kodi pale mpakani Holili na Himo, wewe unahitaji pesa, mkulima amepata faida na barabara zetu hazijachimbwa na magari ya wengine badala ya magari yetu na mkulima wetu ameshapata faida. Turuhusu mazao yaende mkulima *ata-debate* mwenyewe wapi atapata chakula Rais ameshawaaga kwamba hakuna chakula cha msaada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la lingine tumekuwa na *Kakono Project* ambayo mwaka jana tuliiwekea mpango hapa fedha zake zipo, mkopo upo wa *African Development Bank*, Malagarasi ipo, pelekeni pesa hii miradi ianze ili iweze kuungeza umeme kwenye Gridi ya Taifa tuweze kupata faida. Nilihudhuria kikao kimoja pale Kakono, Mtukula nikakaa pale Misenyi, nikazungumza nikaona wale watu wa *African Development Bank* baadhi yao ni wa Kenya wanaendelea na *project*. Nilipokaa nikawaza kama *this guy's* apo kwenye hii *project* wana uwezo wa kuikwamisha mpaka *TANESCO* yetu hii miradi isiweze ku-*take over* ili kupata umeme.

Mheshimiwa Mpango naomba hili uende nalo uliangalie ili tuweze kuona ni wapi imekwamia hii *Kakono*

Project na Malagarasi ili tuweze kuzalisha huu umeme wa maji. Leo ukienda Mtera inazalisha megawati 80 lakini Mtera maji hamna, yamekauka, yatashuka kesho kutwa huwezi kuzalisha hizo megawati lakini ule umeme wa Kakono ni maji ya Nile hayatakati, hayatashuka megawati zetu 87 zitaingia kwenye Gridi ya Taifa na bado tutaendelea kupata faida, naomba hili liangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine uvuvi bahari kuu. Kuna Mheshimiwa mmoja amezungumza hapa, uvuvi wa bahari kuu sasa hivi Tanzania wanachofuata ni suala la leseni shilingi milioni 30, sijui shilingi milioni 40, ukivua saa mbili ndani ya bahari kuu una meli yako unatengeneza shilingi triliioni moja. Hicho ni chanzo Mheshimiwa Mpango nenda nacho, uje na mpango wa kutuambia tunanunua meli, tunavua bahari kuu, samaki za kwetu *tu-export* samaki tupate faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo, asilimia 70%, 80% ya Watanzania wanaenda kwenye kilimo, uje na mpango wa kuniambia benki hii inapataje pesa, wewe ndiyo unazo. Hii Benki ya Kilimo leo ndiyo inayokwenda kuokoa watu, benki nyininge sasa hivi *zimesha-stuck*, haziwezi ku-*invest* kwenye Kilimo kwa sababu ya hali ilivyo na mikopo mingi chechefu sasa hivi ni ile ambayo *wali-inject* kwenye kilimo hawawezi kwenda zaidi kwa maana hiyo sasa kilimo kitaenda kushuka. Nikuombe Mheshimiwa Mpango, Benki ya China (*China Agricultural Bank*)ina uwezo wa kutukopesha, itafutie hii benki mtaji iweze kukopesha wakulima wetu ambaa ndiyo pesa hiyo itakayozunguka mwisho wa siku utakutana nao kwenye *TIN*, vioski na mama ntilie, upate watu wa kutoza kodi ambaa wameshapata huku kwenye kilimo. Mheshimiwa Mpango hii benki naomba ukija utuambie unaenda kutengeneza shilingi ngapi huko ndani unaichomekea hapo ili iweze kusogea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la afya. Miaka ya 85 kurudi nyuma tulikuwa na vyuo vyetu vya *RMAAs* (*Rural Medical Aids*), tulikuwa tuna-*produce* wale watu ambaa walikuwa wanakwenda kufanya kazi kwenye zahanati zetu

kule vijijini leo zahanati tunazozijenga kwenye mpango wa Wizara ya Afya kwa maana ya afya hazina wataalamu. Tufanye mpango tuwarudishe hawa *Rural Medical Aids* wakafanye kazi kwenye zile zahanati zetu kwa sababu kuna *nurse mmoja* atagawa dawa, atazalisha wanawake au atafunga vidonda. Watu hawa wakipatikana kwenye zahanati zinazojengwa nchi nzima afya za watu wetu zinaweza kubaki salama. Nikuombe muangalie ni namna gani mtapanga kurudisha wataalam hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango nikushukuru kwanza jambo moja ambalo umeonyesha kwenye Mpango hapa, suala la kujenga barabara ya kutoka Handeni - Kibirashi - Kiteto – Chemba - Kondoa – Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe hii barabara sasa kwa sababu imeingia kwenye Mpango ipate pesa iweze kutengenezwa. Wakati hii barabara inatengenezwa tunaomba mtutafutie wafadhili kwenye ukanda huo huo wa kutengeneza viwanda vyta kuchambua mchele, kutengeneza unga, kusindika mafuta ya alizeti, kuzalisha juisi ya matunda huko Tanga ili *along that road* na bomba la mafuta wakati linapita, magari yanapita kupeleka mizigo bandari ya Tanga ili ile mizigo inapopita kuelekea Kanda ya Ziwa, Rwanda, Burundi, Uganda na Kongo basi kuwepo na hivyo viwanda viweze kuzalisha na hayo mazao ya mbegu yaende kwenye hizo nchi ili na sisi wakulima wetu na wananchi kwenye hizo kanda waweze kuwa wamepata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru lakini nikuombe msiwafunge Watanzania waweze kutembea *East Africa*. Mmeona speechya Museveni kule kwenye bomba la mafuta Tanga ametukana watu weupe hataki kusikia hii biashara, anasema *East Africa* tuna *population* ya *one seventy thousand people* ambapo tunaweza kuwa ni soko la mazao na kitu chochote tunachozalisha hapa nchini. Watanzania msiwafunge acheni watoke mkiwabana sana *they will burst. (Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakibete.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kushiriki kuchangia maoni yangu juu ya Mpango. Kabla kuanza kuchangia kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia niwapongeze Mawaziri wote walioteuliwa na zaidi nimpongeze Mheshimiwa Mpango na Naibu wako pamoja na watendaji wote katika Wizara hii ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Mpango wetu ukianza na ule ukurasa wa 34 hasahasa katika suala la afya imeonesha kwamba utajikita zaidi katika kuboresha Hospitali za Kanda na Mikoa mbalimbali. Mimi nataka niongezee jambo moja kwamba katika Sera ya Afya kama ambavyo tunajua wote inatakiwa kila kijiji kiwe na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya na kila Wilaya iwe na hospitali. Kwa mantiki hiyo katika huu ukurasa wa 34 sijaona kama haya mmeyazingatia kufuatana na Sera ya Afya ambavyo inataka. Kwa hiyo, ningependa hili jambo mlizingatie mtakapokuwa mnaleta ile *final draft*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili katika jambo hilo hilo ni katika suala la matibabu (*telemedicine*). Nimeona mmekazia sana kupeleka ama kutibu watu ambao tayari wameshaathirika na magojwa mbalimbali, aidha, iwe nyemelezi ama yawe magojwa yale ya kuambukiza. Kwa hiyo, nilitaka nitoe maoni yangu kwamba ni muhimu sasa kutoa elimu kwa jamii kuhusu magonjwa mbalimbali kabla ya kuanza kuyatibu kwa sababu tunasema *prevention is better than cure* kwa maana nyingine ni kheri kinga kuliko tiba na ndiyo maana Serikali inatumia pesa nyingi sana kutibu wakati pengine tungetumia fedha nyingi zaidi kutoa elimu kwa hayo magojwa nafikiri kizazi chetu cha Tanzania tungekuwa tuko salama zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependekeza kwamba muongeze neno ama teknolojia ya kutibu kwa njia ya mtandao (*telemedicine*). Hii teknolojia nimekuwa nikizungumza humu Bungeni tangu mwaka jana kwa maana itarahisisha kupunguza kwanza muda wa mgonjwa kwenda kwa daktari lakini pili elimu hii ama teknolojia hii itatibu

wagonjwa wengi zaidi kwa sababu daktari anaweza akawa yuko Dar es Salaam anatibu wagonjwa ambao wako mikoani. Kama ambavyo mnafahamu madaktari tulionao ni wachache inabidi daktari mmoja huyohuyo awe *fully utilized* kutibu wagonjwa wengi zaidi kwa njia ya mtandao kwa maana kwamba mgonjwa anaenda sehemu ambapo kuna mawasiliano na anawasiliana na daktari wake *through telemedicine*. Kwa hiyo, ningefurahi zaidi kuona hii *telemedicine* inakuwa *implemented* hapa nchini Tanzania. Najua mmeshaanza *pilot study* lakini ni vizuri zaidi kuweza kufanya haraka zaidi kwa mikoa mingine kwa sababu wagonjwa wengi wanarundikana mahospitalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine nikija katika suala la nishati kwa maana ya umeme, ukisoma katika Mpango wetu tumetilia mkazo zaidi kwenye umeme wa maji. Umeme huu wa maji kama mnavyofahamu kwamba unatokana zaidi na maji lakini wakati mwingine mazingira yanakuwa si rafiki sana kwa kuwa vyanzo vya maji huwa vinakauka kufuatana na mabadiliko ya tabia ya nchi ya dunia.

Kwa hiyo, ningependekeza kwamba ni vizuri sasa pia tukajikita katika umeme unaotokana na joto ardhi (*geothermal*), sijaona katika Mpango wetu hapa. *Geothermal* ni muhimu kwa sababu ule ni umeme ambao tunaita ni *renewable* tofauti na maji yakishatumiwa wakati mwingine kama vyanzo vimekauka na huku umeme hatutaweza kupata.

Umeme upo wa aina nyingi kuna ule wa upепо, wa gesi ambao tuko nao lakini nao bado haujawa *effectively fully utilized* pia ni vizuri tukaendelea kuu-utilize, kuna umeme wa *solar energy*, *biomass energy* lakini nikazie zaidi katika *geothermal* kwa sababu kuna maeneo mengi katika nchi yetu ya Tanzania *geothermal* ama jotoardhi umeme huu unapatikana. Zaidi katika umeme kuna hili jambo la bomba la gesi ningefurahi ama Watanzania wengi wangefurahi kuona bomba hili linaanza sasa kusambazwa mikoani kote na lisiihie tu Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nikija katika suala la maji, maji ni uzima, maji ni uhai, maji ni utu na maji ni roho. Waheshimiwa Wabunge wengi mmelalamikia hapa mara nyingi ukisoma ule ukurasa wa 32 tunaona kuna baadhi ya miradi ambayo itaendelea katika mpango ujao, ni vizuri katika Mpango wetu kama tutaunda chombo maalum kama ambavyo imeundwa *TARURA* kwamba chenyewe kijikite zaidi katika kuleta maji kwa maana ya vijiji na mijini. Sasa hivi kwa tafiti niliyoifanya nimeona Halmashauri nyingi sana hazina wataalamu na ndiyo maana miradi mingine mingi inashindwa kuendelea kwa sababu hamna ile *M&E (Monitory and Evolution)* katika ufuutiliaji wa miradi. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba kiundwe hicho chombo maalum kwa ajili ya suala hili la maji vijiji na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija katika suala la kilimo, ukisoma ule ukurasa wa 28 utaona kwamba kilimo kimetiliwa mkazo lakini wewe Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba sasa tuna shida kubwa sana na masoko ya mazao ambayo tumezalisha, kila zao bei yake imeshuka. Kwa mfano, ukichukulia mahindi yameshuka, viazi nichukulie mfano kwa mfano kule tulikokuwa tunalima nyumbani debe moja lilikuwa linauzwa shilingi 10,000 hadi shilingi 15,000 lakini sasa hivi debe moja ni shilingi 2,000 kwa maana ya gunia zima ni shilingi 10,000 badala ya shilingi 65,000.

Kwa hiyo, kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara katika Mpango wetu kama wataanzisha *section* ambayo itakuwa inatoa taarifa kupitia njia ya teknolojia kama simu *whatever* kwa wakulima wote, tuwe na *database* ya wakulima ambao wanalima mahindi, choroko na kila aina ya zao wanapewa taarifa kupitia hizo simu walizonazo ama hiyo *database* ili wawataarifu sehemu gani masoko hayo kwa sasa bei ipo juu. Kwa hiyo, kama Mpango huu ungezingatia hilo ingekuwa ni jambo zuri na lenye tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kuwekeza kwenye kilimo tumeona mazao kama chai, mahindi na baadhi ya maeneo bei ya chai ipo chini sana, lakini wenzetu jirani Kenya

iko bei za juu, kwa sababu wametafuta masoko nje ya nchiyao hasa hasa Uingereza. Kwa hiyo na sisi kama tungeweza kutafuta hayo masoko ingekuwa rahisi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija katika suala la teknolojia, tumeona katika ukurasa ule wa kwanza wa mwongozo wa maandalizi wa mpango wa bajeti umezungumzia mifumo mingi ambayo itatengenezwa, mimi nitoe angalizo hapa. Tumeona teknolojia hii imekuja kwa kasi katika nchi yetu ya Tanzania pia nitoe angalizo kwa maana ya mifumo hiihii ndiyo inatumika katika masuala ya udukuzi.

Kwa hiyo, lazima tuwe *very sensitive* sana tunapo-*implement* mifumo hii kwa kuwa hata wale wanaofanya *programming, coding* na vitu vingine vyote wanajua namna gani ya kuiba kupitia mifumo hii kwa kuwa mimi na wewe ambaao ni *end user* hatuwezi kujua lakini kwa kuwa mimi nimeyaishi haya nafahamu. Kwa hiyo, ni vizuri sana haya mambo yazingatiwe katika Mpango wetu. Tusiletu tu mifumo kama kuleta lakini tujue pia na *consequences* baada ya kutumia mifumo hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona katika hii mifumo kwa mfano hii ya *EFD*, *EFD* ni mifumo ambayo inatumika kukadiria mapato lakini risiti zake zile baada ya muda, ukinunua leo bidhaa ukapewa risiti baada ya wiki moja ama wiki mbili au mwezi zinafutika maana yake unakuwa hakuna tena ushahidi wa kusema wewe ultumia ile *EFD*. Kwa hiyo, ni vizuri zaidi kama hizo *integrated systems* zitakuwa na mifumo ambayo inatoa risiti ambayo ni *permanent*. Kwa nini mfano ukitoa *photocopy* karatasi idumu zaidi wakati *EFD* ambayo ni ya fedha isidumu, kwa hiyo, nafikiri hilo pia mliweke vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa kuwa hizi teknolojia ni nydingi wakati mwengine wanatumia *commercial software* ambazo ni gharama zaidi, tunaweza tukafikiri tunapunguza gharama lakini kumbe tunaongeza gharama.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri watumie *open software* ambazo zinatumika nchi nydingi za Scandinavia na ambazo ndizo ziko *applicable* duniani kwa sasa, kwa sababu hizi *commercial software* ni gharama na tunakuwa hatujapunguza chochote kile zaidi ya kuongeza gharama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika suala la TEHAMA, ingependeza na ingefaa zaidi kuundwe Bodi ya wana-TEHAMA kama ambavyo kuna Bodi za Uhasibu, Bodi za Ukandarasi, kwa sababu teknolojia ndani ya nchi yetu inakuja kwa *speed* zaidi. Kama tutakuwa na hawa watu kwa pamoja maana yake itaturahisishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine kama Finland wameendelea zaidi kwa sababu waligundua ile Kampuni ya Nokia, ukienda Korea Kusini kuna Samsung, ukienda Marekani hivyo hivyo lakini tukiwa na Bodi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakuwa na Mheshimiwa Kiza Mayeye, Mheshimiwa Devotha Minja na Mheshimiwa Matiko, kama kawaida makubaliano yenu ni *two in one*. Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilsitishwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na
Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2018/2019**

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wachangiaji wetu wa jioni leo anaanza Mheshimiwa Kiza Mayeye, ajiandae Mheshimiwa Devotha Minja na Mheshimiwa Matiko.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi kwa kunipa uzima na afya tele na kunifikisha mahali hapa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikishukuru chama change, Chama cha Wananchi (CUF) chini ya Mwenyekiti mahiri Profesa Ibrahim Lipumba pamoja na Naibு Katibu Mkuu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa kusimamia vizuri Katiba ya Chama cha Wananchi (CUF). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano, kutupokea vizuri, kuwa pamoja na sisi, kutuelekeza na kutufundisha mambo mbalimbali toka tulivyoingia Bungeni mpaka siku hii ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Phillip Mpango kwa Mpango huu wa Maendeleo, Mpango huu ni mzuri lakini haimaanishi kila kitu kizuri hakina kasoro. Kwa hiyo, mimi

nimpongeze lakini pia naomba nichangie kama ifuatavyo katika Mpango huu wa Maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza nataka nianzie katika suala zima la hawa wawekezaji. Serikali yetu inasisitiza na inasema kwamba tunahitaji wawekezaji. Kwa hiyo, ningeomba Serikali yetu iwapo wawekezaji uwezo wa kuja kuwekeza katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. Kuna maeneo ambayo kwa mfano ninakotoka Mkao wa Kigoma, huu ni mkoa ambao uko katika *plan hii ya Regional Economic Zone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkao wa Kigoma mpaka sasa kuna zaidi ya heka 690 katika eneo la Kisezi ambalo limetengwa kwa shughuli hizi za uchumi. Ningemuomba Mheshimiwa Waziri, mhakikishe kwamba mnavutia wawekezaji katika eneo hili kwa sababu eneo hili ni *potential*, ni eneo ambalo tukilitumia vizuri kwa uchumi tutainua Pato la Taifa na hata mkoa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwambie Mheshimiwa Waziri katika eneo hili la Kisezi tayari kuna mwekezaji ambaye anatengeneza umeme wa jua na mpaka sasa ameshatengeneza megawati tano, lakini kuna ukwamishaji. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama Serikali yetu inasema kwamba inatoa kipaumbele katika sekta binafsi ihakikishe umeme huu wa jua ambao mwekezaji huyu ameuweka katika eneo lile uweze kuunganishwa na *TANESCO* Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu *TANESCO* wanakataa kuunganisha, lakini mpaka leo Kigoma hatujaingia katika Gridi ya Taifa. Ningeomba tuingie katika mpango wa Gridi ya Taifa na sio Kigoma tu bali ni Mikoa yote ya Magharibi ikiwepo Sumbawanga, Katavi na Kigoma. Kwa hiyo, naomba katika Mpango huu mhakikishe kwamba mikoa hii tunaingia katika Gridi ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *TANESCO* Kigoma wanasema kwamba hawawezi kuunganisha umeme huu

lakini katika akili ya kawaida unajiuliza ni kwa nini hawataki? Kwa sababu kama mwekezaji huyu anatumia shilingi 490 kwa *unit* moja *TANESCO* Kigoma inatumia shilingi 700 ka *unit* moja kwa akili ya kawaida unaona kabisa kwamba mwekezaji huyu umeme wake uko chini. Ni kwa nini Serikali haitaki mwekezaji huyu umeme wake uunganishwe *TANESCO* Mkoa wa Kigoma? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika maeneo yale ambayo Serikali imeyatenga kama maeneo ya maendeleo, nirudi Kigoma. Kigoma mpaka dakika hii bandari kavu imeanzishwa, hii *Central Corridor*, Umoja wa Nchi za Maziwa haya Makuu wamefikia uamuzi kwamba Kigoma iwe ni bandari ya mwisho kwa mantiki kwamba watu kutoka Burundi, Kongo badala ya kufuata mizigo Dar es Salaam wataweza kuifuata Kigoma na tayari eneo limetengwa la Katosh - Kahagwa, tunatengeneza kitu tunasema *C/F* Kigoma. Kwa hiyo, tutakuwa na bandari kavu pale na tayari watu wamepisha ujenzi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri katika Mpango huu tuhakikishe kwamba bandari hii inaanza mara moja kwa sababu kupitia bandari hii vijana wa Kigoma watapata ajira lakini sio Kigoma tu Tanzania nzima kwa sababu huu mpango ni wa Taifa watapata ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeiti, pia nimwambie Waziri kwamba mbali na ajira mzunguko wa pesa utakuwa ni mkubwa katika Mji wa Kigoma na mzunguko wa pesa ukiwa mkubwa katika Mji wa Kigoma hilo ni Taifa, Taifa tutapata pato. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri ufanye unavyoweza bandari hii ianze mara moja. Labda ningejua, Wizara ya Fedha mpaka sasa mmejipangaje katika suala hili na Mamlaka ya Bandari imefikia wapi katika utekelezaji wa maamuzi haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Mpango wa Mheshimiwa Waziri. Hakuna mahali ambapo nimeona kuna uwezeshaji wa kijana na mwanamke. Hakuna mtu asiyejua kwamba kijana ni mtu muhimu katika Taifa hili lakini hakuna mtu asiyejua kwamba mwanamke ni mtu muhimu katika

familia na Taifa. Naomba sasa Serikali ije na Mpango madhubuti wa kumwezesha kijana huyu ambaye leo anamaliza shule lakini hana ajira na mama huyu ambaye amekaa nyumbani hana kazi. Tuandae mikakati ambayo itamwezesha mama, wote tunajua mama ni nani katika familia, ukimwezesha mama atasomesha watoto. Kwa hiyo, tuwe na vyanzo vya kuwasaidia akina mama, mabenki yatoe mikopo kwa akina mama. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri katika Mpango unaokuja umfikirie sana kijana na mama wa Kitanzania, *SACCOS* za akina mama Serikali iweze kuzisaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tena suala la uwekezaji. Kumekuwa na maeneo mengi ambayo wawekezaji wanataka kwenda kuwekeza lakini hakuna ushirikiano mzuri. Kwa taarifa nilizopipata katika eneo hili hili la Kisezi, Mkoani Kigoma Serikali ya Japan inataka kuja kuwekeza, watengeneze bidhaa wao wenyewe na watafute masoko wao wenyewe masoko wao wenyewe na watumie uwanja wa ndege wa Kigoma. Hata hivyo, Serikali haioneshi ushirikiano na wawekezaji hawa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeomba kama kweli tunataka kusonga mbele katika maendeleo ya Taifa tutoe kipaumbele katika suala zima la uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika suala zima la kilimo. Hakuna mtu asiyejua kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Wote hapa leo ni Mawaziri, Wabunge wengi tumesomeshwa na wazazi wetu kwa sababu ya kilimo. Naomba Mpango huu utakaokuja sasa muwasaidie wakulima, muwape pembejeo, mbolea, muwasaidie kupata masoko kwa sababu tunaposema leo tuna nchi ya viwanda, huwezi kuwa na viwanda kama wewe mwenyewe huna *product* za kupeleka kwenye kiwanda chako. Huwezi kusubiri mahindi kutoka Kenya, huwezi kusubiri korosho kutoka nchi jirani, tuhakikishe sisi wenyewe tunakuwa na *product* zetu ambazo tutazipeleka katika viwanda vyetu. Kwa hiyo, nimuombe sana Waziri, Wabunge wengi wameongelea kuhusu suala la kilimo, naomba kilimo kipewe kipaumbele, kilimo ni uti wa mgongo. Kama Serikali tunataka kusonga

mbele tuhakikishe kilimo kinathaminiwa kwa asilimia 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niongelee suala la elimu. Miundombinu ya elimu katika nchi yetu ni mibovu. Walimu wengi nyumba zao ni mbovu. Walimu hawa ndiyo wametufikisha mahali hapa leo. Walimu hawa ndiyo wamekutoa wewe Waziri, mimi Mbunge.

Kwa hiyo, naomba tuwathamini walimu kuanzia kwenye makazi, nyumba wanazokaa ni chache. Mikoa mingi ina changamoto walimu hawana nyumba na hata nyumba ambazo zipo unakuta haziko katika mazingira mazuri. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja na Mpango huu ahakikishe miundombinu kwa walimu, waongezewe mishahara lakini nyumba na makazi yawe mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika elimu nizungumzie suala la madarasa. Maeneo mengi hasa ya vijijini wanafunzi wanasomea nje, hakuna madarasa. Serikali ijitahidi kuweka madarasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nizungumzie miundombinu ya wanafunzi. Shule nyingi vijijini watoto hawana vyoo. Sasa jiulize kama tunashindwa kuweka matundu ya vyoo katika shule, binti huyu ambaye amekwenda shule, kwa sababu tayari kuna watoto wa darasa la saba wameshaanza kuona hali ya usichana wao, ameingia katika hali ya usichana hakuna maji, hakuna choo mniamweka katika mazingira gani binti huyu wa kike? Kwa hiyo, mniamfanya sasa huyu binti akishaingiwa na ile hali na wenzie wamemuona, kesho hawezi kurudi shule. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri mhakikishe mnawajali wanafunzi katika huduma za maji mashulenii, vyoo na hasa mtoto wa kike mumsaidie apate huduma hizi ili aweze kwenda shule kama watoto wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Minja dakika saba na nusu na Mheshimiwa Matiko dakika saba na nusu.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia sana kitabu cha Waziri Mpango, nisikitike tu kusema mambo mengi tunayoyaona ni yale yale, hakuna mambo mapya. Mheshimiwa Mpango nilitegemea ungekuja na mikakati mipyä kuhusu suala la bandari. Tukizungumzia bandari, tumeambiwa bandari ikisimamiwa vizuri inaweza ikasaidia kuongeza Pato la Taifa hili tukaachana na kukimbizana na watu wanyonge, wafanyabiashara wadogo ambao hawana nguvu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari illvyo hivi sasa ukiwaliza wafanyakazi wa bandari wanakwambia hawaijui siku yao wala saa. Bandari imegeuka kuwa siasa, viongozi mbalimbali wanakwenda na *camera* kwenda kutumbua viongozi wa bandari, wakurugenzi wa bandari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango atuambie asione aibu, kama unahitaji kusaidiwa kwenye bandari usione aibu sema. Nchi zingine zenye bandari zinafanya nini zinafanikiwa, kwa nini Tanzania hatufanikiwi? Tafuta *experts* wa kusaidie tufanyaje bandari yetu iweze kusonga mbele ichangie Pato la Taifa. Kila siku Mheshimiwa Mpango wewe unazungumzia, ooh, kodi zitaongezwa kwenye sigara na kadhalika, kumbe tuna bandari ambayo ingeweza kusaidia hata hizi sigara ambazo tunasema zina madhara tukaachana nazo kwa sababu kuna siku Watanzania wataamka watalielewa neno “no smoking” na sijui mapato tutapata wapi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Bandari ya Mtwara, yenye kina kirefu, lakini tumeifanyia kazi kwa kiasi gani? Leo tulikuwa tukisikia *TRA* wanatangaza mapato yao wamepata kiasi gani, lakini ukienda bandarini hakuna meli, meli utakayoikuta imebeba kokoto inapeleka Qatar kwenye

kuandaa Kombe la Dunia. Kwa nini meli zisiwepo pale ambazo tunajua zime-*import* tunahakikisha tunapata mapato? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango usione aibu, tafuta namna ambayo utashauriwa na wataalam waweze kusaidia tufanyaje bandari ya Tanzania iweze kusaidia kuongeza pato na kuwapunguzia mzigo Watanzania ambao wanakimbizana huko, mtu unamkuta ana kamtaji kake ka laki mbili anaambiwa anunue *EFD machine* ya shilingi laki nane, hii ni ajabu sana. Kamtaji ka laki mbili, laki tano unaambiwa nunua *EFD machine* ya laki nane, *are we serious?* Bandari isimamiwe na ifanye kazi yake vizuri iokoe jasho na vilio vya Watanzania. (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji anayezungumza sasa hivi, bandari yetu sasa hivi kwa takwimu inachangia asilimia 44 ya mapato na hilo siyo pato dogo, asilimia 44. Bandari ya Mtwara sasa hivi iko katika matengenezo inafanyiwa ukarabati wa kuongeza kina chake tayari kazi imeanza, sasa sijui anazungumza kitu gani? Naomba nimpe hiyo taarifa. (*Makofi*)

MWENTEKITI: Taarifa hiyo Devotha.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siipokei, nilifikiri ananiambia kwamba bandari inafanya kazi kwa zaidi ya asilimia 100, ananiambia 40? Bandari tunayo miaka mingapi toka uhuru mpaka sasa hivi tunazungumzia bandari hiyo hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu *fine* za barabarani. *Traffic* wametoka kwenye lengo la kusaidia kupunguza ajali za barabarani, sasa hivi wamegeuka kama maofisa wa makusanyo wa *TRA*. Nikizungumza hayo wanaotoka Dar es Salaam wanaelewa, shida wanazokutana nazo watu wenye magari, *traffic* hivi sasa wanafungua mpaka *bonnet* kuhakikisha wanakusanya mapato na kila mwisho wa mwezi wanatoa tathmini, tumekusanya milioni kadhaa kwa sababu ya matatizo na makosa mbalimbali ya barabarani, hivi hii ni faida ni hasara? Hivi hili ni tatizo au? Kwa sababu huwezi ukasema umekusanya mapato kwa *fine* za barabarani maana yake hujafanya kazi yako ipasavyo. Tultegemea wangkuja na taarifa kwamba ni namna gani wamepunguza ajali kutoka asilimia fulani kwenda asilimia fulani na siyo kutuletea mapato, hii sio kazi yao, ni kazi ya *TRA* hii. Kama tuna nia ya kukuza uchumi ni lazima tuangalie vitu hivi na sijui kama Mheshimiwa Mpango kwenye hili amewawekea *traffic* wapi maana wanaonekana nao wanafanya kazi ya kukusanya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu habari ya viwanda. Nimesikia kwamba hivi sasa mikoa inatakiwa kuwa na viwanda 100. Hivi ni viwanda vipi? Tunasema mtu akiwa na cherehani tano tayari ni kiwanda, *are we serious?* Tuna viwanda vingapi ambavyo vimekufa hivi sasa havieleweki? Mkoa wa Morogoro wenyewe una viwanda zaidi ya 20 *vime-collapse*, hakuna ajira, wengi wanafugia mbuzi hivi sasa. Viwanda vya Morogoro watu walichukua wakafanya kama *collateral* kwenda kuchukulia mikopo kufanya shughuli zao zingine lakini viwanda vimekufa. Kwa nini tusivitazame viwanda hivi ambavyo tayari vipo ambavyo vilanzishwa kwa nguvu ya Mwalimu Nyerere? (*Makofi*)

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa sana Wabunge wanapochangia wawe na uhakika na *data* wanazozitumia. Mheshimiwa Mbunge ameendelea kulalamika kwamba Serikali haifanyi kazi yoyote, anategemea viwanda vilivyoanzishwa na Mwalimu Nyerere na anatoa mfano wa Morogoro vingeweza kuwa vimefuliwa na vinaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa kwamba Serikali yetu, Serikali siku imeshaanza kutekeleza jambo hilo na yeye kama Mbunge wa Mkoa wa Morogoro hawatendei haki wananchi wa Morogoro kama *ha-support* nguvu za Serikali ambazo tumezifanya katika mambo yafuatayo:-

(i) Kiwanda kilichokuwa kinatengeneza maturubai, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeshamaliza utaratibu wa kimfumo na kimkakati wa kukifufua kiwanda kile na kuhakikisha wananchi wa Morogoro wanapata ajira. (*Makof!*)

(ii) Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika Mkoa wa Morogoro imeshaanzisha mradi mkubwa wa kufufua Kiwanda cha Sukari kwenye Gereza la Mbigili na inaanzisha kiwanda kingine kikubwa cha sukari eneo la Mkulazi na huo ni Mkoa wa Morogoro. (*Makof!*)

(iii) Kwa kushirikiana na wawekezaji katika Mkoa wa Morogoro Mheshimiwa Waziri Mkuu ameenda kukagua kiwanda kipywa kikubwa sana ambacho kitakuwa kinatengeneza sigara za kuuzwa nje ya nchi ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge wakati mwagine wanapochangia wawe wanajua pia na juhudzi za Serikali zilizofanywa. Hatukatazi watusaidie kutushauri lakini *wa-appreciate* pia juhudzi za Serikali zilizofanyika. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa taarifa?

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa siikubali. Mimi nilifikiri angenieleza kwamba tayari viwanda vimeanza kufanya kazi. Hizi hadithi anazosema tumeanza kuzisikia siku nyingi tu. Kusema leo tutafufua, kesho tutafufua, watu wa Morogoro tulishazoea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie kwenye sekta ya utalii. *World Bank* wanatuambia sekta ya utalii ikisimamiwa ipasavyo ina uwezo kabisa wa ku-cover budget yetu kwa mwaka. Hivi sasa tunajiliza pamoja na vivutio tulivyonavyo, hifadhi tulizonazo lakini bado hakuna kitu ambacho tunaona kama vile tunafanya kwa malengo ya kuhakikisha sekta hii inanyanyuka na inachukua nafasi kusaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hoja zinazoendelea hivi sasa tunataka kuona Waziri anasimamia pale kwenye sekta ya utalii kutoa ushauri na kuangalia tufanyakaje tuende mbele badala yake sasa Waziri anayepata nafasi yeye ana kazi ya kuangalia aliyetoka alifanya nini na vijembe. Aje na mkakati kwamba yeye atafanya nini kutupeleka wapi ili sekta hii itusaidie, si kufufua makaburi Mawaziri wengine wamefanya kitu gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna mahali ambapo tumekosea, ni lazima tuwe na mipango mikakati ambayo itatusaidia ili sekta hii ya Maliasili na utalii iende kuwasaidia Watanzania kama vile...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumpa Taarifa mzungumzaji kwa maneno aliyoongea kuhusiana na Waziri anapiga vijembe. Mimi niko kwenye Kamati ya Maliasili na ni Mjumbe mwenzangu, mambo yanayofanywa na Waziri huyu aliyeeteuliwa sasa yanaungwa

mkono na Watanzania wengi, kwa hiyo, tusikatishane tamaa badala ya kupongezana tunaanza kupigana vijembe humu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla aendelee kufukua makaburi ili tuwakamate hawa walotutesa muda mrefu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Devotha, taarifa?

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu naye ni Mjumbe mwenzangu kwenye Kamati mimi ninashangaa sana kwenye Kamati anasema vile huku leo anasema hivi. Yeye juzi hapa amesema Mheshimiwa Kigawangalla akae vizuri vinginevyo atatumbuliwa kama Mheshimiwa Maghembe au siyo, sasa sasa hivi anatupa taarifa ipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumza kukuza uchumi bila kuangalia jinsi ya kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja. Ukiangalia hali ilivyo hivi sasa huwezi kuwatoa watu ambaao ni matajiri wanaoishi kama malaika useme waishi kama mashetani, haiwezekani, hivi vitu vyote vinategemeana. Sasa ifike mahali watu waangalie sekta binafsi zinafanya nini na Serikali ione ni jinsi gani ya kusaidia sekta hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunaona hasara ambazo zinapatikana kwa hivi sasa kwenye sekta nyingi. Kwa mfano, *Club Bilicanas* iliyokuwa inamiliikiwa na Mheshimiwa Mwenyekiti Mboge ilivunjwa kwa jazba na kadhalika lakini hivi sasa *clubile magari yana-park*; kulikuwa kuna migahawa, kuna Gazeti la Tanzania Daima, watu wangapi wamepoteza ajira? Wafanyakazi wangapi walikuwa wanategemea pale kuishi maisha yao? Leo hii kweli, *taxi* ndiyo zina-park pale? Hatuwezi kujenga uchumi kwa kuumiza watu. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji anayezungumzia habari ya Bilicanas kuvunjwa. Bilicanas ile ilivunjwa na Serikali baada ya Mwenyekiti wao kushindwa kulipa deni kubwa alilokuwa akidaiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ilichukuliwa na alishindwa kesi ambayo mwenyewe alikuwa ameifungua. Kwa hiyo, ilivunjwa ili kumuondoa na mpango wa Serikali ni kupaendeleza pale kulingana na *Master Plan* ya Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Devotha, taarifa?

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuulize Waziri, sasa baada ya kuvunja ndio Serikali imelipwa hilo deni? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi hauwezi kujengwa kwa uonezi. Tunafahamu aliyekuwa *DC* wa Hai ambaye alienda kwa jazba kuvunja mashamba ya Mwenyekiti Mheshimiwa Mbobe na baadaye akawa *promoted/kwenda* kuwa *RC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbobe alikuwa anafanya kilimo cha *green house* lakini sasa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi niulize kilimo cha *green house* kina *conserve mazingira* lakini watu wa Kagera wanaolima kwa jembe wameambiwa walime mpaka mtoni hawaharibu mazingira. (*Makofi*)

Kilimo cha *green house* ambacho kinatumia *water drip*, ni maji kidogo sana, lakini matokeo yake ni...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

WABUNGE FULANI: Ahaaaa, bado Mheshimiwa, hajamaliza dakika zake.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, ngojeni. Mheshimiwa Devotha hebu kaa. Ulianza *exactly* na dakika 10, sasa hivi umetumia dakika...

WABUNGE FULANI: Kulikuwa na taarifa.

MWENYEKITI: Sasa si dakika saba na nusu za kwako za halali na dakika saba na nusu za taarifa.

WABUNGE FULANI: Hapana.

MWENYEKITI: Hapana nini sasa? (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Matiko, ajiandae Mheshimiwa Kapufi.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa sababu muda ni mchache mengi nitawakilisha kwa maandishi lakini kwa uchache huu niende kuzungumzia baadhi ya mambo kwenye Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea ukurasa wa 40 kipengele cha kwanza kabisa kimeainisha misingi na matarajio ya ukuaji wa uchumi. Kwenye kipengele cha kwanza kinasema kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na utengamano wa jamii ndani na pia nchi za jirani. Nafikiri hapa ingetakiwa ibadilishwe iandikwe kuimariswa kwa amani, usalama, utulivu na mambo mengine kwa sababu sasa hivi ilivyo huwezi kusema kwamba Tanzania tuna usalama ilhalii tukishuhudia wananchi wanatekwa, wanauawa, wengine viongozi wakubwa kabisa wanapigwa risasi nyumbani sehemu ambayo ni *secured*. Hatuwezi kusema

kwamba tuna amani ilhali maisha ya Watanzania ni magumu sana. Wale wote ambao mfano wametolewa kwa vyeti *fake* na wale wengine wameambiwa ni darasa la saba hawajapewa *pension, gratuity* ya kuondoka leo useme kwamba kuna amani Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeshuhudia na Mheshimiwa Msigwa ameomba Mwongozo hapa nchi jirani Kenya kwa yale ambayo yamejiri kwenye kuchomwa kwa vifaranga, ng'ombe kukamatwa na mambo mengine. Kwa hiyo, kipengele namba moja ukibadilishe kiseme, kutakuwepo na matarajio ya ukuaji wa uchumi iwapo kutaimarishwa amani, utulivu, usalama na mambo mengine lakini sio kwamba kuendelea kuwepo ilhali hivyo vitu hatuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine siku zote nasema hatuna uhalisia kwenye mipango yetu na bajeti ambazo tunazileta hapa. Tusipokuwa na uhalisia ni dhahiri hatutafika pale ambapo tunataka kufika kama nchi. Leo ukiangalia kwenye kitabu chako mwenyewe umeainisha bajeti ya maendeleo ya mwaka 2016/2017 ambayo ilikuwa ni shilingi trillioni 11.8 ilitekelezwa kwa asilimia 55 tu. Hii ya sasa hivi kwa *quartermoja* ya mwaka 2017/2018 imetekelezwa kwa asilimia 11, *on average* mpaka tunamaliza itakuwa asilimia 44 mpaka 50 au ikienda au ikienda zaidi tuseme 60. Sasa ikienda na *trend* hii ina maana tunapanga vitu bila kuangalia uhalisia, *time frame*, vipaumbele ni vipi, mwisho wa siku tunakuwa tunapoteza rasilimali za wananchi kukaa hapa tunajadili. Siku zote nashauri kwamba ni bora tuweke vitu ambavyo tunajua tutavifikasi ndani ya muda kwa *resources* tulizonazo walau tunapokuwa tumekuja *ku-discuss* Mpango mnatuambia kwa mwaka uliopita tumeweza kufanya mambo ya maendeleo kwa asilimia 80 au hata 85, 90 sio kwa asilimia 44 au 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine na hiki naomba kabisa tuwe *sober* kwa nachoenda kukiongelea sasa hivi. Kwenye *allocation* ya kodi za wananchi, maana imechukua *discussion* nyingi hapa na watu wamekuwa na hisia tofauti.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mimi natokea Kanda ya Ziwa lakini hili nalipinga na nalipinga *with facts* na sisi kama wawakilishi wa wananchi ambao tumetumwa hapa Bungeni tukalitafakari ili tuweze kuishauri Serikali vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaambiwa ujenzi wa jengo la *TRA* Chato, ghorofa kubwa sana limejengwa kule. Leo tuijulize Chato kuna mzunguko gani mkubwa wa fedha, kuna biashara gani kubwa kule Chato mpaka twende tuwekeze ghorofa? Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inakusanya mapato gani kule Chato tukawekeze lile ghorofa la mamilioni ya kodi za Watanzania? Tutafakari kama Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni Uwanja wa Ndege wa Chato, kabisa. Mimi sipingi uwanja wa ndege kujengwa Chato lakini Uwanja wa Ndege wa Chato ultakiwa kuwa ni chini ya kilometra moja ya *run way*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pamoja na kwamba kuna kukiukwa kwa Sheria ya Fedha za Umma ambayo tulipitisha hapa shilingi bilioni mbili, lakini naambiwa zimetumika zaidi ya shilingi bilioni 39, hiyo ni hoja lakini sio hoja kubwa sana kwangu, tuijulize sisi Watanzania na hawa ambao wanamshauri Rais...

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Matiko ni Mchumi mzuri....

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kanuni?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Sina muda wa kupoteza Mheshimiwa Msigwa, Kanuni najua...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Sina muda wa kupoteza kuisoma hiyo Kanuni, tunawapotezea muda wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimkiwa Matiko ni Mchumi mzuri na nataka tu kumpeleka kwenye hicho Kipengele anachosema kwamba hataki kuzungumzia sana lakini anam-*accuse* Waziri wa Fedha kwamba Sheria ya Fedha imevunjwa. Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Esther Matiko Sheria ya Bajeti (*Budget Act*) Na.11 ya mwaka 2015, akienda kusoma kifungu cha 41 pamoja na Kanuni ya 28(1) na (2), Waziri amepewa mamlaka ya kufanya uhamisho usiozidi asilimia tano ya bajeti yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kulisema hili kwa sababu naona Wabunge wanalichukulia jambo hili kama ni kosa kubwa liliofanywa kwa nia fulani lakini *Budget Act*, kifungu cha 41, narudia kusema, Sheria ya Bajeti kifungu cha 41 kimempa mamlaka Waziri wa Fedha kufanya mabadiliko hayo. Sasa nataka kujiuliza hiyo shilingi bilioni 39 inayosemwa, je, inazidi kweli hiyo asilimia tano?

Naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Esther kwamba anataka kupotosha maana ya sheria na mamlaka aliyopewa Waziri wa Fedha. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther kwanza kaa.

Waheshimiwa Wabunge, mipango ya Serikali kuna *strategies* nyingi sana. Kuna *strategy* za usalama, majeshi, *rapid deployment* ya forces. Maeneo yale yakivamiwa lazima kuwe na uwanja wa kuweza kubeba ndege kubwa za jeshi ambazo tunazo za kupeleka majeshi. Tuna uwanja mkubwa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mtware, tuluijenga kwa madhumuni mawili, ulinzi wa Kusini na kupeleka mafuta Zambia, hizi ni *strategy* za Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Matiko endelea.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi nicheke kidogo. Wakati tunapitisha na kwenye kitabu chake cha Mpango wakati ule tunapitisha kwa ajili ya upembuzi yakinifu zile shilingi bilioni mbili walisema ule uwanja wa Chato unajengwa kwa ajili ya usafiri ndani ya Geita na mikoa jirani hawakusema *otherwise*.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilinde, kingine nasema kuhusiana na...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Taarifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Muda wangu muulinde maana bado.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, dada yangu, anayetoka Kanda ya Ziwa, amezungumza kuhusiana na ghorofa iliyojengwa kwa ajili ya *TRA* pale Chato. Sasa nilitaka kumuuliza ni kanuni ipi au ni sheria gani kwenye nchi hii inayosema ofisi mpya za *TRA* zinazojengwa huko mkoani tujenge *slope*? Ni sheria gani anayotaka kuitumia kwamba kujengwa ghorofa Chato la *TRA* ni makosa Chato tuwajengee *slope*?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko, Taarifa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu hajatoa taarifa ameuliza swali, nitamjibu kesho wakati wa kipindi cha maswali na majibu kama Waziri Kivuli wa eneo husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* hapa ipo nimejibu kwamba wakati inakuwa *allocated* hapa ilikuwa ni uwanja kwa ajili ya usafiri ndani ya Geita na mikoa jirani. Hawakusema kwamba kwa ulinzi, usalama na mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa Mheshimiwa Jenista, ilikuwa ni shilingi bilioni mbili, ukiongeza shilingi bilioni 39 inakuwa ni shilingi bilioni 41, sijui ni sheria ipi hiyo? Pia *reallocation* yake tunataka tujue imekuwa *reallocated* kutoka kwenye kifungu kipi kuja kwenye hizo shilingi bilioni 39? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nimesema kwangu *issue* siyo sheria zaidi, lakini unaenda kuwekeza huo uwanja mkubwa pale Chato wa *runway* zaidi ya kilometra tatu ni ndege gani inaenda kutua pale kubwa hivyo? Hiyo ni *misuse* ya hela za walipa kodi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajiuliza mara mbili, leo tunasema kwamba Serikali inahamia Dodoma, *of which I support 100%*; Makamu wa Rais anahamia Disemba, Mheshimiwa Rais tunaambiwa anahamia mwakani. Bunge la Kumi tulipitisha uwanja wa Msalato ujengwe mpaka leo haujajengwa, Rais akija hapa tunatarajia wakija wale Marais, *like Trump* akija hapa ana ndege ambayo ni *Boeing 737* itatua hapa Dodoma au itaenda kutua Chato? *Why don't we rethink* tukaja tukajenga kwenye uwanja wa Msalato maana itakuwa ni *double cost* kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanakuja Marais ambao wanatumia ndege kubwa, Rais Magufuli anaondoka Dodoma kwenda kuwapokea Dar es Salaam maana haka ka-uwanja ka-Dodoma hakawezi kuwapokea. Kwa nini hizo hela tusingeweza kujenga hapa Msalato, kule Chato

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

tumjengee uwanja wa kuweza kutua ndege ya kawaida *like Precision, Bombadier* na ndege ya Serikali kuliko kujenga uwanja mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu kubwa au basi kama tunataka tuijenge Chato tungeweza kujenga hospitali kubwa kabisa ku-save maisha ya Watanzania kuliko *ku-sink shilingi* bilioni 39 kwenye uwanja ambao hautatumika au tungeweza kujenga Chuo Kikuu pale kama tunataka tuijenge ile Chato ikue vizuri, *unlike tulivyofanya sasa hivi.* (*Makofi*)

TAARIFA

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, muda wetu ni mchache sana.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie watulie watajibu baadaye.

MWENYEKITI: Bado tuna wachangiaji wengi, kwa maana hiyo, kuna watu watakosa kuchangia hapa sasa. Haya Mheshimiwa Innocent.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Esther Matiko kwamba ukiangalia *geopolitics* za *East Africa* na nchi za *Great Lakes*, kujenga uwanja Chato uko *strategically located*. Ukiangalia upande wa Ngara kuna *deposit* kubwa za *nikel* ambapo katika Bara la Afrika hamna *deposit* kubwa kama iliyopo pale Ngara. Isaka kuna *dry port*, Serikali inajenga reli kwenda Kigoma na Mwanza lakini pia kwenda Rwanda. Kwa hiyo, kwa upande wa miundombinu kujenga uwanja Chato ni kuweka miundombinu ambayo inashabihiana katika kukuza uchumi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Matiko hebu kaa kidogo. Mheshimiwa Mwinyi, wewe ni rubani mzoefu sana na mimi ni *ex-engineer* wa ndege. Uwanja wa Dodoma, hebu tueleze kwa uzoefu wako *3,000 metres Boeing 757* inatua au haitui?

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli haiwezi kutua, haitui. (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Sawa, lakini Trump akija haji na ndege anakuja na *Helicopter One*. Haya, Mheshimiwa Matiko. (*Makofii*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Innocent pale, mtani wangu, kwanza taarifa yake siipokei lakini pili, ngoja nimsamehe nilikuwa nampa dongo moja ila nimsamehe, niendelee kuchangia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Innocent nilimuona juzi wakati Rais amezuru kule, anapiga magoti kumuomba shilingi bilioni 30 za maji. Wajibu wako kama Mbunge ni kuisimamia Serikali hela za walipa kodi zije zifanye kazi kule, *not to kneel down before the President* ili uweze kuletewa mradi wa maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, Chato bado, tumeona ujenzi wa *traffic lights* pale Chato, nikaijuliza hawa watu wanamuogopa Magufuli kwa nini wasimshauri vilivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini dhima kubwa ya hili, ukiangalia kuna miji mingi na ina *high congestion* ya magari leo mmeenda kujenga Chato na kuna picha niliona sitaki kuamini kama kweli ni ya kule lakini nilivyopita mimi Chato sikuona kama kuna *congestion* kubwa ya magari mnaweka *traffic lights* Chato, wanapita punda. *Misuse of funds* za walipa kodi wa Tanzania wakati tuna majengo ya shule hajajengwa, hospitali nydingi zinakosekana wamama wajawazito wanafariki hakuna huduma *proper*, mnaenda kujenga *traffic lights* za Chato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndiyo *the only way* kwa kauli mbiu ya Tanzania ya viwanda kama ingeenda vizuri, tungewekeza kwenye kilimo tungeweza kufikia hii ndoto ya Tanzania ya viwanda. Ukiangalia bajeti ya ruzuku ya mbolea na mbegu ya mwaka 2015/2016 tuliweza *ku-allocate* kwa kaya zaidi ya 900,000 lakini ukija 2016/2017 tume-*allocate* ruzuku ya mbolea na mbegu kwa kaya 370,000 tu. Leo tunasema tunaleta ukombozi kwa hawa Watanzania halafu wakilima wanataka kuuza mazao yao, mnawazuia badala ya kuwatafuta masoko. Mwaka 2015 kahawa Tarime ilikuwa inauzwa shilingi 2,000 kwa kilo leo ni shilingi 600 halafu tunasema nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango na watu wako wanaokushauri naomba ukae uangalie vizuri ni jinsi gani tunaweza ku-*move* na haya ambayo tunakupa hapa kama Wabunge myafanyie kazi ili Tanzania tunayoitaka iweze kufikiwa. Nina imani kabisa kwa vivutio ambavyo Tanzania tumepewa, tungewekeza kwenye utalii kwa nchi hii tusingekuwa wategemezi tungeweza kujitosheleza kabisa. Tuna vivutio vingi vya kitalii ambavyo vingi havipatikani hata kwenye mataifa mengine lakini tume-*underutilize*, kwa nini? Ni kwa sababu *priority* zetu zinaenda kwa kinyume, *we are thinking backward*. Leo *TTB* ingepewa fedha za kutosha ingeweza kutangaza utalii wetu.

MWENYEKITI: Nimekuongeza dakika mbili zile za misukosuko. (*Kicheko*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Ooh! Nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeweza kuiwezesha *TTB* kupitia *Tourist Development Levy* tukapeleka fedha nyingi ili sasa waweze kuvitangaza vivutio vyetu na kufanya wajibu wao kama inavyotakiwa. Leo unakuta *TTB* wakiomba fedha ili waweze kujidesha wanapata chini ya asilimia 30, tunashindwa kuvitangaza vivutio vyetu. Ukiangalia tuna *beaches* nyingi sana, kuna nchi zingine zinajidesha kwa vivutio vya utalii walivyonyavyo ambavyo ni vichache

ukilinganisha na Tanzania. Sisi Tanzania aliyeturoga nadhani alishafariki, tulishapewa laana ambayo haifutiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukae tujitafakari sisi kama Wabunge wa Bunge la Kumi na Moja tukiondoka tutakuwa tumeisaidia vipi nchi yetu. Ni wengi humu wanasafiri nchi mbalimbali ikiwemo Mawaziri, mnaposafiri huko mnajifunza nini ambacho mnakileta Tanzania ili tuweze kukitumia kuhakikisha kwamba nchi yetu ina-move? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Taifa. Nazungumzia deni la ndani, kuna wakandarasi ambao wanaidai Serikali...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi na ajiandae Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi nianze kuchangia Mpango huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni eneo la kilimo. Mimi eneo la kilimo naomba niliweke katika sura zaifuatazo. Namwomba Mheshimiwa Waziri mipango yetu na kama ambavyo mmeeleza hapo iendelee kujikita katika kuzingatia tafiti mbalimbali. Nalisema hilo kwa sababugani?

Leo hii isitokezee kwamba kwa sababu korosho ina bei kubwa basi kila mtu akatamani kulima korosho, twende kwa tafiti. Kwa misingi hiyo kama ambavyo nimeendelea kusema hapo kwa kupitia tafiti tunaweza tukafahamu ni kanda zippi zinfaaa kitu gani na isitokezee tu kwamba kwa sababu leo pamba ina bei nzuri basi kila mmoja akataka kulima pamba, naomba mipango ituelekeze huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, eneo hilo hilo la kilimo upande wa mahindi ambao kila mmoja amezungumzia hapa, mimi nitatoa mfano na wanasesma

kama huna vielelezo, haujafanya utafiti usiongee, naomba niongee kwa vielelezo na kwa utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nililima maharage lakini baada ya kulima maharage nikafanya maoteo kwamba mahindi yatanipatia pesa nzuri, kwa hiyo, nikabilisha maharage kununua mahindi. Ni mkulima mimi niliyelima maharage, lakini nikanunua mahindi, nikayahifadhi kwa maana nipate fedha nzuri kwa maana ya maoteo. Leo hii nisipopewa nafasi ya kuuza mahindi yangu, sitokuwa na nafasi ya kulima tena hata maharage, nitakuwa nimekatwa miguu.

Kwa hiyo, naomba sana katika maeneo hayo, wale wote ambao wamelima mahindi wapewe nafasi vinginevyo tutakwenda kutengeneza mazingira ya watu hao kutoweza kusimama kwa miguu yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba nusu ya 2017 kilimo kilichangia kutoka asilimia 2.7 mpaka 3.1, umuhimu wa kilimo uko pale pale. Nafahamu kwamba kwa kupitia kilimo ni sehemu kubwa ambayo inaa jiri Watanzania walio wengi, lakini mipango iendelee kutusaidia. Kilimo hiki ambacho ni cha kijungujiko (*hand to mouth*) sort of economy, tunatakiwa tutoke huko. Haiwezekani ikawa Watanzania wengi wako kwenye kilimo lakini mwisho wa siku kilimo hiki kisifanye watu tujitegemee. Ni bora hata wachache wakalima lakini wakalima kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala la afya. Nilishauri mara ya mwisho, ni kweli nimeona hospitali kama ya Muhimbili na Bugando tunaendelea kuzipa vifaa tiba na kuongeza vifaa mbalimbali. Ushauri wangu unabaki pale pale, tuna mipango ya kuboresha Hospitali za Mikoa, mimi binafsi natoka Mkoa wa Katavi, tukiboresha Hospitali za Mikoa tunapunguza msongamano wa watu kwenye Hospitali hizo za Bugando, Muhimbili na kwingineko. Kwa hiyo, niliombe sana hilo tuendelee kufanyia kazi kwa maana ya kuboresha maeneo haya ya chini. Ukiniboreshea mimi Katavi, ukimboreshea wa Kigoma na wa Tabora

tutapunguza watu kutegemea maeneo hayo. Eneo la afya naomba nitoke kwa sura hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la maji. Itakuwa ni kichekesho, mara ya mwisho nilizungumza hapa pia nikasema nchi hii tuna uwezo wa kufanya muunganiko wa maji kuwa kama *design* ya buibui. Mtu wa Nyasa akiunganishwa kupitia Ziwa Nyasa na Viktoria wakiunganishwa kupitia Ziwa Viktoria, Tanganyika tukiunganishwa kwa kupitia Ziwa Tanganyika, nchi hii itakuwa na mtandao wa mabomba ya maji. Hatuna sababu ya kwenda kwenye vyanzo ambavyo siyo vyta uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo hii katika Mkao wa Katavi tunazungumzia habari ya Bwawa la Milala na chanzo kingine cha Ikorongo wakati Ziwa Tanganyika lipo kilometa 120 kufika Manispaa ya Mpanda. Miradi mingine tunayolona ya kutoa maji VI-ictoria iwe ni dira kwenye maeneo mengine. Hatuna sababu, nimesema kwingineko duniani watu wanabadilisha mpaka maji ya bahari kuwa maji safi ya kunywa, sisi hatutakiwi kufika huko kwa sababu vyanzo vingine vyta maji safi, baridi ya kutumia tunavyo, ni mipango tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la misitu, naomba eneo hili nilizungumze kwa kina. Leo tunazungumzia miradi mbalimbali, tukizungumzia hata suala la *Stiegler's Gorge* na kwingineko. Nilifarijika sana mtaalam mmoja majuzi katika semina ile tulipokuwa tunazungumzia suala la Sera ya Taifa ya Misitu alipotuambia pasipo misitu hata suala la umeme tunaouhitaji hautokuwepo, habari ya *Stiegler's Gorge* na kwingineko kwa sababu maji hayatapatikana. Hata tukizungumzia suala la utalii, lina uhusiano wa moja kwa moja na misitu kwa sababu kwa kupitia misitu kuna *biodiversity* ambayo hiyo moja kwa moja inakwenda na masuala ya *ecosystem*, tukikosea hapo iko shida kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye mipango yetu tuendelee

kuboresha suala hilo la misitu. Leo mkizungumzia mipango yote, yawe ni mabwawa ama vitu vingine bila kujikita kwenye kuhifadhi misitu, tatizo ni kubwa, umeme hatutokuwa nao na wakati mwingine hata kilimo pia itakuwa shida na eneo hili naomba tuendelee kupewa elimu pana. Wakati mwingine ukiona miti imetunzwa sehemu, sio kwa sababu anatakiwa mnyama awe pale, ni kwa ajili ya kutengeneza *biodiversity* pamoja na *ecosystem* ambayo ina nafasi kubwa kwenye kumsaidia binadamu. (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha, chama kimeleta maelekezo na ninyi mtapunguziwa muda kwa kuongeza wachangiaji. Kwa hiyo, muda wako umekwisha lakini nikupongeze kwa mchango mzuri na umewatendea haki wana Jimbo kwa mchango mzuri, ahsante. Mheshimiwa Mwalongo, ajiandae Mheshimiwa Mwambalaswa. (*Makofii*)

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Mpango huu wa maandalizi ya maendeleo wa mwaka 2018/2019.

Pia nitakuwa ni mchache wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kuiendesha na kuisimamia nchi yetu. Sisi Wana-Njombe kwa maana ya Jimbo la Njombe tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwamba tumepata mafanikio makubwa katika kipindi chake, tunajengewa kituo cha kisasa kabisa cha afya katika Kijiji cha Ihalula chenye thamani ya shilingi milioni 500, tunajengewa soko la kisasa katika Mji wa Njombe lenye zaidi ya shilingi bilioni nne lakini pia tunajengewa stendi ya kisasa kabisa katika Mji wetu wa Njombe. (*Makofii*)

Kwa hiyo, hayo ni mafanikio mazuri na nampongeza sana Mheshimiwa Rais na tunamshukuru sana kwa kutupatia hizo fedha za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na kuchangia Mpango wa Maendeleo ambao upo mbele yetu, sisi Njombe tunaitwa Njombe Mjini, lakini ni wakulima, kwanza kabisa nianze na suala la wakulima. Watu wengi wameongelea suala la mahindi, ni kweli kabisa suala la mahindi kiuchumi, mfumuko wa bei katika nchi yetu unashikiliwa na mahindi. Kama Serikali inalionna hilo na inataka kweli wananchi hawa wanaolima mahindi waweze kunufaika na kilimo, lakini vilevile waisaidie Serikali kuweza kushikilia mfumuko wa bei basi ihakikishe kwamba Serikali inawekeza vizuri kwa wakulima kwa maana ya kuwapa pembejeo, wataalam wa ugani na mbegu zilizo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Njombe kuna Kituo cha Usimamizi wa Mbegu Bora, kituo kile kina wataalam wachache, kina gari moja linatumika Kanda nzima kwa ajili ya udhibiti wa mbegu. Sasa hawa wakulima wanaolima mahindi na kile kituo ndio kinadhibiti mbegu za aina zote za mpunga, mahindi na kahawa, kwa kweli inaonekana kwamba tunafanya tu kwa sababu sheria imesema, lakini nia ya dhati ya kusaidia wakulima inaonekana haipo, wakulima wanauziwa mbegu *fake*, wanaletewa mbolea zisizofaa na kadhalika. Niombe sana tuimarishe huduma kwa wakulima wakati tunatambua kabisa kwamba mahindi ndiyo yanayoshikilia shilingi ya Tanzania iweze kuwa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwa suala la wakulima, lipo zao la viazi Njombe ambapo vinadhurika sana. Viazi tunalima Mkoa wa Njombe lakini vilevile Mkoa wa Mbeya, Tanga na Kilimanjaro. Viazi vyta Tanzania vinaathiriwa sana na viazi kutoka nje hasa katika ujazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niombe sasa Serikali kupitia Idara ya Vipimo tutengeneze mifuko maalum kwa ajili ya zao la viazi. Mazao mengine kama kahawa na korosho yana magunia na viazi tuwekwe mifuko maalum ya viazi ambapo unajua kabisa piga ua mfuko huu hauzidi kilo 90 na huo ndio mfuko wa viazi, ye yeyote atayekutwa sokoni na mfuko tofauti na ile maana yake huyo awe ni mhalifu, itakuwa imeasaidia sana wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo zao la parachichi katika Jimbo langu la Njombe Mjini, parachichi za Njombe ni za *export*. Mwaka huu tume-*export* tani 700 lakini kwa bahati mbaya sana tuna-*export* kwenda nchi jirani na wale wa nchi jirani ndio wanapeleka Ulaya. Niombe sasa Serikali itusaidie, wakulima hawa wa parachichi kwanza kabisa wapatiwe mbegu bora, lakini pia tupate wataalam kutoka Serikalini kwa sababu parachichi hizi ni za *export* maana yake tayari zitatusaidia kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba tatizo kubwa la parachichi ni kwamba hatuna *pack house*. Katika Halmashauri yetu tuna *pack house* moja tu na hawa wanaokuja kutoka nchi za nje kuchukua parachichi wanakuja na magari yao maalum yenyе ubaridi. Kwa hiyo, Serikali ione kwamba kuna nafasi ya kuwekeza kwenye miundombinu ya ubaridi ili kusudi wananchi wanaolima parachichi waweze kupata mahali maalum pa kutunzia hizi parachichi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kutokana na mfumuko wa kilimo hiki, wananchi wengi wameitikia sana na parachichi zinaendelea kuongezeka. Itusaidie kwamba sasa parachichi ziwe *exported* kutoka Njombe kwenda masoko ya nje Ulaya na kadhalika lakini tukipeleka Kenya maana yake wanatulipa *Tanzanian shillings* halafu wao ndio wanapata dola na sisi hapa tuna shida kubwa sana ya dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambao napenda kiliongelea ni umeme. Upo umeme wa *REA* Awamu ya Tatu lakini vilevile lipo suala la *TANESCO*. *TANESCO* ndio wanaweka umeme katika maeneo ya mijini pale Njombe tuna vijiji vilivyo karibu na mji kilometra tano kama Itulike havina umeme na havina umeme kwa sababu havimo kwenye *REA*, lakini vilevile vinatakiwa viwe *TANESCO* na uwezo wa *TANESCO* wa kupeleka umeme uko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwenye bajeti itakayoandaliwa tuone *TANESCO* wanavyopewa miradi ya mijini angalau wapewe miradi unayokwenda mpaka

kilometra tano, wanapewa mita 700, 600 au 300. Sasa utaona vijiji vilivyo karibu na mji havipati umeme, kwa hiyo, niombe sana hilo liangaliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufanikiwa kiuchumi tunahitaji barabara nzuri. Katika Jimbo langu la Njombe Mjini iko barabara inayoenda Ludewa inaitwa barabara ya Itoni – Manda. Awamu zote za uongozi zimekuwa zikiisemea barabara hii iwekwe lami, lakini mpaka leo katika Jimbo langu kazi hii ya kuweka lami haijaanza. Niombe sana katika Mpango ujao basi litekelezwe hili kwa sababu barabara hii inasaidia wananchi kusafirisha mazao ya kilimo lakini inasaidia vilevile huduma mbalimbali kwa Wilaya ya Ludewa na kuendelea mpaka Ziwa Nyasa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu, tunahamasisha viwanda lakini tusipowapa elimu watu wetu hapa tunarudisha umanamba. Vijana hawa wataingia kwenye viwanda hivi watafanya kazi ya kupanga vitu kwenye maboksi na hatutajivunia kwamba vijana wetu wamepata ajira, itakuwa wamepata ajira lakini watakuwa wamepata ajira ya kijungujiko na yenye manung' uniko. Watakuwa watu wa kuhangaika tu kukunja mashati kuweka kwenye mifuko, tuwape elimu vizuri ya ufundi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu ya ufundi ambayo tunapaswa kuwapa vijana hawa iko elimu inaitwa *industrial maintenance*. Katika *industrial maintenance* vijana watajifunza mambo yanayohusiana na marekebisho ya mitambo mbalimbali ndani ya viwanda. Leo hii *VETA* mtaala wanaotumia kufundisha, wanafundisha watu kutengeneza vigae vyta moto wa mkaa, ndiyo ataenda kufanya kazi kiwandani huyo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, Jimboni wamekusikia unavyowatetea. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwambalaswa kwa dakika saba.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Fedha na Mpango, Naibu Waziri na wataalam wote kwa kazi nzuri. Nia ya kuuleta Mpango hapa Bungeni ni kuujadili na kuuboresha ikiwezekana, kwa hiyo, sidhani kama kuna Mbunge ye yote ambaye anaudhihaki na kuukejeli, kazi yetu ni kuuboresha na kuujadili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Mbunge mwenzangu ambaye hajui tunu za Tanzania nataka nirudie mimi. Tunu za Tanzania ya kwanza ni lugha yetu ya Kiswahili, ya pili Muungano wetu, ya tatu ni utu na udugu wetu na ya nne ni amani na utilivu. Hizi tunu hazikuja Tanzania kwa bahati mbaya, viongozi/waasisi wetu walitumia nguvu na resourcesnyingi sana kuzi-*inculcate*kwa Watanzania na ndiyo maana Tanzania imekuwa mfano wa kuigwa duniani kwa sababu ya hizo tunu nne. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zinapoanza kutokea kauli za kutugawa kwa majimbo na ukanda humu ndani zinasikitisha sana. Unajua sisi Wabunge ni viongozi na kiongozi kwenvye jamii yoyote watu unaowaongoza wanapenda kuiga lile unalosema na unalotenda. Kwa hiyo, tunayoyasema humu watu wetu kule wataiga. Naomba Bunge lako hizi tunu nne tuzilinde kwa nguvu zetu zote, ahsante sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kidogo Mpango aliouleta Mheshimiwa Mpango. Ameanza na miundombinu kwamba inasaidia kuchochaea maendeleo kwenvye nchi kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye umeme. Nimeona miradi mingi ya kuongeza uzalishaji wa umeme kwa sababu umeme ni *driver* kubwa ya kuchochaea maendeleo ya uchumi. *Stiegler's Gorge* itazalisha megawati 2,100 ikikamilika, na *source* kubwa ya maji ya mto unaokwenda kulisha *Stiegler's Gaugen*i Mto Ruaha. Ukiuona Mto Ruaha ulivyokuwa mwaka 2008 na ukiuona leo, inasikitisha.

Kwa hiyo, naiomba Serikali inapopanga kwenda kuweka mtambo wa kuzalisha umeme pale *Stiegler's Gorge* iweke mpango kabambe sana wa kufanya *conservation* ya *The Great Ruaha*, vinginevyo tutakuwa hatuna maji ya kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejaliwa kuwa na vyanzo vingi nya umeme, wengine wamesema asubuhi jotoardhi, juu, upopo, naomba Serikali iangalie kote huko ili tuweze kuwa na umeme mwingu wa kutosheleza viwanda vyetu na umeme mwingu wa *ku-export*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa China wameendelea mpaka kufika hapo walipo walikoanzia ni mbali sana. Kwanza walikuwa na *revolution* ya kilimo, lakini baadaye wakaona waanze viwanda vidogo vidogo, wakawapeleka vijana wao kwenda kusoma kokote kule nje kwa gharama yoyote na waliporudi kwa fani ile aliyosome, walikopeshwa fedha na vifaa waende kufanya hiyo shughuli ambayo walisomea; hao ndio wameanzisha viwanda ambavyo sasa hivi China ina mabilionea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hata sisi, juzi Mheshimiwa Rais alikuwa Kagera, Kiwanda cha *Kagera Sugar* kinafanya vizuri sana; kimeajiri vijana wa Kitanzania wanafanya kazi pale. Serikali inaweza ikafanya vivyo hivyo, ikawachukua vijana wa Kitanzania waliosoma, kama ni kilimo, iwawezeshe, iwakopeshe, iwape ardhi waanzie kule tuwe na mapinduzi ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye maji, wenzangu wengi wamesema, miaka mitano, sita ijayo maji yatakuwa ni *crisis* sana duniani. Naomba Serikali ianzishe Wakala wa Maji Vijijiini na Mijini kama ilivyo kwa Wakala wa Barabara, kama ilivyo kwa Wakala wa Umeme na kama ilivyo *TANROADS*. Ni muhimu sana Serikali ianzishe Wakala wa Maji Vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombinu ambayo nilikuwa nimesema, nije kwenye reli ya kati ya *SGR*,

reli ya Tanga kwenda mpaka Musoma, reli ya kutoka Mtwara kwenda mpaka Liganga, lakini reli ya *TAZARA* ni reli ambayo tayari ni *standard gauge*, inahitaji kuboreshwa tu na kuwekewa umeme. Naomba Serikali iangalie sana reli hii kwa sababu nayo itafungua nchi yetu kwa nchi ambazo zipo kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile reli hii itakuwa inapita kwenye *dry port* ambayo itaanza kujengwa pale Mbeya, kwa hiyo tunakuwa na *block trains* za kutoka Dar es Salaam kwenda Kigali na Bujumbura. Kutakuwa na *block trains* kutoka Dar es Salaam kwa reli ya *TAZARA* kwenda Mbeya, kwenda kuwasaidia wenzetu wa Zambia, wa Malawi na wa Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, tunu za Tanzania ni hizo nne nillzozisema, nimesema Muungano, Lugha ya Kiswahili, utu na udugu na amani na utulivu. Bunge lako lizienzi na kuzilinda tunu hizi kama mboni za macho yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKTI: Ahsante, Mheshimiwa Paresso unan dakika tano, Mheshimiwa Susan kwa dakika kumi.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika mpango huu uliowasilishwa na Serikali hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, napenda kushauri Serikali inapoleta mipango hasa kwenye miradi mikubwa, isiwe na miradi mikubwa mingi ambayo itagharimu fedha nyangi tena za mkopo, lakini matokeo yake inachukua muda mrefu. Ni vizuri mkawa na miradi michache, hata kama mtakopa lakini angalau iwe michache mwisho wa siku iweze kuwa na ufanisi. Kama ambavyo mmefanya hapa, kuna miradi mingi lakini ukiangalia hata mipango ya miaka miwili nyuma iliyopiata hivyo vivyo, mmekuwa na

miradi mingi sana ambayo hata leo ukifanyia tathmini nafikiri hakuna hata mmoja ambao tayari umeshaanza kuonesha matokeo, lakini tena mmekopa maana yake mnaendelea kuendeleza Deni la Taifa.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni bora muwe na miradi michache yenye matokeo ya haraka lakini itakayotumia fedha kidogo au hata kama ni nyigi lakini kwa ukopaji ambao utakuwa si wa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nichangie katika Sekta ya Utalii. Pato la Taifa asilimia 17.2 inachangiwa na Sekta ya Utalii. Maana yake ni kwamba asilimia 25 ya fedha za kigeni inatokana na utalii. Lakini ukiangalia hapo kwenye mpango ambao umewasilishwa na Serikali hamjatilia mkazo wa kutosha wa namna gani sekta hii ya utalii ambayo inaingiza kiwango kikubwa cha Pato la Taifa inawezeshwa ili kuhakikisha utalii huu ambao unaingizia fedha za kigeni nchi hii uweze kuendelea kwa kiwango kikubwa. Mfano, umesema hapa Mheshimiwa Waziri, kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na utalii. Maana yake ni kwamba mmekuwa mkizoea kuendeleza kuongeza kodi kwenye sekta ya utalii au kwa watu ambao wanafanya biashara ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tuliwashauri hapa wakati tunapitisha bajeti kwamba mfute baadhi ya kodi zilizopo kwenye utalii, hamkufuta, wenzetu wa Kenya wakafuta, sisi hapa tukaongeza. Maana yake ni kwamba unaendelea kufanya sekta ya utalii ni ghali sana hapa nchini, mwisho wa siku mzungu au mtalii ye yote atachagua kwenda kwenye eneo ambalo ni rahisi na ataona vile vitu ambavyo anavitaka, kwa hiyo mkiwa mnashauriwa, Waziri mpokee ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu anayewekeza kwenye hoteli za kitalii analipa kodi 46. Mheshimiwa Waziri ni vizuri sana muwe na kodi chache ili watu wengi waingie kwenye kuwekeza kwenye utalii ili tuendelee kupata wagoni

maana yake utalii utakuwa ni rahisi. Tulinshauri sana Mheshimiwa Profesa Maghembe kipindi hicho lakini hakusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi nyingine ni ya *TALA license*, unalipa dola 2,000 kwa magari matatu. Uwe na magari 100 unalipa dola 2,000. Ni kwa nini msifanye kodi hii ikalipwa kwa gari? Ukilipa kwa gari maana yake utawa-*encourage* watu wengi wawe na magari, utalii utakua, ushindani utakuwa mkubwa, biashara itakua. Unalipa dola 2,000, magari 100; wale *Leopard Tours Arusha*, makampuni makubwa wana magari 100 mpaka 200 lakini analipa dola 2,000. Kijana wa Kitanzania aliyepambana amepata hela ana magari matatu analipa dola 2,000, hii ni nini Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeishauri Serikali, tulimshauri sana Mheshimiwa Maghembe hapa hakusikia akaendelea kushukilia msimamo huo, nafikiri ni vizuri muangalie hilo. Lakini sekta hii ya utalii pia imeajiri vijana wengi ambao walikosa ajira lakini wameji-*engage* huku. Kwa hiyo, tunategemea kwamba jinsi ambavyo utalii utaongeza Pato la Taifa ndivyo ambavyo wawekezaji wataingia kwenye sekta hii, ndivyo ambavyo pia vijana wetu wengi watapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, Serikali ya Awamu ya Tano mliingia kwa nguvu kubwa sana mkaesema nchi hii ni nchi ya viwanda, Tanzania ya viwanda. Lakini siku hizi wimbo huu umeanza kupotea, sijui mnaendeleaje, hausemwi kwa nguvu ile ambayo mlanza nayo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matamko ya kutafuta kiki za kisiasa. Mheshimiwa Waziri jana wamezindua, wanasesma kila mkoa utajenga viwanda 100, maana yake mikoa 26 tunategemea kuwa na viwanda 2,600. Sasa hivi viwanda mnavyotamka, kwanza mtupe tafsiri yake, kwa sababu akija Waziri wa Viwanda anasema vyerehani vitatu kiwanda, akija mwingine anasema viwanda ni viwanda, mtupe tafsiri sahihi ya viwanda ni nini ili siku tunapowafanya tathmini ya hivyo viwanda ambavyo mmekuwa

mkiwaambia Watanzania tujue ni viwanda kweli au si viwanda. Kwa hiyo msitafute kutafuta *cheap* kiki za kisiasa kuwanufaisha Watanzania wakati sio sawasawa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Susan, dakika kumi.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kukubali ombi la Mheshimiwa Paresso ili aniachie dakika kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na maswali, yaani ni hivi, tunajadili hapa maswali yaulizwa Bungeni na Mheshimiwa Dkt. Mpango yupo na anajua swali gani likulizwa karibu Bunge zima linasimama. Lakini unapokuja kuweka mipango ili Watanzania wengi wanufaike unatuletea mipango ya kujenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndiyo *reflection* ya Waheshimiwa Wabunge kwamba wao wanataka reli ya Dodoma? Ni *reflection* ya Watanzania kwamba wao wanataka kiwanja cha ndege cha Chato? Ni kweli ni matakwa ya Waheshimiwa Wabunge, wao wanataka bombardier? Kwa nini mnatufanya namna hii? Kwa nini wakati Bunge watu wanauliza maswali katika mipango ya nchi hii huangalii ni nini watu wanataka ndani ya Tanzania, sisi ndio wawakilishi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasmama wengi kwenye maji, lakini leo unatuletea mipango ya maji ya vijiji totototo, wakati Tanzania tuna mito, tuna maziwa, tuna kila kitu. Kwa nini usituletee maji ya bomba, mpango ambao utaonekana mnakwenda kutega sasa maji katika milima, katika mito ambayo tutakuwa na kilimo cha umwagiliaji na maji yatatirika kila kijiji? Kwa nini mnakwenda kutuchokozea ardhi chini ili ituletee matetemeko ndani ya nchi ya Tanzania?

Kwani Mungu aliweka Mito hapa Tanzania alikosea nini? Naomba mipango inapokuja ndani ya maji usituletee mipango mingi ya visima. Tumia mito, maziwa ili tupate maji ya umwagiliaji na maji ya bomba salama na kunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata umeme huo. Umeme wa maji nasikia ni rahisi. Huko nyuma katika vitabu nilisikia sana wana mipango, kwa mfano kule Mlimba kuna mto mkubwa kabisa ambako unakwenda kumwaga maji mpaka huko Kilombero, mpaka Rufiji, huko kwenye *Stiegler's*, lakini kule mmekusahau kabisa. Milisema mtazalisha umeme kwenye Mto Mpanga, leo katika mipango yenu hakuna kitu, mmedandia *Stiegler's Gorge*. Nini? Tatizo liko wapi, kwa nini mnapanga mipango halafu mnaiachia njiani, kwa nini hammalizi? Kwa hiyo, mimi nilitegemea mipango iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye gesi, Watanzania wote walijua sasa gesi imepatikana, tukasifiwa hapa kwamba gesi sasa ndiyo mkombozi wa Watanzania, kila mmoja alijua baada ya miaka fulani gesi..., sasa hivi mimi niko kwenye Kamati ya Nishati na Madini; gesi sasa hivi ni kitendawili, na wakati ule Mheshimiwa Mnyika alikuwa Waziri Kivuli wa Nishati na Madini alisema leteni mikataba ya gesi hapa Bungeni, mikataba mnayosema tofauti na mliyoingia kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo utakuta eti Serikali imedhamini *Songas* imekwenda kuchukua hela huko halafu *Songas* hawana chochote. Mitambo ya *TPDC*, mitambo ya *TANESCO*, lakini *Songas* kamujiri tena huyo mbia *Pan African Energy*, halafu huyo huyo anaunasibu tena wa *TPDC*. Hela tumekopa Tanzania; kuna gesi hapa?; halafu Serikali ndiyo inakwenda kulipa ule mkopo. Ule mkopo haillipi Serikali, inalipa kwa Watanzania, wapigakura wetu. Nini ninyi? Haya mambo gani mnatuletea hapa? Hizi figisufigisu hapa za nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna matatizo makubwa ndani ya nchi yetu. Labda kama unashinikizwa,

maana tumuonee huruma na huyu jamaa. Hapa unaambiwa hii nchi hakijachakuliwa Chama cha Mapinduzi, amechaguliwa mtu mmoja, alichukua fomu peke yake, kwa hiyo hata ukiwa Waziri ukibisha tu imekula kwako. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan, nenda kwenye hoja, usitumie maneno ya dhihaka Kanuni zikakubana, nakuomba nenda kwenye hoja changia mchango wako ukimaliza kaa chini, tulia uende nyumbani.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa bwana, lakini Mheshimiwa Spika jana alisema tuseme tu tusiwe na wasiwasi, sasa wasi wasi wa nini Wabunge wa CCM, lakini na mimi mwenyewe si Mwenyekiti wangu kaniambia niseme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida za Watanzania kwa mfano kule Mlimba na maeneo mengine ni kuunganishwa barabara za mikoa na wilaya kwa sababu Watanzania wengi ni wakulima. Lakini leo Mheshimiwa Dkt. Mpango atuambie, katika mpango huu unaokuja, je, ni barabara ngapi nchini Tanzania zitakwenda kuanzishwa na kujengwa kwenye viwango vya lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasaidia nini? Inasaidia kwa sababu Watanzania wengi ni wakulima. Kwa hiyo, watapitisha mazao yao lakini itasaidia sana wanawake ambao wanajifungua katika mazingira magumu na Hospitali za Wilaya ziko mbali. Haki ya Mungu wanaokufa nchi hii ni vijijini. Kwa hiyo, barabara zitaokoa uchumi kwa wakulima, zitaokoa vifo vya akina mama na watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipata barabara inawezekana kabisa tutapunguza vifo vya akina mama kwa sababu sera ya Taifa kila kata kuwe kituo cha afya, kila kijiji zahanati. Hebu tuambie mpango madhubuti wa kutimiza sera ya Taifa kwamba kuna vijiji vingapi nchini Tanzania vina zahanati, kuna kata ngapi zina vituo vya afya na mpango wa Serikali ni nini katika kutatua haya matatizo. Hatuwezi kukubali wananchi wanakufa huko, hasa akina mama na

watoto. Tunaomba uje na huo mpango ili utuambie tupunguze vifo, tuokoe akina mama na watoto na tuokoe wakulima wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu mimi nilitegemea uje na mpango, kwa kuwa tayari tuna vituo vya JKT na hii tunasema kwenye nchi ya viwanda, ungekuja na mpango hapa kwamba JKT itachukua vijana iwe darasa la saba, iwe vyuo vikuu, watakwendu kufanya huko stadi mbalimbali na kufundishwa uzalendo halafu wakitoka huko wanakuwa na *package* ya kuwakopesha kwenda kutengeneza viwanda. Mngechukua hata wataalam kutoka China, na hiyo ilikuwa llani ya CHADEMA, tulisema JKT itakuwa si tena mabunduki tu, kutakuwa na mpango maalum vijana kwenda huko kujifunza mafunzo mbalimbali ili kwenda kuokoa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wa reli, mmechukua mkopo mnajenga reli mpaka Dodoma, lakini *TAZARA* mmeisahau. Tatizo ni nini? Hii *TAZARA* inapita hata Selous, watalii walikuwa wanatoka Dar es Salaam wanakwenda kwa treni mpaka Mlimba, au wengine wanapita kwa barabara mpaka Mlimba wanaingia Selous; lakini leo barabara hakuna, reli yenye haina uhakika. Tatizo liko wapi? Uje na mpango katika kukuza utalii kule Selous ili hawa watalii waje kwa barabara au waje kwa *TAZARA* ili tuone kwamba tunakuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya nimeshazungumza. Kwa ujumla naomba angalia hoja za Waheshimiwa Wabunge, angalia maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Unapokuja na mipango yako zikusanye ujue tatizo ni nini halafu ukija na mpango elekeza kule ambako Wabunge wengi wanaleta maswali Bungeni ili tutatue haya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mengine ya bombardier na nini yatakuja tu, hivyo viwanja vya Chato, hii tumeshakula bogi umetuingizia huku mabilioni ya hela wakati wengine hata maji hatuna, umetuingizia huku mabilioni ya hela, unakopa wakati sisi hapa ultakiwa ukope

turudi vijijini kwetu tuwaambie tumekopa kwa sababu tunajenga barabara, tumekopa kwa sababu tunajenga vituo vya afya, tumekopa ili tujenge zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tungekuwa radhi kabisa kuiunga mkono Serikali kwa kukusanya kodi, tungefunga mikanda kwa sababu tunajua mpaka kufikia mwaka fulani matatizo ya maji litaisha, barabara pamoja na zahanati yataisha, lakini sasa hivi hatujui hiyo mikopo itamaliza tatizo gani. Sisi watu wa Mlimba hatuna shida ya ndege bombardier, hatuna shida ya kiwanja cha Chato lakini madeni hayo yanatupata wote, hiyo si tabia nzuri, acheni. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya umemaliza? Mheshimiwa Salum Rehani, ajiandae Mheshimiwa Janeth Massaburi.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi nashukuru kuweza kupata nafasi hii adhimu ya kuchangia kwenye Mpango huu wa mwelekeo wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia mpango katika nchi hii lazima uwe na vyanzo ambavyo vitawezesha utekelezaji, lakini vile vile utawezesha upatikanaji wa mapto ya nchi hii; lakini vile vile utaonesha taswira ya mabadiliko ya maendeleo. Mimi sina tatizo na mipango iliyokuwemo kwenye masuala ya miundombinu, iko vizuri na tunakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango mkubwa ambao unatazamiwa uweze kuleta mabadiliko chanya katika nchi yetu ni wa uanzishwaji wa viwanda mbalimbali, na hasa hivi ambavyo vimetangazwa na Waheshimiwa Mawaziri katika kila mkoa. Navyo vimejikita kwenye uzalishaji wa kilimo na mazao mbalimbali ambayo tunategemea tuweze kuyachakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hivi vitabu vyote viwili, mwelekeo na mpango wenywewe uliopo bado kama

nchi hatujaonesha mwelekeo thabiti kwenye uzalishaji wetu ukoje. Hakuna *projection*s sahihi ambazo tunalenga kwamba mwaka huu tutaweza kuzalisha mazao kiasi fulani. Kwa baadhi ya mambo tayari tumeshatoa maelekezo na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulikuja tukaishauri hapa Wizara ya Kilimo na Serikali ijikite kwenye uanzishaji wa mbegu mpya za pamba. Leo mikoa ya Kusini tumetoa maelekezo na tunatarajia kama kweli wataweza kufanikisha ule mpango tuliokuwa tumewapa wa uzalishaji wa hekta zile zilizokuwa zimeshatengwa, tutaweza kupata mpaka marobota kwenye 600,000; kitu ambacho kwa uzalishaji uliokuwepo nyuma kilikuwa ni ndoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukija kwenye upande wa mazao ya mahindi, bado Serikali haijaweza kusaidia katika eneo hilli. Mahindl kwetu ndicho chanzo kikuu cha kila kitu; chakula na viwanda ambavyo vimo ndani ya maeneo yetu. Lakini leo bado nchi haijaweza, kuanzia kwenye mbegu tu ambazo tungeweza kuwapa wakulima wetu wakazalisha katika kiwango ambacho kinastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takiwimu za kitafi zinaonesha kuwa asilimia 75 ya wakulima Tanzania waliozalisha mazao mbalimbali wanazalisha chini ya asilimia 30 ya mazao ambayo wangetarajia kuyapata ya asilimia 100. Nina maana gani? Maana yangu ni kwamba kwamba kila wakulima 100 kama ingeweza kuzalisha gunia 40; kwa eka moja mkulima huyu uwezo wake anazalisha gunia 12. Sasa hapa bado hatujajipanga, wakulima wanatumia nguvu zaidi mbegu bora haipatikani, mbolea bora haipatikani lakini vile vile na pembejeo za viuatilifu hazipatikani kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa *ijipange* itie msukumu zaidi kwenye uzalishaji wa mbegu bora, kwenye uzalishaji wa kuhakikisha kwamba tunazalisha mbolea katika nchi yetu. Lakini vilevile Serikali iweze kuhakikisha kwamba viwanda vile vyaa viuatilifu vilivyokuwa vimeanzishwa hapa nchini vizalishe viuatilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi nchi inatakiwa iweze kuwa na maono, kuwe na teknoloji ambayo ndiyo itaweba kututoa katika uzalishaji mdogo kwenda kwenye uzalishaji mkubwa hatimaye kupata bidhaa au *raw materials* kwa ajili ya viwanda tunavyotaria kuvianzisha. Tuna uzalishaji mkubwa wa chai katika maeneo yetu lakini ndani ya masoko ya nje Tanzania ni nchi ambayo inazalisha kidogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii chai sisi tunazalisha kati ya tani 35,000 lakini wenzetu Kenya wao wako kwenye tani zaidi ya 400,000, lakini hizo 400,000 Tanzania sisi tunachangia kuwapa Kenya bidhaa. Mimi niipongeze Wizara ya Kilimo kwa uwamuzi thabiti wa kuanzisha mnada wa chai ndani ya nchi, na hii itawasidia sana Watanzania kile kidogo cha pesa za nje zinazopatikana ziweze kutumika ndani ya nchi. Ile chai illyopo maeneo ya Iringa, Mbeya, Njombe na maeneo mengine kule Arusha na sehemu nyingine itaweba kusaidia sasa kuanzisha soko la minada ya chai kama tunavyofanya kwenye minada ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kama nchi tutaweza kuwashawishi wenzetu wa Malawi, Waburundi Warwanda kuunga katika huu mnada ambao tuliokuwa nao hapa hivyo kuhakikisha kwamba tunapandisha bei ya chai kutoka shilingi 600 kwenda kwenye 1000 na zaidi. Wito wangu ni kwamba Serikali ijikite kwenye vile vyanzo ambavyo tutaweza kuongeza mapato zaidi kuliko kuangali kwenye mambo ya miundombinu tu peke yake. (*Makofii*)

Kuhusu mifugo, Tanzania tunazaidi ya ng'ombe milioni 28 lakini kwa kweli katika uzalishaji wa maziwa hatumo kwenye ramani ya uzalishaji wa maziwa; tunazalisha watani wa lita milioni mbili tu ambazo vile vile hazina takwimu sahihi. Lakini Tanzania nchi moja ambayo inaaagiza maziwa mpaka kutoka Zimbabwe, hii kwa kweli ni aibu. Kitu gani tunachowenza kushindwa kukifanya ndani ya nchi hii kuweza kukauka maziwa na kutengeneza maziwa ya unga? Tukichukua hao *indigenous breed* tuliokuwa nao hatoi lita moja moja tu kwa ng'ombe milioni nane , lita milioni...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Janeth Massaburi, ajiandae, Mheshimiwa Leah Komanya na ajiandae Mheshimiwa Chikota Abdallah. Mheshimiwa Janeth Massaburi bado?

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa huruma, si mwelesi wa hasira mwingi wa rehema ambaye ye ye ndiye amenipa kibali kuwa katika Bunge hili leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu mpewa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Spika pamoja na ninyi Wenyeviti wote. Kwa kipekee vilevile niwashukuru Wabunge wote kwa mapokezi mazuri na upendo waliounesha kwangu. Naomba Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuzidi kuwatetea wananchi wengi wa Tanzania walio wanyonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi, chama chenye kuleta matumaini kwa Watanzania hasa wanyonge kwa kunilea vyema na kunishauri, na hapa nilipo ni Chama changu cha Mapinduzi ndiye mlezi thabitii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu, wazazi wangu, watoto wangu, shemeji zangu, majirani ndugu na marafiki kwa kunilea na kunipa moyo na hasa wakati mgumu nilipoondokewa na rafiki yangu mpenzi wangu Didas Massaburi. Mwenyezi Mungu azidi kumpokea katika makao yake ya milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu mimi nimeona kuna mambo mazuri mengi, lakini si maana kwamba yote ni mazuri tu na ndio maana kuna miaka mitano ya kujisahisha na ndio maana kuna bajeti za kila mwaka, penye mapungufu unajaza, unatoa wazo la kuleta manufaa.

Katika mpango wa miaka mitano (2016/2017 - 2020/2021) wametenga kanda tano maalum za kiuchumi. Kuna eneo maalum la uwekezaji la Bagamoyo hilo liko Mkao wa Pwani, lengo kuu ni kujenga bandari ya kisasa ambayo itaruhusu meli kubwa na eneo hili litakuwa lango kuu la biashara za kikanda na kimataifa, lakini kutakuwa pia na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kituo cha viwanda cha Kurasini Dar es Salaam. Mradi huu pia utaimarisha ushirikiano wa kibiashara kati ya Tanzania na mataifa mengine kupitia uwekezaji katika miundombinu ya kubiashara na ujenzi wa viwanda; huo kumbuka ni Mkao wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu kuna maeneo maalumu ya uwekezaji ya Mkao wa Kigoma. Lengo kuu la mradi ni kuwa na eneo maalumu wa uwekezaji litakalokuwa na bandari huru (*free port*). Kutakuwa na mitaa ya viwanda, kongani za kitalii na kituo cha biashara. Hili limetengwa kutumia vizuri fursa za kijirografia ambayo itaweza kuhudumia nchi za Kongo, Burundi, Rwanda na Zambia. Kumbuka ni Mkao gani huo? Ni Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la uwekezaji Mkao wa Mtwara eneo hili pia kutakuwa na uwekezaji jumla ya hekta 110 ambazo zimetengwa maalum kwa lengo la kujenga bandari huru ambapo kuna kampuni ambazo zinaendelea kufanya utafiti katika eneo lile na vilevile watajenga viwanda, Mkao wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tano ni Mkao wa Ruvuma, kuna uwekezaji wa jumla ya hekta 2030 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa (*heavy industries*)

vitakavyotumia malighafi ya gesi na chuma. Viwanda nya kuongeza thamani na mazao ya kilimo kama korosho na viwanda nya vito vinatoka Mtwara hii ni Mikoa mitano Pwani, Dar es Salaam, Kigoma Mtwara na Ruvuma hii Mikoa yote inatoka Kanda ya Ziwa? Mikoa inatoka Chato? Tusipotoshe wananchi wetu, Watanzania wana akili sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Miradi mikubwa ambayo naona inasemwana sana, mradi wa *Stiegler's Gorge* naona umekuwa ni mjadala mkubwa. Hata hivyo hiki ni chanzo cha nishati ya umeme. Tumesema Tanzania ya viwanda bila umeme hatuwezi kuwa na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna reli. Nakumbuka mimi katika Bunge la mwaka 2005 mpaka 2010 kulikuwa na mjadala wa Bunge kuhusu reli, barabara zinaharibika magari makubwa yanatumia barabara kila mwaka kuna fedha za kutengeneza barabara. Sasa sisi tunashauri Serikali inatekeleza, imekuwa kazil! Shirika la ndege... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, ahsante sana, Mheshimiwa Leah ajiandae Mheshimiwa Chikota.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mpango wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza naomba kwa kuongelea utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kulipa madeni ya wakandarasi wa miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Wakandarasi wamelipwa shilingi milioni 672 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji. Nina amini watakapokamilisha wataenda kumtua ndoo mwanamke na

vijiji vya Lubiga, Itinje, Mwandoya, Igobe, Mwanuzi, Mkoma, Mwamalole na Bukundi vitanufaika na miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nipende pia kuongelea fedha za miradi ya maendeleo. Kumekuwa na upungufu wa kutokuletwa au kuchelewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hili ni tatizo katika takribani Halmashauri zote za nchi nzima. Miradi imekuwa ikitekelezwa nusu nusu au kwa kusucasua au kutekelezwa kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakitekeleza hatua yao ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo Serikali imekuwa ama inaleta fedha kidogo za *CDG* ama kutokuleta kabisa fedha za *CDG* ama kutokuleta kabisa fedha za *CDG* na kusababisa miradi mingi kuwa viporo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Meatu mpaka sasa ipo miradi viporo ya miaka 10, tisa na nane. Halmashauri ya Wilaya peke yake kwa kipindi cha kuishia Juni, 2017 walikuwa na miradi ya viporo ya shilingi bilioni tano na walitenga shilingi milioni mia tano zikiwa ni fedha za *CDG* na mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza. Kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Waziri aweze kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyo viporo. Kama Halmashauri ya Wilaya ya Meatu peke yake tu inadai shilingi bilioni tano, na kwa mwaka mmoja tu imepanga milioni 500; kwa hiyo itachua miaka 10 kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Meatu ilikuwa na tatizo la uvamizi wa wanyama pori katika makazi ya wananchi pamoja na mashamba ya wananchi na kusababisha vifo ama mavuno yao kuliwa na wanyamapori. Hata hivyo sioni jitihada yoyote inayofanywa na Serikali ya kuwafidia wananchi ambao mazao yao yalikuwa tayari kuvunwa lakini yakaliwa na wanyama poli. Naiomba Wizara pia iweke mpango wa kulipa fidia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alisema Mkuu wa Wilaya ambaye ataleta tatizo la njaa latika Wilaya

yake ataonekana kwamba hatoshi; lakini sisi Wilaya ya Meatu wananchi wamejitahadi lakini wanyamapor i wamekula mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu ukamilishaji wa Daraja la Mto Sibiti. Ni muda mrefu sasa wananchi wamekuwa na kiu ya kuona daraja hilo sasa limekamilika. Hata hivyo tangu Septemba, 2016 katika kikao cha ushauri wa Mkoa tulihaidiwa kwamba vyuma vya kufunga daraja hilo vinatengenezwa China, lakini mpaka leo ni mwaka wa zaidi vifaa hivyo havijafungwa na tulihaidiwa kwamba masika hii tutapita. Mimi binafsi nimekuwa mpitaji wa hiyo sioni dalili yoyote ya kukamilika kwa daraja hilo. Binafsi ninaona mradi unaenda pole pole. Kukamilika kwa daraja hilo kutainua uchumi wa Mkoa wa Simiyu hususani katika Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hata vifaa vya ujenzi vimekuwa vikipanda bei kutokana na mzunguko kwamba vipite Shinyanga ndipo vije Mkoani Simiyu, lakini kukamilika kwa daraja hili kutakuwa ni mkombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu elimu ya bila malipo. Tunaishukuru Serikali kwa kuleta mpango wa elimu ya bila malipo. Hata hivyo mpango huu umesababisha ongezeko la udahili kwa wanafunzi na kusababisha upungufu wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Meatu kuna changamoto ya wanafunzi kutembea umbali mrefu mpaka kwenda kusoma na kusababisha mahudhurio kuwa hafifu. Kwa mfano shule ya sekondari Mwamaloe *form one* walianza wanafunzi 78, lakini waliohitimu ni wanafunzi ni 23. Moja ya sababu iliyo sababisha ni umbali mrefu. Kwa hiyo, wanafunzi waliacha shule kwa ajili ya umbali mrefu. Kwa maana hiyo ninaomba shule ya bweni ya Wasichana ya Nyalanja ijengewe uwezo ikiwa ni kuongezewa mabweni pamoja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, Mheshimiwa Chikota, ajiande Mheshimwa Julius Kalanga, ajiandae Mheshimiwa Mwita Waitara.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitaanza na mchango wangu kipengele cha mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji na hasa sehemu ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayofanya katika ujenzi wa barabara katika nchi yetu. Pia kipekee nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuanza barabara ambayo Wabunge wa Mtwara tulikuwa tunaipigia kelele, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala hadi Masasi; barabara yenyeye urefu wa kilometra 210. Sasa hivi mkandarasi yuko site anaanza ujenzi wa kilometra 50 kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara hadi Nnivata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yetu Wanamtware kwamba mpango ujao sasa utaonesha maendelezo ya ujenzi wa barabara hii. Tunatarajia sasa tuone kipande kingine cha kilometra 50 kutoka Nnivata kuendelea hadi Newala na hatimaye tukamilishe kilometra 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa korosho. Tunapozungumzia korosho Tanzania tunazungumzia Wilaya ya Nanyamba, Tandahimba, Newala na Masasi. Takribani asilimia 60 za korosho ya nchi hii inazalishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa wazo la kuanzisha Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*). Wazo hili ni jema, na

wazo hili litaharakisha ujenzi wa barabara ambazo zinamgusa mkulima, zile *feeder roads*. Hapa ninaomba niishauri Serikali yangu, kwanza niwapongeze *TARURA* kwamba wameanza vizuri sana. Kuna Mtendaji Mkuu yupo na Wakurugenzi wake wanaanza kuchakarika kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa barabara za *TARURA* ni takriban kilometra 108,000. Mtandao huo ni mkubwa na tukiendelea na *formula* ile ya zamani wa kwenye *Road Fund* yaani *TANROADS* wanachukua share kubwa kuliko hii *TARURA*, sabini kwa thelathini, *TARURA* watashindwa mara moja.

Kwa hiyo ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapokuja na mpango wa maendeleo wa mwaka 2018/2019 utueleze *TARURA* sasa itapata asilimia ngapi ya fedha za Road Fund na *TANROADS* watapa asilimia ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ningependekeza, kwa sababu mtandao wa barabara wa *TARURA* ni mkubwa, kama nilivyosema ni takriban kilometra 108,000 tufanye nusu kwa nusu; yaani 50 iende *TANROADS* na 50 iende *TARURA* ili ikajenge barabara ambazo mkulima wan chi hii anatumia kila siku akiwa na balskeli, bodaboda akibeba mazao yake na kupeleka shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahuksu matumizi ya gesi. Wasemaji wengi sana wamechangia kuhusu gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi yetu imejaaliwa kuwa na *reserve* kubwa ya gesi, lakini kama walivyosema wachangiaji wengi hatujatumia hii fursa vizuri. Matumizi yake bado ni ya kusuasua. Mwekezaji aliyopo *Mnazi bay (MNP)* ana uwezo wa kuzalisha au kutupa *cubic feet* milioni 136 kwa siku ili zitumike pale Madimba na Mtwara lakini kwa siku tunatumia *cubic feet* milioni 40 tu, kwa hiyo utaona ni kiasi gani yule mwekezajia anazalisha lakini hakitumiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali yangu kuongeza kasi ya matumizi ya gesi; mtumiaji mmojawapo ni kiwanda cha Dangote. Hadi leo pamoja na maamuzi ambayo alitoa Mheshimwia Rais akiwa pale Mtwara, kwenye ziara kwamba Dangote apewe gesi hadi leo kiwanda cha Dangote hakujapewa gesi. Kuna urasimu usio wa lazima, hebu tupunguze urasimu tumpe Dangote hiyo gesi na kiwanda cha Dangote kikipata gesi hata bei ya saruji anasema itashuka mpaka shilingi 8,000 kwa mfuko, na hii itawasaidia Watanzania wetu. Kwa hiyo, naomba Serikali yangu iongeze kasi ya kutataua changamoto ambazo zinakwanza Dangote kupewa gesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukitosha Mpango wa Maendeleo wa mwaka jana ulisema kuna mradi wa kujenga miundombinu ya kusambaza gesi majumbani kwa mikoa ya Mtwara na Lindi, mradi huu hadi leo haujaanza. Nalomba Serikali yangu itoe pesa kwa *TPDC* ili mradi huu uanze. Mradi huu ukianza basi matumizi ya gesi yataongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti. kuna mradi mkubwa wa kuchakata gesi na kuwa kimiminika ule wa Lindi, Mradi wa *LNG*. Mradi huu kila siku tunaambiwa kwamba tupo kwenye maandalizi ya eneo la mradi. Maelezo haya sasa tumeyachoka ni ya muda mrefu tunaomba sasa tuwe na lugha nyingine. Ni mradi mkubwa na naomba Serikali iongeze kasi ya kukubaliana na hawa wafadhili ili mradi huu uanze. Mradi huu ukianza utatoa fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu wa Mtwara na Lindi na vile vile tutaongeza matumizi ya gesi ambapo sasa bado gezi ipo ya kutosha lakini matumizi yake bado ni ya kususua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu maji; hakuna Tanzania ya viwanda bila maji ya kutosha. Tangu mwaka juzi tukiwa Bungeni hapa tumeambiwa kuhusu miradi 17 ya maji ambayo itapata ufadhili kutoka Benki ya India. Miradi hii itanufaisha miradi ya Makonde, Muheza, Njombe na Zanzibar. Hadi leo hii tunaambiwa bado kusainiwa *financial agreement...* (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Julius Kalanga hayupo, nafasi yake itachukuliwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi dakika tano na Mheshimiwa Waitara dakika kumi.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa dakika zangu tano nitachangia mambo machache katika Mpango huu wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, sote tunajua tunaelekeea kwenye uchumi wa viwanda kama kauli mbiu ya Serikali ilivyo, lakini hakuna namna yoote kama walivyosema wachangiaji waliotangulia kwamba tuelekee kwenye uchumi wa viwanda bila kufanya mapinduzi ya kilimo. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwanza tukaboresha kilimo chetu na hasa aina ya kilimo tunachokifanya. Tuna vyanzo vingi, tuna rasilimali nyingi lakini sasa ni namna gani tunatumia rasilimali zile. Wamesema wachangiaji wengi, malalamiko ni mengi, wakulima wamelima mazao mengi lakini hayawezni kuendelezwa na kuweza kusafirishwa ili waweze kuimarisha uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja yangu kwenye eneo hili ni kwamba tuangularie ni namna gani tunavyoweza kutumia rasilimali tulizonazo kuimarisha kilimo chetu nahasa kujenga mfumo wa kilimo cha umwagiliaji. Kanda ya Ziwa kuna Ziwa kwa mfano na maeneo mengine, lakini namna gani tunatumia rasilimali hii ya maji kuweza kutengeneza kilimo cha umwagiliaji tuweze kuzalisha mazao ambayo yanawezni kutumika kama rasilimali kwenye viwanda vyetu lakini hasa kuimarisha uchumi wa wanachi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la afya. Tunapoelekeea kwenye uchumi wa viwanda, tunapojenga mfumo wa kuimarisha uchumi wetu ni vizuri na ni muhumi sana tukaimarisha afya za watu wetu vilevile ili waweze kushiriki kwenye uchumi huu. Lakini namna gani sasa maeneo

yetu na watui wetu tumewajengea mazingira ya kuimarisha afya zetu? Nimepitia mpango huu lakini sioni eneno lolote linaloongelea kuendelea kutoa elimu kwa watu wetu katika kujikinga na maradhi lakini na kuimarisha mazingira ya afya kwenye ngazi za msingi. Tumeongelea kuimarisha Hospitali za Rufaa na Hospitali nyngine za Mkoa lakini tunaweza tukapunguza msongamano kwenye hospitali hizi kama tutaimarisha vituo vya afya na zahanati kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutawekeza nguvu kubwa sana kweye hospitali za *level* ya juu tukasahau maeneo ya chini, bado watu wetu wanapoteza sana maisha kule chini kwa sababu katika ngazi za msingi huku zahanati na vituo vya afya hazina uwezo, wataalam wa kutosha, vifaa vya kutosha kuweza kuimarisha afya zao. Vilevile hawana elimu ya kutosha kujiklinga na maradhi. Kwa hiyo, kwenye mpango huu tuweke kipengele kinachojumuisha kutoa elimu na kuongeza *package* kwa ajili ya kujenga zahanati, kumalizia maboma yaliyojengwa huko nyuma ambayo hayajakamilika ili tuweze kuimarisha afya kwenye maeneo ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneno lingine ni eneno la mawasiliano, kwa sababu hatuwezi kuimarisha uchumi wetu kama mawasiliano kwenye maeneo yetu hayako vizuri. Wamesema wachangiaji waliotangulia, haiwezekani kwamba tujenge uchumi ulio imara kama mazao yanayolimwa hayawezi kusafirishwa kutoka *point* moja kwenda *point* nyngine. Maeneo yetu mengine bado hayako vizuri sana kimawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango huu inaonesha kwamba kuna kuimarisha usafiri kwenye maziwa yetu, lakini bado hatujaimarisha sana Shirika la Meli (*MSL*). Tungeweza kuimarisha Shirika hili tukaweza kuwapa uwezo wa kutosha, watajenga mfumo mzuri sana wa mawasiliano kwenye maziwa yetu na kwa maana hiyo sasa watu walioko visiwani na maeneo mengine yaliyoko pembezoni wanaweza sasa kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko na hivyo

kuimarisha uchumi wa watu wao kimsingi kwenye maeneo yake yaliyo pembezoni. Vile vile kuweka mfuatano wa usafiri wa mazao na watu kwenye mazingira yetu. Bila kufanya hivyo bado huu wimbo wa ujenzi wa uchumi ulioimara utakuw ana kasoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeshauri, pamoja na mambo mengine yote yaliyoongeleta kwenye mpango tuimarishe vilevile Shirika hili la Wakala wa Meli ili kuiweza kuwa na nguvu ya kutosha kuimarisha usafiri kwenye maeneo ya maziwa. Kwa mfano sehemu kama kutoa Ukerewe kuunganisha na sehemu ya nchi kavu, kuna matatizo makubwa sana ya usafiri wa meli, hali ambayo inafanya mazao mengi ya watu kutoka kwenye visiwa hivyo kupotea na kwa maana hiyo kuathiri uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilifikiri niliongelee, wamesema...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Bukwimba

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na mimi niungane na wenzangu wote ambao wanamshukuru Mungu kwa kuponywa kwa Mheshimiwa Tundu Lissu na anaendelea vizuri na afya yake inazidi kuimarika. Lakini nianze na mambo machache ya jumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kwenye vipaumbele hivi vilivyopangwa, nimeona vipaumbele viro kumi, ile kaulimbiu ya Serikali ya Tanznaia ya viwanda *reflect* kwenye vipaumbele. Kwenye mpangilio huu viwanda ni kipaumbele cha kumi, maana yake kwenye mpangilio ni cha mwisho kwa hiyo maana yake ni kwamba inawezekana tunaendelea kuibadilisha hiyo kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo jinginela jumla ambalo nadhani ningemshauri Mheshimiwa Waziri Mpango alipokee ni kwamba mwaka wa jana mpango ulikuja wa mwaka mmoja, na vipaumbele vilikuwepo na mwaka huu vimekuja tena. Tulishauri na mimi ningeomba nirudie tena, kwamba Mheshimiwa Waziri ni muhimu tukubaliane kwamba hivi sisi kama Watanzania, kama Taifa tunaweza kupata kiasi gani kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo? Ukipatikwa ambacho unaweza kupata kutoka *whatever the sources* kama ni nje, ndani, vyovoyote vile tukubaliane ni mambo gani machache ambayo yanaweza kutekelezwa yakakamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na utakumbuka kwenye bajeti ile ilikuwa shilingi triliuni 29.5 lakini haikufika hata asilimia 70 katika utekelezaji wake. Mwaka wa jana tena imekuja shilingi trillioni 31.4 hatutafika asilimia 70 mpaka 80 kwa mwenendo ulivyo mpaka sasa. Sasa maana yake ni kwamba mipango mingi tuliyopitisha itakwama na hiyo kimsingi ndiyo inazua malalamiko mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu la jumla ambao nashauri hapa, inawezekana watu wanapotoa maoni kuna tafsiri tofauti, watu wanaleta hisia za ukanda na nini, lakini ukweli ni kwamba kama kuna mipango, miradi mbalimbali inatekelezwa ambayo miradi hiyo haikujadiliwa kinagaubaga kwa uwazi Bungeni hapa watu watalalmika hakuna namna, yaani hiyo msikwepe. Mwambieni Mheshimiwa Rais wazi kama analazimisha mipango tunayotaka itekelezwe ni hii mliyoleta hapa tukapitisha, mkitekeleza hii hakuna atakayelalamika. Kwa hiyo, watu wasikwepe wasikimbie kivuli chao. Ni kwamba mipango iliyopangwa itekelezwe, kama kuna mapungufu sheria inaruhusu na Katiba inaruhusu tuje tubadilishe mlete maombi inaruhusuwa. Fedha kama ikipungua usitumie kinyemela, rudini Bungeni hapa, lete mapendekezo tutaridhia hicho ndicho ambacho Wabunge wanasema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kumekuwa na kauli mkanganyiko sana na hizo kauli ni jambo la jumla sana.

Kwenye miradi mbalimbali, Mheshimiwa Rais akisema kauli maeneo mbalimbali watu wanashituka kwa sababu Watanzania wanajua kwa mujibu wa Katiba hii Rais anapatikana kwa kura nchi nzima na kanda zote zimemchangua. Kwa hiyo, unapoona kiongozi mkuu wa nchi anakwenda mahali anatamka kauli ya kiupendeleo hiyo watu hawawezi kuishangilia, wataipinga, watalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninyi cha muhimu ni kupokea mambo, mwambieni Mheshimiwa Rais kwamba huyu ni kiongozi wa nchi akizungumza tunataka atoe suluhu na tiba kwa kero za Watanzania hayo mahitaji ya Watanzania, kwa hiyo msikimbie kivuli chenu na wala msilalamike hapa kuna mjadala wa ukanda hakuna ukanda. Maneno yanayozungumzwa aidha na Mawaziri na viongozi mbalimbali na Mheshimiwa Rais yanawagawa Watanzania. Kwa hiyo, mkifuta hiyo kauli, mshaurini kimya kimya ni muhimu abadilishe kauli za namna hiyo, azungumze kama Rais wa nchi. Hayo ni mambo ambayo kimsingi hayana upendeleo wowote myapokee na kuyafanya kazi ni ushauri tu...

MWENYEKITI: Nenda kwenye hoja Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa...

MWENYEKITI: Rais hana upendeleo wowote.

MHE. MWITA M. WAITARA: ...nilisema natoa ushauri wa mambo ya jumla sasa nakwenda kwenye Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya umeme kipaumbele cha kwanza, mimi Mheshimiwa Mpango nakushauri, kwa sababu kumekuwa na mpango wa umeme wa *REA* na Watanzania wote na Wabunge wote wanasubiri umeme utekelezwe; umeona kuna malalamiko hapa wanasema wakandarasi walitangazwa lakini baadhi ya maeneo hawaonekani tena, walizindua miradi haijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu litekelezwe likamilike kila mahali, kwa maana ya nchi nzima. Hauwezi kuzungumza habari ya viwanda; yaani umeme kwa matumizi ya kawaida haujakamilika, haupo maeneo mengi ni giza, kwenye shule ni giza. Kuna visima vyta maji vimechimbwa maeneo mbalimbali hauwezi kutumia maji kwa sabbau hakuna umeme na hakuna uwezo wa kununua jenereta. Pelekeni umeme wa kawaida kwanza halafu hiyo ziada iende kwenye viwanda, watu watakuwelewa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni ujenzi wa miundombinu. Hawa Wabunge wanasesma kuna maeneo ambayo mpaka leo Mkoa kwa Mkoa haujaunganishwa, Wilaya kwa Wilaya haijaunganishwa, hilo jambo limezungumzwa mara nyingi. Kama unazungumza habari ya ujenzi wa miundombinu nendeni mkamilishe uhakikishe kwamba Mkoa kwa Mkoa kuna mawasiliano ya kutosha, Wilaya kwa Wilaya halafu uhamie kwenye ajenda nyingine msiguse guse hapa na pale mnahama mnaacha viporo vingi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la mifugo. Kumekuwa na malalamiko, kwa kweli hii ni lana kubwa katika Taifa hili. Watu wote hapa mnategemea kula nyama na mifugo kwa kweli ni mali kubwa sana. Viatu ni humo humo, ni kila kitu lakini inawezekanaje sasa hivi mtu akiwa na mifugo inaonekana kama ni uadui? Yaani kuna ugomvi mkubwa kati ya wakulima na wafugaji. Hakuna malisho ya wanyama, hakuna mahitaji muhimu katika maeneo yale, mifugo inakufa, mifugo inachomwa na hili jambo mnalifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mfano pale Dar es Salaam kuna mnada mkubwa sana wa Pugu ambao unaitwa mnada wa kimataifa, lakini ukienda katika eneo hili ukimwambia mtu wa kawaida kwamba ni mnada wa kimataifa hawezi kukuelewa. Hata kama lile ndilo eneo pekee ambalo Dar es Salaam wanalitumia kwa nyama lakini ni eneo la hovyo. Hakuna josh, hakuna mabwawa, hakuna

vyoo, hakuna uzio, ratiba haijulikani, rushwa nje nje! Sasa mambo haya ukiyazungumza watu wanasesma kwamba labda ni kuituhumu Serikali, si kuituhumu Serikali tunasesma ili mkayafanyie kazi, mkaarekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ugomvi mkubwa kati ya wafugaji na wakulima, ugomvi kati ya wafugaji na hifadhi za wanyama. Wale watu wa hifadhi wanachukua mifugo ya wananchi, wanaitoa nchi kavu wanapeleka kwenye mapori, wanawatoza fedha nyingi kweli kweli. Kwa hiyo, mpaka wale wananchi wanaofuga wanaona kwamba kufuga ni laana wanaamua kuachana na ile biashara lakini watu wa vijijini ng'ombe ndiyo benki yao. Ukitaka kuzungumza hapa elimu mtoto asomeshe hawa ambaao wamekosa mikopo ya Bodi ya Mikopo maana yake mtu kama ana ng'ombe wake atauza ili asomeshe mtoto. Sasa ng'ombe mmechukua, mmewatelekeza, wamekuwa, wanachomwa na wananyang'anywa. Kwa hiyo nadhani jambo hili lazima pia lifanyiwe kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona hapa ni miradi ya maji. Mheshimiwa Kiwanga amesema hapa kwamba Mheshimiwa Waziri unatakiwa uwe na akili ya kawaida, yakiulizwa maswali hapa na wewe Mwenyekiti asubuhi umesaidia maswali mengi kwenye upande wa maji ni kwamba kama watu wanahoji sana maana yake maji ni shida karibu kila kona. Ukipensa hivi Mbunge wa Dar es Salaam Ukonga utafikiri kuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kuna watu mpaka leo wanachota maji kwa kutumia zile kata, mvua ikinyesha ndiyo maji wanayokunywa. Sasa jambo hili limekuwa wimbo wa kila siku. Mheshimiwa Mpango wewe kama Waziri /legacyako itakuwa ni nini? Tuambie basi angalau katika mpango huu umeweka miradi ile yote ya maji ambayo imeanzishwa ikamilike, uibue miradi mingine mipya, Wabunge wakija hapa tuache kupiga *story* ya maji kila siku kama watu ambaao hatuna uelewa, tuzungumze jambo lingine. Ile miradi mliyoanzisha kamilisheni, ile miradi mikubwa angalau basi mwaka ukiisha utuambie mimi kama Waziri wa Mpango na

timu yangu nimetekeleza mpango huu umekamilika tukose maswali. Hilo nafikiri ukilifanya utakuwa umetenda haki sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kila mwaka, kila Mbunge hapa, hakuna Mbunge ambaye halilii maji katika eneo lake, umekuwani wimbo wa Taifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango utusaidie, pangeni vipaumbele, kilio cha Wabunge kipokee, tekeleza ili maneno humu ndani yaweze kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, susla la utawala bora. Mimi nilikuwa nataka nishauri, maendeleo haya hayawezi kuja kama kuna hofu katika Taifa, kama watu hawana amani katika shughuli zao, kama mtu anafunga duka. Hivi ni mfanyabiashara gani mjinga ambae atakwenda kukopa mkopo wa Benki, afungue biashara halafu mwanaume mmoja anasema kuanzia leo funga maana yake ukifunga duka lake akafungwa na ye ye hawatawekeza Mheshimiwa Mpango, na wewe unajua ni mtaalam, hawatawekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna watu ambao ni *very sensitive* kama matajiri ambao wana fedha zao. Nataka mahali ambapo kuna amani, utulivu na kuaminiana, anakuwa *confortable* na anawekeza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Taifa hili utawala bora na demokrasia imekuwa ni shida. Sisi hata haya mambo tunayozungumza hapa tukitaka kukosoa tu kwamba data hizi si za kweli, Pato la Taifa *figure* hizi si za kweli unaambiwa ukamatwe uwekwe ndani. Sasa lazima tujadili, maendeleo ni pamoja na demokrasia, maendeleo maana yake ni uhuru wa kuzungumza, kupokea maoni. Kama mnafanya kazi nzuri kwa nini mnakamata watu? Kwa nini watu watishiwe maisha? Kwa nini watu wapigwe risasi? Kama kunafanya maendeleo, sisi tuachenii tuseme tunavyosema bila kuvunja sheria, bila *ku-personalize* mambo halafu ninyi mtende kazi. Muwaambie ninyi CHADEMA, CUF mlikuwa mnapiga kelele sisi tulitekeleza hiki na hiki, tushindane kwa namna hiyo. Fanyeni kazi tukose hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hoja zipo nyingi kweli kweli tunazoweza kuzijibu. Hoja zipo na hazina majibu, ni kwa sababu ninyi mna-concentrate kutushughulikia hapa, ni muhimu huu utaratibu uishe. Wekeni uhuru wa kutoa maoni, tukosoe Serikali, tukosoe mipango ya Mheshimiwa Mpango halafu mkatekeleze mtuambie ninyi mlipiga kelele sasa sisi tumefanya moja, mbili, tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya bure, bahati nzuri mimi ni mwalimu kitaaluma. Hili jambo ni jema, wanafunzi wameandikishwa darasa la kwanza wengi sana. Sasa shida iliyopo umezuka ugomvi sasa katika ya wazazi na walimu. Serikali ilisema elimu ni ya bure sasa...

(Hapa kkengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante!

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti haya lakini ilikuwa bado.

MWENYEKITI: Ahsante dakika kumi zimekwisha. Waheshimiwa Wabunge zimebaki dakika 45 ni za Wabunge watatu wa CCM, wamekubaliana kugawana muda. Kwa hiyo Wabunge ninaowataja sasa wajiandae tutaanza na Mheshimiwa Bukwimba, ajiandae Mheshimiwa Musa Ntimizi, Mheshimiwa Mipata, Mheshimiwa Jitu, Mheshimiwa Kanyasu, Mhesimiwa Dau, Mheshimiwa Kigua, Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Maige. Tunaanza na Mheshimiwa Bukwimba kwa dakika tano.

MHE. LOLEIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Mpango wa Taifa mwaka 2018/2019. Kabla ya hapo kwanza nianze kwa habari ya uwanja wa ndege wa Chato. Mimi binafsi napenda kusema kwamba Chato iko Geita na Geita kuna watu lakini na kanda yote ile kuna watu, kwa hiyo tunahitaji huduma ya kiwanja cha ndege. Kwa hiyo, Serikali haijafanya makosa kujenga kiwanja Chato kutokana

na shughuli za kiuchumi zilizopo kule. Sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla tunahitaji kuwa na kiwanja tena kikubwa zaidi ya hicho. Kwa hiyo, niombe Serikali iendelee kuwekeza fedha zaidi ili kuwezesha ujenzi wa hicho kiwanja cha Chato kwa sababu kitawezesha wananchi wote wa Geita, Kahama pamoja na sehemu mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma tulikuwa tunatumia uwanja wa Mwanza. Uwanja wa Mwanza ni mbali na wakati mwingine kuvuka feri pale unaweza ukakuta feri haipo kwa hiyo unaweza ukachelewa hata ndege. Sasa hivi kwa kuwa na kiwanja Chato kinaturahisishia maisha. Na sisi ni Watanzania vilevile kama Watanzania wengine ambao wana viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ujenzi wa jengo la *TRA* kule Chato. Mimi nadhani tunatakiwa kujenga vitu vya viwango. Kwa hiyo, mimi niipongeze *TRA* kwa kujenga jengo zuri katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende sasa katika Mpango. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kutuletea Mpango mzuri. Kwa upande wa barabara nilikuwa naangalia jinsi ambavyo wamejikita kuangalia miundominu muhimu kwa ajili ya kuwezesha uchumi wa kat, kulingana na Sera ya Taifa, kwamba tumejipanga kuwa na uchumi wa kat mpaka kufikia mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo nilikuwa napenda kupongeza kwa upande wa barabara. Niombe sasa kwamba kwa upande wa barabara ile Sera ya Taifa ya kusema kwamba tutaunganisha kwa barabara za lami mikoa kwa mikoa, lakini vilevile wilaya kwa mkoa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri tuwekeze fedha nydingi kwenye upande huo ili kuweza kuwezesha kuiunganisha mikoa. Kwa mfano kuna hii barabara ya kutoka Geita ambayo inaunganisha Mkoa wa Shinyanga pamoja na Mkoa wa Geita. Barabara kutoka Geita kuititia Bukoli kwenda mpaka Kahama ni barabara muhimu sana kiuchumi. Kwanza ndio barabara inayotumika

na magari mengi yanayobeba mizigo mbalimbali kwa ajili ya kupeleka shughuli bidhaa kwenye shughuli za madini katika mgodi wa GGM pamoja na wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, ninaomba barabara hii isisahaulike kwenye mpango ujao ili ianze kujengwa kwa sababu ni barabara ya muda mrefu imekuwa siku nyingi inazungumziwa lakini hatuoni utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ili tuweze kufikia uchumi wa katilazima Serikali iwekeze kwenye kilimo. Kwa mfano sehemu ambazo kuna maziwa pamoja na mito tuangalie kilimo cha umwagiliaji. Nikiangalia Getia tumezungukwa na Ziwa Victoria, tuanzishe miradi ya umwagiliaji ili kuwawezesha wananchi kuweza kuwa na vyakula pia kuwa na uwezo wa kupata bidhaa ili ziweze kutumika katika viwanda yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa elimu. Ili tuweze kuwa na Tanzania ya viwanda lazima tuwekeze kwenye elimu. Kikubwa zaidi, kuwianisha na Sera ya Taifa ya kuwa na VETA kila wilaya mkoa. Niombe suala hili Serikali iwekeze kwenye mpango, kwamba kila mkoa tuwe na chuo cha VETA. Kuna wilaya na mikoa mingi ambako hatuna VETA. Kwa kuwa vijana wengi wanahitaji elimu ya VETA kwa hiyo niombe sasa kwenye mipango yetu na bajeti zijazo tuhakikishe fedha zinatengwa kwa ajili ya kujenga VETA katika wilaya na mikoa yote ili kuwawezesha vijana wetu kupata ujuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunatarajia kupeleka umeme kwenye kila kijiji... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako...

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musa Ntimizi ajiandae, Mheshimiwa Mipata, ajiandae Mheshimiwa Jitu.

MHE. MUSSA R. NTIMIZI: Nashukuru kwa kupata nafasi na mimi pamoja kwamba ni dakika tano *at least* nichangie katika Mpango huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Mpango huu mzuri ambao na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunatimiza wajibu wetu katika kuongeza yale ambayo tunadhani yanaweza kusaidia katika kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa Taifa unajumuisha mipango midogo midogo tuliyokuwa nayo katika maeneo yetu, katika wilaya zetu, katika majimbo yetu ndio wanatengeneza mpango mkubwa wa Taifa letu. Mengi yameshazungumzwa lakini na mimi nilitaka niseme mambo machache kwa haraka haraka kwa sababu ya muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia eneo la kilimo. Eneo la kilimo likitengenezewa mkakati mkubwa linaweza kusidia mapato ya nchi yetu, linaweza kusaidia wakulima wetu, linaweza kusaidia wakulima wetu, wakapata mapato yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita katika zao la tumbaku. Serikali lazima, lazima, lazima iangalie Mpango ulio bora wa kuliimarisha zao la tumbaku. Zipo changamoto nyingi; lakini nataka niseme pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali yetu bado zao la tumbaku halijamkomboa mkulima na halijachangia vizuri Pato la Taifa. Kama zao la tumbaku likisimamiwa vizuri linaweza likachinga katika Pato la Taifa kwa kiasi kukubwa sana. Niombe sana Mheshimiwa Waziri katika Mpango wako tuangalie namna ya kupata soko zuri la tumbaku nina hakika kabisa wakulima wetu kule tuna wahamasisha wafanye kilimo ili waondokane na umaskini, wanaweza kuondokana na umaskini kwa kiasi kikubwa kama zao hili la tumbaku litasimamiwa viilivyo vizuri zaidi.

Halmashauri zetu zinategemea sana sana mapato yanayotokana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundominu. Nipongeze kwa kuanzisha TARURA, lakini kama walivyosema watu wengine TARURA inahitaji iwezeshwe kifedha ili kusaidia ujenzi wa barabara katika maeneo yetu. Unapohamasisha viwanda, viwanda hivi vinatakiwa vipate pembejeo kutokana na mazao ya wakulima wetu. Wakulima wanalima vijiji ni barabara ni mbovu, kutoa mazao toka vijiji kuleta katika soko ni tatizo kubwa sana. Tukiimarisha TARURA, malengo yake yakatimizwa sawa sawa, mipango yake ikawa mizuri nina hakika kabisa itatusaidia sana katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la afya, hili tunalizingumza kila siku. Tuweke mpango ullothabiti wa kujenga vituo vya afya katika kila kata katika nchi yetu ya Tanzania. Tunapoimarisha Hospitali za Wilaya na za Mikoa hazitosaidia sana kama hatutoimarisha vituo vya afya katika kila kata, vituo vya afya vitasaidia kupunguza msongamano katika Hospitali za Wilaya na katika Hospitali zetu za Mikoa, hili ni jambo la msingi sana. Katika mpango nimeona tunaimarisha sana Hospitali za Rufaa na za Mikoa. Lakini hazitosaidia sana kama wananchi wengi watakuwa wanatoka katika zahanati zetu wanaenda moja kwa moja kutibwa kwenye Hospitali za Rufaa. Wanatakiwa wakitoka kwenye zahanati waende kwenye vituo vya afya ili kupunguza msongamano katika Hospitali zetu za Wilaya na za Mikoa; hili ni jambo la msingi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu wafugaji wetu. Wafugaji wakitengenezewa mpango ulio bora wataleta pato kwa taifa, viwanda vyetu vitapata bidhaa za maziwa, ngozi na tutapata viwanda vya kutengeneza viatu. Hata hivyo leo wafugaji wanaonekana ni adui katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawa ndio wapiga kura wetu, lakini kama nilivyosema tukiangalia vizuri na

tukawatengenezea mazingira yaliyo bora wafugaji hawa wataleta pato kubwa sana katika nchi yetu na kuchangia katika kuboresha uchumi wetu. Tuwatengenezee mazingira bora ya kufugia badala ya kuendelea kuangaika nao. Kama hawajatengewa mazingira yaliyo bora tutaendelea kusumbuana naona haitotusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimetumia muda wangu vizuri nashukuru kwa kupata muda huo, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mipata ajiandae Mheshimiwa Jitu.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika hotuba yetu ya mpango. Mimi nina maeneo matatu/manne na la kwanza ni kilimo. Tunapoingia kwenye uchumi wa viwanda hatuna namna ya kukwepa kuendeleza kilimo na wachangiaji wengi wameeleza. Manufaa ya kilimo yanaonekana na yako wazi, kwanza ina mchango mkubwa sana kwenye uchumi wa Taifa, lakini pia imewaaajiri Watanzania wengi. Kilimo kinaweza pia kikatusaidia kwenye soko la ndani la bidhaa zinazotokana na viwanda. Kwa hiyo, kwa vyovypote vile hatuwezi kukwepa. Sasa ninavyoona mimi kwenye Mpango huu na Mipango yote iliyopita hatujatia mkazo wa kutosha kwenye kuimarisha kilimo chetu, ninaomba hili jambo lizingatiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sisi Mkao wa Rukwa katika msimu uliopita tumezalisha zaidi ya tani 710,602; mahitaji yetu sisi ni tani 257,553. Kiasi cha mahindi ambayo sisi tumetoa nje ya mkoa na kwa sababu tuna utaratibu wetu kwenye njia zinazotka nje ya mkoa; tumetoa tani 50,189. Ziada tuliyonayo leo ni zaidi ya tani 402,859.

Kwa hiyo nina wasiwasi hata takwimu za Mheshimiwa Waziri; tulikuwa tunaongea nae leo kwamba anasema Taifa lina ziada ya tani 700,000 za chakula kwa sasa ikiwa sisi Mkao wa Rukwa tu tuna tani 402,859.62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi wetu mahindi ndiyo kila kitu. Ndiyo kwenda shule, mahindi ndiyo afya zao na ndio uchumi wao. Kwa hiyo, usipoweka mfumo mzuri wa masoko katika mahindi sisi umetuumiza. Nilikuwa nafikiri kama Taifa tuangalie, kwa sababu uzalishaji wa mahindi utaendelea kuwepo, haiwezekani kila mwaka tunakuja hapa kuzungumza kwa kutoa mishipa minge, kukaza maneno ya hovyo, Wabunge kuweka vikundi vikundi. Lazima kama Taifa mjue kwamba kuna wakulima wa mahindi na mahindi yataendelea kulimwa. Sasa nilazima tuwe na mfumo unaoeleweka, mkaanzisha hata kitaasisi au *NFRA* ikaimarishwa, ikapewa hata mtaji ili iwe inanunua katika maeneo ambayo kilimo kinafanya vizuri halafu baadaye inaweza ikafanya biashara ama nje ya nchi au sehemu ambazo kuna upungufu wa chakula katika mataifa mengine kuliko kuwa na jambo lisilo na majibu ya uhakika kila mwaka. Hii nafikisi si nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha kilimo nina kata yangu ya Nkandasi. Kuna shamba la *Milundikwa State Farm* limenyang'anywa na Jeshi na wananchi sasa zaidi ya 2000 hawana shughuli ya kufanya. Sasa watachangiaje katika Mpango huu? Ninaiomba Serikali itume wataalam wake wakaone jinsi wananchi hawa ambao wamekaa miaka 18 katika eneo hili lakini leo wanakuja kufukuzwa na Jeshi bila sababu za kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waagizeni viongozi wakafanye utafiti waone haki iko wapi kwa sababu eneo hili walipewa kihalali na maandishi yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji. Nimeona Mipango mizuri sana katika ukurasa wa 53 katika kitabu chetu cha Mpango na nimeona pia Wizara inavyojitahidi katika kushughulikia suala hili kwa kipindi hiki, hasa baada ya Bunge kuamua kushughulikia suala hili kikamilifu.

Mheshimiwa Mwneyekiti, dosari niliyoiona ni utoaji wa pesa. Zile pesa ambazo zinapatikana moja kwa moja kutoka

Wizarani, zinazokwenda kwenye Wizara kwa maamuzi ya Bunge zinakwenda vizuri kwenye kusukuma miradi. Lakini zile ambazo zinapatikana kutoka Wizara ya Fedha zinachelewa na hazitusaidii sana kusukuma miradi, hii iangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke vizuri, Wilaya ya Nkasi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Jitu, ajiandae, Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyekiti Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia leo, lakini pia nilpongeze Wizara kwa kuleta Mpango, ni Mpango huu wa miaka mitano ambao tunanyofoa vipande vipande kila mwaka ili kuutekeleza mpango huu. Hakuna cha ajabu na hakuna kitu kipyaa, ni mambo tuliyoyapitisha mwaka wa kwanza tulipoingia Bungeni. Muhimu ni vipaumbele, mimi naona tumepishana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vipaumbele kuna mambo ambayo tungebadilisha, yale ya kusogea huko mbele na yale ambayo tungeanza nayo. Muhimu kabisa katika mpangio huu, na kitu ambacho sijaona kama kimewekwa katika mpango wa mwaka huu ambao tunataka kuutekeleza, (2018/2019) ni suala la utafiti. Hakuna nchi inayoweza kuendelea bila ya kuwekeza katika utafiti katika Nyanja zote, iwe kilimo, mifugo, uvuvi, elimu, sayansi, afya na masuala mengine yote kwa kweli hata bajeti ambayo huwa tunatenga kwenye utafiti huwa inakuwa ni ndogo sana, haitoshi hata kwa kitengo kimoja. Katika vituo 16 vya utafiti vile vifaa vyote sasa hivi vimekaribia kuwa vimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sehemu nyingine ambayo ingeweza kutusaidia sana ni katika masuala ya hali

ya hewa, tungewekeza zaidi huko. Kama tunataka wakulima wetu wanufaika tukiwekeza kwenye masuala ya hali ya hewa, kama ilivyo kwenye nchi za wenzetu unaambiwa kesho mvua itanyesha muda wa saa fulani, hata wakulima wetu, mimi ninaweza kwenda kupanda mbegu leo kwenye udongo wakati mkavu lakini nina uhakika wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali ikae pamoja na kuangalia suala zima la uratibu. Hapa kila Wizara inajitegemea kama vile ni Serikali yenyewe; mfanye kazi kama timu. Niwapongeze juzi Mawaziri wannne walipozindua ule mpango wa viwanda kila mkao na viwanda, huo ndio uratibu inatakiwa mkae mfanye kazi kwa pamoja. Tuna mifano mingi, tumechimba visima leo mwaka wa tatu umeme haujafikishwa, lakini ingekuwa mnafanya kazi kwa kuratibu Wizara zote, idara zote zinafanya kazi kwa pamoja miradi ile ingekuwa inatekelezwa na mafanikio yangekuwa yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la kuwa na sera na mfumo wa kodi ambaao ni *stable*, ambaao haubadiliki kila wakati. Mwaka huu tunaweza tukapitisha jambo fulani watu wakaona sera imekaa vizuri na masuala ya kodi, *tax regime* imekaa vizuri mwakani tumebadilisha tunarudisha, hiyo ndiyo inafanya watu warudi nyuma na kwa mfumo huu hatutoweza kuendelea kwenye masuala ya viwanda tunayotarajia kwamba itashika kasi. Ni muhimu viwanda vile vidogo na vidogo kabisa mngevi-regulate; haya mambo ya Osha, *fire*, nani mngewaondoa mtu akishalipa leseni yake na muanzishe *one stop center* kila mkaoa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye sheria mtu asipojua sheria haikupi kinga mahakamani lakini tungekuwa na *center* moja; mimi nikienda uniambie ni kiasi fulani nikilipa masuala mengine yote wao ndio watanielekeza. Kila mkaoa kuwe na *one stop center* watu wafanye kazi na viwanda vidogo na nini kama mlivyo-regulate kwenye uzalishaji mdogo vivyo hivyo fanyeni kwenye viwanda, pasiwe na urasimu mkubwa utakuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kuliko yote pia ni kuwekeza kwenye Benki ya *TADB*. Wakulima hawahitaji kupewa sadaka wala ruzuku, wekeni pesa kwenye benki tukakope na si wajanja wajanja. Wakulima wanaweza kukopa, wakafanya shughuli zao wakalipa hizo hela. Hiyo benki leo haina hela. Mkulima wa kati na wa juu kama anashindwa kukopa pale mdogo atapataje? Kwa hiyo, ninaomba tuwekeze pale na tuhakikishe kwamba benki hiyo inakuwa na mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tukirudi kwenye suala la utafiti ni *cost of production*. Utakuwa na viwanda, lakini kutoekana na utitiri wa hizi *regulatolly bodies* yaani taasisi za udhibiti unakuta tozo zao zinakuwa ni nyingi kiasi ambacho hata tukizalisha gharama ya ile bidhaa yetu siku zote itakuwa juu kuliko bidhaa ambayo unaagiza kutoka nje ya nchi. Leo hii hata mfumo wetu ukiagiza bidhaa kutoka nje nyingi hazina kodi, hasa zinazotoka kwenye nchi za Afrika Mashariki na Kat. Hayo usipoyafanyia kazi hata tukiwa na viwanda hapa bidhaa zetu hazitauzika. Kwa hiyo, ni vizuri ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango mfanyie kazi suala la utafiti ili tuweze kupata... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae, Mheshimiwa Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Kigua.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuzungumzia uwanja wa ndege wa Chato. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini na ninashangaa sana watu wanaoona uwanja wa ndege unaojengwa Geita/ unaojengwa Chato kwamba ni matumizi mabaya ya fedha. Watu wana-*define* uwanja mkubwa kwa urefu wa *runway*,

lakini nadhani wanapungukiwa *exposure*. Uwanja mkubwa ni *facilities* na uwanja ule ili uwe mkubwa ungekuta linajengwa jengo la abiria kubwa, kwa hivyo ndipo ungesema uwanja mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe tu, wamesema uwanja wa ndege uko pale *strategically*, wanasahau kwamba kutoka Chato kwenda Rubondo ni kilometra 30 na tunahamasisha utalii. Pia wanasahau kutoka Chato kwenda Biharamulo ambapo kuna mbuga za wanyama za Buligi pamoja na Biharamulo pale ni kilometra 50. Wanasahau kwamba tuko karibu kilometra 100 kwenda mpakani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaposema ni *strategic airport* watu wengi hawaelewi tunazungumza nini, wanawaza tu kwamba ni uwanja wa Rais kwenda nyumbani. Mimi nasema ule uwanja umejengwa sehemu sahihi na uwanja ule sisi tunauhitaji ungejengwa katika eneo lolote lile. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo jingine ambalo watu ni lazima walifahamu Rais alikuwa akitua Mwanza kwenye uwanja wa ndege wa Mwanza kwenda Chato anatembea kilometra 270 anakwenda kupumzika. Akitua Bukoba anatembea kilometra 250 kwenda kupumzika. Sasa amejenga uwanja karibu anapokwenda kupumzika wanapiga kelele. Mimi nataka niwashauri, *issue* ya ukubwa si urefu wa uwanja, nenda kasome, *issue* ya ukubwa ni *facilities* za uwanja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya *TRA*, jengo la *TRA* watu wanafikiri kurudi nyuma unakwenda mbele unaenda wapi? Badala ya kusema tunajenga jengo likae miaka 50 mbele wewe unawaza kujenga *slope*.

Mimi nasema hata ofisi za Serikali tuache sasa, tuanze kujenga majengo ya ghorofa. Habari ya taa ni habari ya Halmashauri yenyewe hata kama wangepita punda tunaangalia usalama wa raia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la madini. Serikali ilipoanza kusimamia vizuri madini sisi watu wa Geita MJINI tumeona manufaa yake na nataka nitoe takwimu hapa. Kabla ya Serikali kuweka mikono yake kwenye madini, mapato ya Halmashauri yangu Januari-Machi ili kuwa shilingi milioni 514; Aprili-Juni shilingi milioni 750; yakaongezeka kidogo hapo. Ilipofika Julai-Septemba tumepata bilioni moja kasoro, maana yake ni nini? Kulikuwa kuna wizi mkubwa sana unafanyika hapa kwenye madini. Wito wangu hapa kwa Mheshimiwa Waziri ninashauri ufanyike uchunguzi kurudi nyuma kuona kwa nini baada ya Serikali kutuma wawakilishi kwenye hizi kampuni za madini mapato ya Halmashauri yangu yameongezeka kutoka shilingi milioni 500 mpaka shilingi bilioni moja wakati kazi ni ile ile? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, tulipitisha Sheria hapa ya *Local Content*, bado watu wa mgodi wanapiga. Bado wana walinzi kutoka nje, bado wana kampuni nyingi kutoka nje ambazo zinaweza kufanya kazi na Watanzania. Wakati wa Mpango wa mwaka uliopita nilishauri hapa kwamba tuna kampuni nyingi sana ambazo zinafanya kazi kwa *remote*, kampuni iko South Africa, iko Australia, inafanya *services* katika Mgodi wa Geita, hawalipi kodi! Bado halijafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kuwaomba hawa watu watulipe *service levy* wanakwambia hii kampuni haipo Tanzania. Naomba kushauri, sheria hii tulioipitisha hapa Bungeni, yaelekezwe haya makampuni ya madini yaweze kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu tunajenga reli kuja Dodoma, mimi nasema *fine*, tunakopa, tunafanya nini, mimi nasema *fine*, lakini wasiwasi wangu ni mmoja tu, hii reli itakapofika Dodoma kabla haijafika Mwanza itakuwa haina msaada mkubwa kwenye uchumi wa Tanzania. Nataka kushauri, badala ya kufanya vipande vipande kwa muda mrefu ufanyike uamuzi wa mara moja wa kuwekeza reli hii moja kwa moja kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ili itakapokamilika manufaa yake yaanze kuonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mimi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tulipata bahati ya kwenda China na tukaenda katika jimbo moja la Guangdong. Tulipotembelea pale, Meya wa mji ule anatuambia jimbo lile limejengwa na *private sector*, anasema Serikali haijajenga miundombinu katika jimbo lile. *Airport*, barabara, madaraja wamejenga *private sector*. Tuache kukopa kujenga miundombinu, tukaribishe... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Dau, ajiandae Kigua. (*Makofi*)

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na uhai kwa siku ya leo. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa wasilisho lake zuri. Mimi kwa haraka haraka nitaanza na hili ambalo *Senator Ndassa* jana alilizungumza kwa undani sana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa siku nne hapa tumekuwa tukijadili huu Mpango wetu, lakini wengi waliojikita katika kujadili hili wamezungumza suala la ubia katи ya sekta binafsi na sekta ya umma. Sasa mimi sitaki kurudia kwenye mjadala huo kwa sababu mengi yameshasemwa. Huu Mpango na Waziri mwenyewe anakiri kwamba katika hili hatukufanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimuombe tu Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hoja yake pengine Bunge hili linasubiri sana kusikia kauli yake moja tu akisema kwamba anakivunja kile Kitengo cha Sekta Binafsi pale Wizarani. Aweke timu mpya pale, tuanze upya na hata kama ikiwezekana tumtafute mtaalam wa nje aongoze kile kitengo na hili wala sio jambo geni. Tulipoanzisha *TANROADS* lilikuwa ni jambo jipyä, lilikuwa jambo gumu, tukamuweka

raia wa Ghana pale akaanzisha kile kitengo na sasa wenyewe tumeweza kukiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Waziri, vunja Kitengo cha Sekta Binafsi pale kwenye Wizara yako, tafuta wataalam hata kama ikibidi kutoka nje, tuanze upya, haiwezekani huu mwaka wa tano tunaimba tu sekta binafsi, sekta binafsi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hali ya kawaida hata wewe mwenyewe unatakiwa uwe *embarrassed* katika *situation* inavyokwenda sasa hivi. Kila siku tukisoma makabrasha hapa *UDART*! Hivi *UDARTile* kweli unaweza sema kwamba ni mfano mzuri wa ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi? Mheshimiwa Waziri kama ninakuuliza pale, hiyo sekta binafsi mle kwenye *UDART* imeingiza kiasi gani unaweza ukaniilibu? Katika hali ya kawaida zile pesa ni za *World Bank* na yule aliyeingia pale sijui Simon nani sijui ndiyo sekta binafsi pale ni ubabaishaji mtupu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku mimi toka niko Chuo Kikuu nasikia habari ya Chalinze - Dar es Salaam *Road Toll* mpaka leo iko kwenye makaratasii. Sasa anzisha kitengo kile upya, wape malengo walau kwa mwaka basi hata tukipata mradi mmoja mkubwa mimi naamini tutasonga mbele sana. Haiwezekani Chalinze - Dar es Salaam miaka sijui sita, hiyo *UDART* mimi kwangu wala siihesabu kama ni mfano mzuri wa ushirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. Lakini katika hali ya kawaida hata hiyo habari inayoitwa kiwanda sijui ya madawa katika hali ya kawaida hicho nacho pia hakiwezi kuwa ndiyo mfano mzuri. Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana utakapokuja hapa uanze na kuvunja kile kitengo tuanze upya, wape malengo wakishindwa toa weka wengine mpaka tutafanikiwa, hilo liliikuwa la kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimeangalia huu Mpango, kuna eneo umesema eneo la kuimarisha utalii, biashara na masoko, ujenzi na ukarabati wa kutengeneza

miundombinu na kutangaza vivutio vyatya utalii hususan kile kinachoitwa *Southern Circuit*, kwa maana ya kwamba utalii wa maeneo ya Kusini. Mimi nitagusia sehemu ndogo tu. Najua eneo la Kusini ni pana sana, nitagusia Kisiwa cha Mafia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Mafia ni maarufu sana kwa utalii, tuna samaki pale anaitwa potwe (*whale shark*), ni samaki ambaye ni wa ajabu na ni mkubwa kuliko samaki wote ukiondoa nyangumi ambaye si samaki na samaki huyu hajatangazwa. Lakini hata kama mkitangaza bado kuna suala la miundombinu. Kwa masikitiko makubwa sana Bandari ya Nyamisati huu sasa ni mwaka wa pili bajeti ya mwaka 2015/2016 zimetengwa shilingi billioni 2.5 mpaka mwaka umekwisha bandari haijajengwa...

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante! Mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Kigua, Mheshimiwa Shekilindi, tutamaliza na Mheshimiwa Maige. Kama Maige hayupo nafasi yake itachukuliwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru jioni ya leo kwa kunipa nafasi niweze kuzungumzia juu ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi. Waliozungumza wamezungumza lakini nataka tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba ukipitia kitabu hiki mengi ya msingi Mheshimiwa Waziri ameyazungumza ukianzia ukurasa wa 42 mpaka 53 yote ambayo yanayohusu maendeleo ya Tanzania yamezungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye vitu vitatu au vinne tu, ni *Public Private Partnership*. Mheshimiwa Waziri mimi naomba ujikite hapa, tutapunguza matatizo kwa

sababu nchi hii ni kubwa, ina changamoto mbalimbali hatuwezi ku-*invest* kwa kutumia *our own funds*, lazima tujikite kwenye *Public Private Partnership*. Mfano mzuri tu ni Daraja la Kigamboni. Tumeona jinsi ambavyo *return* kubwa inapatikana pale. Kuna usafiri *DART*, yote hiyo ni mifano mizuri. Mimi naomba usipate kigugumizi Mheshimiwa Waziri, hebu tuone namna gani tunaweza kujikita huko zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la *VETA*, naomba mfumo wa *VETA* ubadilike. Elimu inayotolewa kwenye *VETA* ni nzuri sana na tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, lakini elimu inayotolewa si ya kisasa. Tuone namna ya kuwaandaa vijana wetu tuweze kutoa elimu ambayo itasaidia kupata vijana tuweze kuwaajiri katika viwanda vyetu hivi. Ukizingatia viwanda ni vya kisasa, kwa hiyo vitahitaji vijana ambao wanasoma au wanapata elimu yenye *IT base*.

Meshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la viwanda, tunazungumza kufufua viwanda, mimi naamini vile viwanda vya enzi ya Mwalimu Nyerere havifai tena. Viwanda sasa hivi ni teknolojia ya kisasa ni eneo dogo kwa hiyo tujikite kuwa na viwanda vichache lakini ambavyo vitakuwa na tija na nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la bomba la mafuta ambalo linatokea Uganda hadi Tanga. Nimeona katika Mpango huu mmezungumzia namna ya kuweka miundombinu na moja wapo ya eneo ambalo mmeligusia ni eneo la barabara ambalo linatokea Handeni hadi Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kabisa kwamba mpango huu ni lazima utekelezeke kwa sababu njia hii ukiacha bomba la mafuta linapita, lakini pia litasaidia kuinua uchumi wa mikoa minne ya Tanga, Singida, Dodoma. Nimeona niyazungumzie hapa nikiamini kabisa ni maeneo muhimu ambayo yatasaidia kuinua uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kwenda haraka haraka ni eneo la *research and development*. Watu tunazungumza hapa, yamezungumzwa mengi sana lakini naomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha hebu tuwekeze kiasi kikubwa sana kwenye *research*. *Research na development* ndiyo ambayo inaweza kututoa hapa kuona kwamba tubebe yapi tuache yapi na tuwe pia na mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu. Kwa sabbu mipango ni mingi na yote inatakiwa kutekelezeka lakini tukitumia *research and development* maana yake tunaweza tukajua kwamba tuwe na *priority* ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu; hata nchi za China na Malaysia, wenzetu viongozi waliotoka huko mbali walitumia wataalam. Hebu nikuombe Dkt. Mpango na Naibu Waziri hebu kaa na timu, kaa na *panel* ya wachumi uje na mpango mdogo ambao unaweza kututoa hapa Tanzania tulipo na kwenda mbele zaidi. Haya wanayolamimika Waheshimiwa Wabunge ni maeneo ya msingi kabisa na ninaamini mawazo ambayo yanatoka katika maeneo yetu ya uwakilishi yana maana kubwa.

Mimi sipendi kukulaumu lakini naamini kabisa haya ambayo waheshimiwa Wabunge wameyasema yana tija na yana faida kubwa na mimi naomba kupitia wataalam wako, hebu yachukue yafanyie kazi. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Shekilindi, ajiandae Mheshimiwa Maige, nafikiri hayupo, kwa hiyo jиандae Mheshimiwa Bashungwa.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya njema na mimi niweze kuongea katika Bunge lako hili Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote nianze kumpongeza kipenzi cha Watanzania, mtetezi wa wanyonge, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Hii ni tunu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu na kama huamini hilo au kama kuna wale ambao hawaamni hilo basi wangeangalia leo jinsi anavyotoa somo pale Uganda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Waziri Mpango kwa kuja na mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo 2018/2019. Na mimi nijikite katika kuchangia hususan katika kilimo. Hatuwezi kuzungumzia mapinduzi ya viwanda bila kuzungumzia mapinduzi ya kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo katika taifa hili, lakini mimi ninachoamini au nilichoona uti wa mgongo unaelezewa tu kwenye vitabu lakini sio kwa vitendo. Kama kweli tunataka twende kwenye mapinduzi ya viwanda ni lazima tuhakikishe kwamba tunaboresha kilimo chetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima walio wengi hapa nchini wanategemea jembe la mkono. Kwa hiyo, nimuombe sasa Mheshimiwa Mpango, hebu panga mipango yako mizuri sasa kuhakikisha kwamba unaweka mipango mizuri katika wakulima wetu hawa kuwawezesha ili waweze kulima kilimo cha kisasa na kuweza kuzalisha malighafi ambayo itasababisha kujenga katika viwanda vyetu. Ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kuna suala la maji. Maji ni uhai na Tanzania yetu hii bahati nzuri imezungukwa na miito na maziwa makubwa sana. Lakini kuna changamoto sana ya upatikanaji wa maji. Mheshimiwa Waziri Mpango sasa aje na mpango kabambe, naamini kabisa kwenye vitabu hivi kwa kweli mpango wake ni mzuri kuhusu maji lakini apeleke pesa za kutosha katika suala zima la maji kwa sababu maji ndiyo kila kitu. Ukizungumzia kilimo lazima uzungumzie na maji, kwa hiyo naomba sasa katika mpango wake Mheshimiwa Mpango ahakikishe anaandaa pesa za kutosha kupeleka kule kwa wakulima hususan katika suala zima la kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuingie kwenye suala la barabara. Barabara ndio uti wa mgongo, ndiyo uchumi katika taifa hili. Ili uchumi wa nchi hii ukue unahitaji barabara. Kwa mfano kule kwetu Lushoto, kuna barabara ambazo zinatakiwa kupandishwa hadhi lakini mpaka sasa ni miaka mitano barabara zile hazijapandishwa hadhi, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri huyu katika mpango wake huu basi zipandishe barabara zile hadhi. Kuna barabara ya kutoka Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya – Mlingano hadi Mashewa ambapo barabara hii kwa kweli ni barabara ya kiuchumi endapo itafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala tena la barabara kutoka Mombo – Soni – Lushoto – Mlalo – Mlola, barabara hii ni nyembamba mno kiasi kwamba hata juzi mwezi wa nne tulipopata mafuriko kwa kweli wananchi wa Lushoto walipata taabu sana, wallkaa zaidi ya wiki mbili bila kupata huduma za msingi. Kwa hiyo, nimuombe sasa Mheshimiwa Mpango katika mipango yake hii basi apange pesa za kutosha ili barabara ile iweze kupanuliwa. Pamoja na hayo kuna barabara za kupandisha hadhi ziweze nazo kupandishwa hadhi. Pia nimshukuru Dkt. Mpango au niishukuru Serikali yangu kwa kuja na TARURA, Mheshimiwa Dkt. Mpango nakuomba sana TARURA ni jambo zuri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Haya, ahsante na TARURA. Sasa tunakwenda kwa Mheshimiwa Maige, kama hayupo Mheshimiwa Inno.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Mpango wa Bajeti ya Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa wasilisho zuri la Mapendelezo ya Mpango huu na nimtie moyo kwa sababu ameleta Mpango huu ili tuweze kumpa ushauri na naamini kabisa mna muda wa kutosha kuweza kufanya

review kwa ku-take *into account* ushauri ambao tunawapa sisi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ya kipekee walivyoweza kusaidia kutoa *commitment* ambayo iko *serious* kwa Mradi wa Maji wa Rwakajunju kwa Wanakaragwe, nawashukuru sana Serikali. Pia nawashukuru kwa *commitment* ya kuweka lami barabara ya Bugene kwenda Benako ambayo itafungua fursa kubwa sana katika Wilaya yetu na Ngara pamoja na nchi za jirani za Rwanda. Nawashukuru pia kwa *commitment* ya kuweka lami barabara ya Mgakorongo kwenda Morongwa itatufungulia fursa na ndugu zetu wa Uganda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo pia nitumile nafasi hili kuzungumzia suala la uwanja wa Chato. Mimi nadhani wenzetu upande ule wamekosa, hoja kwa sababu huwezi ukatumia muda mahsus wa kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Taifa unazungumzia taa kufungwa kwenye uwanja wa Chato. Taa za shilingi milioni tano unasimama Bungeni unasema Serikali imetumia shilingi milioni tano, yaani ni kukosa hoja kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia jiografia ya nchi yetu na nchi za jirani *East African Communities* na nchi za *Great Lakes* ni sahihi kabisa kuweka uwanja pale Chato kwa sababu lazima tuangalie *future*, tuisiangalie leo. Chato ina *access* ya Ziwa Victoria pale, kwa hiyo, ukiweka *dry port* ya Isaka (bandari kavu), ukaweka *potential* ya kutumia usafirishaji wa maboti ya mizigo kwenda Kenya na Uganda, Chato iko *strategically located* kwa ajili ya kuhudumia mikoa ya kule upande wa Kagera, Geita hata Kigoma, DRC, Burundi na Rwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye siasa tufanye lakini si kwenye mambo ya maendeleo ambayo yako *serious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mpango wa maendeleo ulioko mbele yetu nipende kushauri Wizara ya Fedha, kwamba mfanye *re adjustment approach*. Serikali na nchi yetu, *vision* ya kuwa na uchumi wa viwanda *by 2025* uko *clear* kwa wananchi wetu, kwa wadau wa maendeleo na kwa *private sector* na dunia nzima. Kwa hiyo jambo hilo ni muhimu sana kwa sababu tuna *vision* ambayo tunataka tuhakikishe mpango mkakati unatupeleka kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninachokiona ambacho ni changamoto na muda wa kubadilisha mkakati upo Serikali ime *front load* sana uwekezaji kwenye sekta ya viwanda na biashara moja kwa moja badala ya kuweka *effort* kubwa ya *ku-facilitate* sekta binafsi iwekeze katika viwanda halifu nguvu ya Serikali *m-front load* bajeti kubwa iende kwenye sekta ambazo zinawahusu Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mpango wewe ni mchumi, ukiichukua ile *Douglas Production Function* kwa uchumi wa Tanzania ambao hauko *complicated* mambo ya *financial market, financial derivatives* Tanzania *we have to do the best with what we have*. Tuna ardhi ambayo ni *arable* tunaweza tukafanya kilimo, tuna *labor force* ya kutosha, asilimia 67 ya Watanzania wako kwenye sekta ya kilimo.

Kwa hiyo, tunachohitaji pale ni kuwa karibu na hawa wakulima, wafugaji, wavuvi na kuangalia katika maisha yao ya kila siku zile shughuli ambazo wanazojishughulisha nazo, tTukiwasaidia wakapiga hatua mbili, ile asilimia 67 ya Watanzania ambao wana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: ... itasaidia kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mambo kadhaa ya kuchangia lakini kwa sababu ya muda nina...

MWENYEKITI: Unayo fursa ya kumwandikia Waziri ili akujibu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, orodha yote ya leo imekwisha na kila mtu aliyeandikwa kwenye orodha na vyama vyake wote wamechangia. Niwashukuru na niwatakie kila la kheri. Bunge linarejea.

(*Bunge Lilitrudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Kuna matangazo ndiyo maana nimewaambia mkae. Kawaida inakuwa juu kwa juu tu.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Miundombinu inatakiwa ikutane kesho Jumamosi saa nne asubuhi kwenye ukumbi wao wa Kamati. Kamati ya Bunge ya Miundombinu kesho asubuhi ikutane saa nne asubuhi na mtawasiliana na Makatibu wenu wawaambie ni ukumbi gani mtakutana. Semina ambayo ilikuwa ifanyike kesho haitakuwepo.

Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge mmatangaziwa kwamba mnaalikwa kushiriki katika mbio za *marathon* zinazojulikana kama *Dodoma Marathon 2017* zitakazofanyika siku ya Jumapili tarehe 12 Novemba, 2017. Mbio hizi zitaanza katika uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 12 asubuhi na kuzunguka maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, mbio hizi zinalenga kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli katika uamuzi wake wa kuhamishia Serikali hapa Dodoma. Hivyo basi, Wabunge wote wenye nia ya kushiriki kwenye mbio hizo wanaombwa kujorodhesha kesho Jumamosi saa tatu asubuhi katika eneo la mapokezi lango kuu la kuingilia kwenye ukumbi wa Msekwa.

Basi, tangazo hili tulishasoma toka asubuhi. Kwa hiyo semina ambayo imefutwa ni ya kesho. Semina ya Jumapili iko kama kawaida. Jumapili semina itakuwa saa tano asubuhi, Ukumbi wa Msekwa.

Baada ya maneno haya, katika mjadala hapa jioni liliibuka suala la uwanja wa Dodoma na nikamuuliza rubani na bado nikatofautiana naye nikampa mahesabu akanijibu, mita 3,000 ni kilometra tatu. *Boeing* zinatua lakini kwa Dodoma kwa sasa haitui kwa sababu *effective runway* inayotumika kwa ndege kutua, kwa sasa kwa uwanja wa Dodoma ni chini ya mita 3,000 kwa maana uwanja haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja ukikamilika kwa mita 3,000 ndege hizi zinatua na ni *strategic area*, kwa hiyo nilitaka kuipongeza Serikali kwa hatua hili ya kujenga na kuongeza *length* ya uwanja huu ili utumike kibiashara kwenye *strategy* zingine muhimu za kiulinzi na usalama wa Taifa hili. (*Makof*)

Baada ya maneno haya naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.40 Jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 13 Novemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi*)